## BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 4 Julai, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la kwanza kwa siku ya leo linaelekezwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Ponsiano Nyami ambaye kabla sijamwita, napenda kumkaribisha Bungeni tena. Kwa sababu alikuwa masomoni kwa muda mrefu, kwenye kiti chake hayupo. Basi Mheshimiwa *Capt.* Komba kwa niaba yake amwulizie swali lake.

Na. 136

**Ujenzi wa Zahanati**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA (k.n.y. MHE. PONSIANO D. NYAMI)** aliuliza:-

Kwa kuwa huduma za afya ni muhimu kwa binadamu kama elimu, na mtu anapougua huwa hana uwezo wa kutembea kwa muda mrefu kutokana na udhaifu wa afya:-

(a) Je, kwa nini Serikali inawakataza wananchi wasijenge zahanati katika kila kijiji kama ilivyo kwa upande wa walimu wanavyojenga shule?

(b) Kama ikitokea kwa wananchi wamejenga zahanati na kuzikamilisha. Je, Serikali itakuwa tayari kuwapa huduma bila kujali umbali kati ya kijiji na kijiji mahali zahanati zilipo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa huduma za afya kwa maisha ya binadamu. Lakini si kweli kwamba Serikali inawakataza wananchi wasijenge zahanati katika kila kijiji kama anavyodai Mheshimiwa Mbunge.

Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha huduma za afya nchini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama alivyoelekeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wakati akizindua Bunge hili tarehe 30 Desemba, 2005, ambapo alisema nanukuu: “Serikali ya Awamu ya Tatu imechukua hatua mbalimbali kuboresha Sekta ya Afya kwa lengo la kuinua kiwango cha ubora wa huduma za afya, kuzisogeza karibu na wananchi na kuongeza uwajibikaji wa watumishi wa Sekta hii. Tutaendeleza hatua hizo, tutaendelea kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali zaidi mijini na vijijini, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati alipowasilisha hoja yake hapa Bungeni alilijulisha Bunge lako Tukufu azma ya kusogeza huduma za afya karibu na wananchi. Kwa kuanzia katika mwaka huu wa fedha 2007/2008, Serikali itakamilisha mpango wa ujenzi wa zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya katika kila Kata na itaendelea kutoa mafunzo ya wafanyakazi kwa ajili ya zahanati na vituo hivyo.

Hata hivyo, kwa maana ya mwaka huu wa fedha kazi kubwa itakayofanyika zaidi itakuwa kwanza ni kuimarisha na kuboresha vituo vile vilivyopo sasa kwa kuhakikisha vina wataalam, madawa pamoja na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi huo utakuja kuanza rasmi katika awamu ya 2008/2009 ambapo ndipo hasa kazi ya ujenzi wa vituo pamoja na zahanati utakapoendeshwa. Napenda kutoa wito kwa Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na Viongozi wa ngazi za Tarafa, Kata na Vijiji wawahamasishe wananchi katika kuchangia ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya. Aidha, Serikali itakuwa tayari kutoa huduma bila kujali umbali, suala la msingi ni huduma bora za afya ili kufikia malengo ya milenia ambayo kwa sehemu kubwa yanaelekeza nguvu zake kwenye masuala ya afya.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Nina swali moja la nyongeza. Serikali ina mpango gani kuzisaidia zile Zahanati ama vituo vya afya vya mashirika ya watu binafsi kama ya dini. Kwa mfano zahanati ya Lituhi katika Jimbo la Mbinga Magharibi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Spika, kwa sasa utaratibu wa Serikali ni ule wa kusaidia zile hospitali ambazo tunaziita ni hospitali teule ambao ndiyo jukumu la Serikali katika kuchangia huduma hiyo. Kwa upande wa huduma zilizo ngazi ya chini kuliko hata Wilaya yaani Kata kwa maana ya Vituo vya Afya, lakini vile vile Zahanati

nao ni mchango tu wa sekta hiyo katika kuboresha huduma hii muhimu. Kwa hiyo, kwa sasa tutaendelea kwanza kuweka nguvu zetu katika ngazi ya Wilaya wakati tunajenga uwezo na pengine kutafakari kwa kina zaidi juu ya hatua zinazofaa kuchukuliwa katika eneo hilo.

Na. 137

**Kampuni za Uchimbaji Madini**

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA (k.n.y. MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya hivi karibuni kampuni kadhaa zimewekeza katika uchimbaji wa dhahabu hapa nchini:-

(a) Je, kuna migodi ya dhahabu mingapi hapa nchini?

(b) Je, tangu mwaka 1995 hadi 2007 ni kiasi gani cha fedha kimepatikana kutokana na kuuza dhahabu na taifa letu limepata mapato ya fedha kiasi gani kutokana na mauzo hayo?

(c) Je, tangu mwaka 1995-2007 ni kiasi gani cha mchanga wa dhahabu kilipelekwa nje ya nchi kusafishwa na Serikali ilipata fedha kiasi gani kutokana na mchanga huo na inahakiki vipi thamani ya dhahabu iliyopatikana katika mchanga huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuna jumla ya migodi mikubwa ya dhahabu sita. Migodi mitatu kati ya migodi ya dhahabu iliyopo hapa nchini humilikiwa na kampuni tanzu za *Barrick Gold Gold Corporation* ya Canada. Migodi hiyo ni mgodi wa Bulyanhulu unaomilikiwa na kampuni ya *Bulyanhulu Gold Mine Limited,* Mgodi wa Tulawaka unaomilikiwa na kampuni ya *Pangea Minerals Limited,* mgodi wa North Mara unaomilikiwa na kampuni ya *North Mara Mine Limited.* Migodi mingine ni Mgodi wa Geita unaomilikiwa na kampuni ya *Geita Gold Mine Limited* kwa ubia kati ya kampuni ya *Anglo Gold* ya Afrika Kusini na *Ashanti Goldfields* ya Ghana, Mgodi wa *Golden Pride* unaomilikiwa na kampuni ya *Resolute Tanzania Limited* ya Australia na mgodi wa Buhemba unaomilikiwa na Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kilichotokana na mauzo ya dhahabu kwa kipindi cha tangu mwaka 1995 hadi Machi 2007 ni dola za Marekani 2,614,326,112.21.

Aidha, kwa kipindi hiki taifa letu limepata jumla ya dola za Marekani 78,429,783.36 kutokana na malipo yatokanayo na mrabaha wa dhahabu.

(c) Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba mchanga wa dhahabu unaosafirishwa nje ya nchi kwa ajili ya kuchenjuliwa unatoka katika mgodi wa Bulyanhulu pekee. Migodi mingine haisafirishi mchanga nje ya nchi. Tangu mwaka 2001 ambapo mgodi wa Bulyanhulu ulianza uzalishaji, hadi mwezi Machi 2007 mgodi wa Bulyanhulu ulizalisha tani 160,940 za *gold-copper-silver concentrate* ambazo zilitoa dhahabu yenye thamani ya dola za Marekani 727,126,559, fedha yenye thamani ya dola za Marekani 7,785,885 na shaba yenye thamani ya dola za Marekani 69,327,389. Kutokana na madini hayo Serikali ilipata dola za Marekani 24,127,195 kama mrabaha.

Mheshimiwa Spika, takwimu za mauzo ya dhahabu na mrabaha uliolipwa Serikalini kwa kipindi cha Januari hadi Machi, 2007 si kamilifu kwa kuwa takwimu za mgodi wa Bulyanhulu ni za awali zikisubiri takwimu za mwisho kutoka kwa kampuni zinazofanya kazi ya utenganishaji wa madini ya dhahabu, shaba na fedha yaliyomo kwenye mchanga uliosafirishwa nje ya nchi.

Takwimu za mwisho za dhahabu inayotoka kwenye mchanga unaosafirishwa nje ya nchi kwa lengo la kutenganisha dhahabu, shaba na fedha huchukua hadi miezi sita kukamilika.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakiki kiasi cha madini ya dhahabu, shaba na fedha iliyomo ndani ya mchanga huo kabla ya mchanga huo kusafirishwa Wizara huchukua sampuli ya *gold-copper-silver concentrate* kutoka kwenye makontena na kuzipeleka maabara. Matokeo ya maabara hutumika kukokotoa mrabaha wa awali ambao hulipwa kabla ya mchanga kusafirishwa nje ya nchi kwa uchenjuaji.

Baada ya uchenjuaji kufanyika, matokeo ya uchenjuaji huo hutumwa Wizarani ili kulinganisha matokeo hayo na yale yaliyofanywa awali na Wizara. Baada ya matokeo ya uchenjuaji kampuni hulipa tofauti ya mrabaha.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Ahsante Mheshimiwa Spika kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza. Katika migodi aliyoitaja inaonekana wawekezaji wake na wabia wake wote ni wa kutoka nje. Na ili nchi iweze kufaidika au Watanzania waweze kufaidika ni vizuri kuwe na mikakati ya kuwawezesha Watanzania nao wawe wabia. Je, Serikali ina mkakati gani kuwawezesha Watanzania katika migodi inayofuata waweze kuwa wabia na tuweze kufaidika?

Pili, ametaja Mgodi wa Bulyanhulu. Kuna utaratibu wa migodi sasa hivi kutoa dola laki mbili kwa Halmashauri. Mgodi wa Bulyanhulu tundu la uchimbaji liko mpakani mwa Geita na Kahama, lakini unatoa fedha dola laki mbili kwa Kahama, na eneo la uchimbaji sehemu kubwa iko Geita. Serikali inasemaje kuhusu suala hilo. Je, itatoa fedha kwa Halmashauri ya Geita? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza tuna mikakati mingi ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanashiriki katika uendelezaji ama shughuli za uchimbaji katika migodi ama madini au rasilimali zilizopo Tanzania. Mojawapo ya mikakati ni ule ambao tumeutaja kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 mpaka 2010 kwamba kupitia Shirika letu la *STAMICO* Serikali ina mpango wa mpango wa kuweka mkakati ambao kwa kutumia Shirika hili tutakuwa tunaliwezesha kuingia ubia na makampuni mengine ama wawekezaji wa ndani lakini hata wa nje ya nchi. Hilo ni moja.

Lakini la pili, ni kutenga maeneo mahsusi kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Zoezi hili limekuwa likifanyika na sasa hivi takriban miezi sita tunafanya na ni maeneo mengi ambayo yameshabainishwa mwaka huu. Lakini pia kuna maeneo ambayo yalikwishabainishwa kabla ya hapo. Yakiwemo baadhi ya maeneo ambayo yako kwenye jimbo la Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, maeneo ya Lwamgasi ambayo anayafahamu vizuri ni Nyarugusu ambayo tayari tumekwishayatenga. Haya yalikuwa kwenye leseni za wachimbaji wakubwa, lakini mkakati huu tunao tumeongea na wawekezaji wakubwa hawa ambao ni wa kigeni tumekubaliana baadhi ya maeneo wayarejeshe kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Tuna mikakati mingi ambayo inaendelea. *(Makofi)*

Suala la pili tunafahamu kwamba tundu kama anavyosema liko upande wa Wilaya ya Kahawa. Hatuna hakika kama kweli mgodi huu sasa hivi umeshafika eneo la Wilaya ya Geita ambako Mheshimiwa Rwilomba ni jimbo lake la Busanda lipo. Tunapokea ushauri huo, tunapokea hiyo changamoto. Ni jambo ambalo tunalifanyia kazi na taarifa tutaipata baada ya kujiridhisha kwa utafiti wa kitaalam. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mchanga unaosafirishwa kwenda nje una madini mengi. Serikali inaweza kulieleza Bunge lako Tukufu ni lini mchanga huo unaweza ukachambuliwa hapa hapa nchini ili kuepuka udanganyifu ambao unaweza kutokea? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nitoe ufafanuzi kuhusu mchanga unaosafirishwa nje ya nchi ambao unakuwa na madini. Ni mchanga unaotoka kwenye mgodi mmoja tu wa Bulyanhulu hapa Tanzania. Mchanga unaosafirishwa ni kutoka kwenye mgodi wa Bulyanhulu. Na niseme tu kwamba hii imetokana na kwanza tumekosa ama wawekezaji wamechelewa kuja kuwekeza viwanda ambavyo vingeweza kuwezesha jambo hili kufanyika hapa kuchenjua kwa maana ya kutenganisha mchanga wenye dhahabu na mchanga huo. Kwa sababu za kijiolojia mchanga wa Bulyanhulu unahitaji kuchenjuliwa kwa kiwango kikubwa kwa sababu unakuwa umechanganyika na madini mengine ya shaba na fedha.

Lakini ni lini kwamba tutakuwa na viwanda ambavyo vitaweza kuchenjua ama kutenganisha mchanga huo na madini yaliyomo ndani. Kwa kweli jambo hili ni la kisera. Sera yetu inaruhusu wawekezaji binafsi na kama tunavyofahamu kwa kiasi kikubwa Serikali imeshajitoa katika kuendesha shughuli za kibiashara. Mimi naomba nilishauri Bunge letu hili Tukufu kwa niaba ya Waziri wangu pia wananchi kwa ujumla

na tunafahamu tuna wawekezaji nina hakika hapa Bungeni wapo tuwakaribishe, ni mtaji mkubwa unahitajika kuwekeza kujenga kiwanda cha namna hiyo. Mchanga sasa hivi unapelekwa nchi za Japan na China lakini tunaomba tuzidi kuwahamasisha wawekezaji waje ili wajenge viwanda, pamoja na kwamba Serikali inafanya juhudi kuwashawishi wawekezaji waje. *(Makofi)*

Na. 138

**Mikataba ya Madini**

**MHE. BINILITH S. MAHENGE** aliuliza:-

Kwa kuwa sekta ya madini ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa Tanzania na kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Nne ilikiri wazi kuwa kuna haja ya kupitia upya mikataba mbalimbali iliyowahi kupitishwa katika sekta hiyo:-

(a) Je, Serikali imeishaanza kupitia mikataba kama ilivyoahidi?

(b) Kama jibu ni ndiyo. Je, Serikali imeishapitia mikataba mingapi mpaka sasa na imebaini kitu gani katika mikataba hiyo?

(c) Kama jibu ni hapana. Je Serikali itaanza kupitia upya mikataba katika sekta hiyo ili kutimiza ahadi yake?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Binilith Santano Mahenge, Mbunge wa Makete, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ya Awamu ya Nne iliona kuwa kuna haja ya kupitia upya, mikataba kufuatia malalamiko kutoka kwa wananchi, Waheshimiwa Wabunge na Wadau mbalimbali kuhusu mchango wa sekta ya madini katika uchumi wa Taifa. Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, katika hotuba yake ya Mei Mosi, 2006 mjini Shinyanga, aliiagiza Wizara ya Nishati na Madini kuunda Kamati ya kupitia mikataba ya madini ili kuhakikisha kuwa pande zote mbili, Taifa kwa upande mmoja na wawekezaji kwa upande wa pili zinanufaika ipasavyo na wakati huo huo Tanzania inaendelea kuwa na mazingira ya uwekezaji yanayovutia na ya ushindani kimataifa.

Kutokana na agizo hilo, Wizara yangu iliunda Kamati iliiyoshirikisha wajumbe Mazingira; Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Wizara ya Fedha; TAMISEMI, Wizara ya Sheria na Katiba; Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST);* Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* na Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO).* Kazi ya kupitia mikataba ya madini ilianza rasmi tarehe 10 Mei, 2006 na kukamilika tarehe 8 Julai, 2006. Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa kazi ya kupitia

mikataba kulifungua milango ya kuanza kwa majadiliano baina ya Serikali na kampuni zenye leseni za uchimbaji mkubwa wa dhahabu ambazo zina mikataba na Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali Na. 83 la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, hapa Bungeni tarehe 25 Juni, 2007, Serikali ilishakamilisha zoezi la kupitia mikataba yote mitano ambayo iliingia na kampuni za uchimbaji mkubwa wa dhahabu.

Mikataba hiyo ni kati ya Serikali na Kampuni ya *Bulyanhulu Gold Mine Limted* inayomiliki mgodi wa Bulyanhulu ulioko katika Wilaya ya Kahama; *Pangea Minerals Limited* inayomilki mgodi wa Tulawaka ulioko Wilayani Biharamulo, *North Mara Gold Mine Limted* inayomiliki mgodi wa *North Mara Mine* Wilayani Tarime, *Geita Gold Mine Limited* inayomiliki mgodi wa Geita katika Wilaya ya Geita na *Resolute Tanzania Limited* inayomiliki mgodi wa *Golden Pride* Wilayani Nzega.

Mheshimiwa Spika, zoezi hilo limebainisha kuwa kuna haja ya kurekebisha baadhi ya vipengele kwenye vivutio vitolewavyo kwa wawekezaji kwa lengo la kuharakisha kampuni hizo kuanza kulipa kodi.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivoyeleza kwenye majibu ya sehemu (a) na (b) Serikali imeishatimiza ahadi yake ya kupitia upya mikataba ya migodi mikubwa ya dhahabu.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa wawekezaji wengi ambao wanatoka nje katika sekta hii ya madini wamekuwa wakitumia muda mrefu sana kwenye suala la utafiti. Serikali itakubaliana na mimi kwamba katika hii harakati ya kupitia mikataba basi kuwe na kipengele kinachoweka ukomo wa utafiti? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa marehemu Baba wa Taifa alichelewesha kwa makusudi uchimbaji wa madini mbalimbali katika nchi yetu kwa nia ya kuwaandaa Watanzania kitaalam na kiteknolojia. Je, Serikali ina mikakati gani sasa hivi ya kuwaandaa watalaam ambao watakuwa wawakilishi wazuri kwenye migodi hii na kutoa taarifa sahihi za uchimbaji wa madini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa ufafanuzi na kwa kweli naungana tu na kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna kila sababu ya kuimarisha ukomo wa vipindi vya utafiti. Lakini ndicho kinachofanyika sasa hivi, kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998 ni kwamba utafiti wa madini wa aina yoyote Tanzania upo katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni ule utafiti wa awali ambao kimsingi leseni inatolewa kwa vipindi vya miaka miwili tu. Hiyo inaitwa *Prospective Lesense with recogonised period.* Hiyo huwa haihuishwi, haina *re-new.* Lakini sehemu ya pili ya utafiti ni ile ambayo

inaitwa *Prospecting lesense* ambayo kwa kipindi cha awali inatolewa kwa miaka mitatu. Lakini pia kuna fursa kama mtafiti hajakamilisha kazi yake ya kuhuisha hiyo kwa vipindi viwili viwili kwa sharti la kwamba kila inapohuishwa asilimia 50 ya eneo ambalo alikuwa analifanyia utafiti inapunguzwa. Kwa hivi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna kila sababu ya kuendelea kuimarisha utaratibu uliopo.

Lakini sehemu ya pili mikakati ya kuwaimarisha wataalam, Wizara inaendelea na kuhakikisha kwamba Kamisheni yake ya Madini inazidi kuijiimarisha. Tuna wataalam sasa hivi siwezi kusema wa kutosha asilimia 100 lakini tuna wataalam wa kutosha kuweza kuendeleza ama kusomea shughuli za madini hapa nchini. Tuna majiolojia waliokamilika na hata mwaka jana tumeajiri wafanyakazi ambao wanahusika moja kwa moja na masuala ya madini kama 20 hivi. Lakini bado pia mtaona katika Bajeti yetu ya mwaka huu tunaomba Kasma, tumeweka Makadirio ambayo yatatuwezesha pia kupata wataalam kwa nia ya kuzidi kujiimarisha katika kamisheni yetu ya madini. *(Makofi)*

Na. 139

**Hitaji la Umeme**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Kwa kuwa umeme ni kichocheo muhimu cha Maendeleo na kwa kuwa hitaji la umeme limekuwa ni lazima sana kwa sasa katika kila eneo la nchi yetu kuliko wakati mwingine wowote, hasa kutokana na Maendeleo ya mawasiliano ya simu za mkononi, Vituo vya Afya, Zahanati na ujenzi wa Sekondari za Kata ambavyo bila umeme ufanisi unakosekana:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kujenga *line* ya umeme kutoka Mtera na kupitia katika vijiji vya Kisima, Chipogoro, Wiyenzele, Mtamba, Rudi, Chogola, Kikuyu hadi Kinusi, ambapo kwa kufanya hivyo itanufaisha Kituo cha afya cha Rudi na Sekondari nne za Kata za Chipogoro, Rudi, Massa na Ipera?

**SPIKA:** Waheshimiwa, tumetoa pole kwa msiba huu kwa namna nyingi sana. Naomba kwenye maswali tusifanye hivyo. Au hata kwenye majibu ya Waheshimiwa Mawaziri. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuvipatia umeme vijiji vya Kisima, Chipogoro, Wiyenzele, Mtamba, Rudi, Chogola, Kikuyu hadi Kinusi na Kituo cha Afya cha Rudi na shule nne za sekondari za Kata za Chipogoro, Rudi, Massa na Ipera inabidi kujenga *line* ya umeme wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 128 kutoka kituo cha kupozea umeme cha Mtera.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa kituo hicho cha kupozea umeme cha Mtera hakina 33 *kv bay* za ziada kwa ajili ya kufanikisha zoezi hilo. Tathmini ya awali inaonyesha kuwa ili kuwaunganishia umeme wananchi wa Ismani, Kisima, Chipogoro, Mtamba, Rudi, Ikuyu, Luhundwa, Chamtumile, Kidenge, Munguwi na Pwaga inahitajika transfoma moja kubwa yenye uwezo wa kupooza umeme kutoka kilovoti 220 hadi kilovoti 33. Aidha, zinatakiwa transfoma 6 zenye uwezo wa KVA 50, transfoma 2 za ukubwa wa *KVA 100,* transfoma 2 za *KVA* 200 na transfoma kubwa moja ya *MVA* 5. Mradi mzima unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 4.3.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa umeme kufika kwenye maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge na itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mtambo wa kuzalisha umeme wa Mtera uko katika Jimbo la Kibakwe Mkoa wa Dodoma. Na sehemu kubwa ya bwawa la Mtera liko katika Wilaya ya Mpwapwa na Dodoma Vijijini, lakini vijiji vinavyozungumza na vinavyotunza bwawa hili na mitambo hii kwa kweli havina umeme. Na wenzetu hapa wanazungumza kwenye madini suala la mrabaha. Je, katika mpango wowote ule hasa ule wa umeme vijijini utakapoanza Naibu Waziri yuko tayari mpango huu unufaishe hasa tunaokaa karibu na mtambo huu wa kuzalisha umeme? Hilo la kwanza.

Lakini la pili kulikuwepo na mpango wa milenia wa kupeleka umeme katika vijiji vya Wota na Pwaga. Lakini ule umeme wa kwenda Pwaga ulisemwa tu kwamba utatoka Kibakwe kuelekea Pwaga.

Je, mpango huu wa milenia utakapokuwa tayari uko tayari Naibu Waziri kuniambia ni vema ukapitia katika vijiji vya Chamtumile, Ikuyu, Luhundwa, Kidenge, Mingui hadi Pwaga kuliko sasa ambavyo inasemwa tu kwamba utaenda moja kwa moja Pwaga kwa kupitia porini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Upande wa swali la kwanza nianze kwanza kumkumbusha habari njema rafiki yangu Mheshimiwa Simbachawene, kwamba utakapoanza mpango wa kusambaza huduma za umeme vijijini kupitia wakala wetu. Habari njema ni kwamba kama tulivyosema kwenye jibu la msingi tayari upembuzi yakinifu umeshafanywa gharama zinafahamika.

Kwa hivi yeye Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa jimbo la Kibakwe, wako sehemu nzuri zaidi kuliko sisi wengine ambao tupo maeneo ambayo yapo ndani ya mpango wa kusambaziwa umeme kupitia wakala wa huduma ya umeme vijijini havijafanyiwa upembuzi yakinifu. Kwa hivi nakubaliana na wewe Mheshimiwa Simbachawene kwamba nitakueleza, Wizara yangu itakueleza muda utakapofika.

Lakini mpango wa *MCC* mpango wa *MCC* unahusu maeneo mengi. Sina hakika na tunadhani si busara kusema kama hatuna hakika kwa jambo hili kama vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vimo.

Lakini nakubaliana na yeye kwamba tuko tayari. Na mimi binafsi niko tayari kwa niaba ya Waziri wangu kuhakikishia kwamba kama mpango huo utakuwa unahusu vijiji alivyovitaja tutamweleza pindi utakapofika na mazungumzo kwa kweli labda hizi ni habari njema ya wafadhili kutoka *MCC* yanaendelea vizuri sana na hivi karibuni mtasikia habari njema. *(Makofi)*

Na. 140

**Kisiwa cha Maziwe**

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya visiwa vizuri ni kisiwa cha Maziwe kilichoko kwenye mwambao mwa bahari eneo la Pangani na kwa kuwa kisiwa hicho kimezama kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira licha ya kwamba ni cha kihistoria, kina mazao makubwa ya viumbe kama vile Kasa na kina mandhari nzuri kwa watalii na wavuvi aina ya Dago:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa wale wote waliokata miti ovyo na kusababisha kisiwa hicho kuzama?

(b) Je, Serikali imefanya utafiti wa kiwango gani kutaka kufahamu kwamba viumbe hao wamehamia kisiwa gani kwa kufanya mazalio yao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Col. Mstaafu Fetel Saad Mgeni, Mbunge wa Bumbwini, lenye sehemu (a) na (b), ninapenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye mwambao mwa bahari pwani ya Pangani kulikuwa na kisiwa kilichoitwa Maziwe. Kisiwa hicho kilikuwa kidogo na hakikuwa na watu ila kilitumika kama dago la wavuvi kutoka sehemu mbalimbali za mwambao mwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matumizi holela katika kisiwa hicho na vitendo vya uharibifu wa mazingira ya bahari, uoto na msitu uliokuwa kwenye kisiwa cha Maziwe ulifyekwa na hivyo kukifanya kisiwa kubaki wazi. Kwa vile ardhi ya Kisiwa hicho ilikuwa mchanga na kwamba kilikuwa tambarare kwenye usawa wa bahari, hivyo nguvu za mawimbi makali ya bahari yalisababisha kisiwa hichio kusombwa na maji na hatimaye kubakia fungu. Eneo hilo huonekana tu wakati wa maji kupwa.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kudhibiti uharibifu, Serikali kupitia Bunge lako tukufu ilitunga Sheria Na. 29 ya 1994, na kuanzisha Kitengo cha *Marine Parks* ambacho husimamia maeneo tete ya bahari ikiwemo Maziwe. Jukumu la *Marine Parks* ni kuweka ulinzi madhubuti wa maeneo yote ya pwani yaliyobainika kuwa na umuhimu wa ee wa kiikoloji na kuyalinda kisheria.

Baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali m a Mheshimiwa Col. Mstaafu Feteh Saad Mgeni lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Hakuna hatua iliyochukuliwa na Serikali kwa watu waliokata miti na kusababisha kisiwa hicho kuzama kwa kuwa watu waliofanya uharibifu huo wa mazingira katika kisiwa cha Maziwe hawakufahamika.

(b) Tafiti mbalimbali zilizofanyika zinabainisha kuwa viumbe na uoto wa asili ndani ya bahari hususan Mwamba wa Maziwe haukuathirika.

Viumbe waliiobainika kuathirika ni Kasa wa kijani *(Green tutle)* na ndege aina ya *Club Plovers* na *Shore birds.* Kasa wa kijani ambao walikitumia kisiwa hicho kutaga mayai wanaonekana kutaga kwenye fukwe za Madete na Saadan; ndege aina ya *club plovers* wanaonekana katika kisiwa cha Mnemba Zanzibar na *Mnazi Bay Mtwara*. Ndege aina ya *shore birds* wanaonekana katika kisiwa cha Maziwe majira ya maji kupwa. Vile vile ndege wa aina hii wanaonekana katika kisiwa cha Sange Pwani, Karange Tanga. Yambe Tanga na ulenge Tanga. Hakuna uthibitisho unaoonyesha kuwa ndege hao ni wale waliokuwa katika kisiwa cha Maziwe. Kuwapo kwa viumbe hawa katika maeneo yaliyotajwa kunatokana na kuimarishwa kwa usimamizi wa mazingira ya bahari kwa njia za doria shirikishi na kutoa elimu ya mazingira kwa wananchi wanaoishi katika hifadhi za bahari.

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu ambayo amenifanya nisiwe na hoja kubwa. Lakini tamuomba suala dogo anisaidie ilivyokuwa kajibu Mheshimiwa Waziri kakubali kwamba uharibifu umefanyika na unahatari ya kuendelea kuharibiwa, ningeshauri, au ningelimshauri Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba umefikia wakati wa kuchukua juhudi na bidii ya kuelimisha suala la mazingira? vinginevyo sisi watu visiwani kuna hatari imetukabana maana vinamalizika visiwa na fukwe nzuri zinapotea.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu msingi kwamba taasisi ya hifadhi za bahari imeanzishwa na kazi yake kusimamia ulinzi katika maeneo ambayo ni tete. Lakini vilevile ushirikishwaji wa jamii, umeanzishwa ili kusimamia rasilimali za bahari. Kamati za Hifadhi na Ulinzi za Vijiji zimeundwa katika vijiji vyote vinavyohusika, vilevile Kamati za Ushauri za Hifadhi zikiwa za makundi mbalimbali pia nazo zimeanzishwa. Vikundi vya kulinda mazingira vya kujitolea vimeanzishwa, lakini zaidi ya yote pia elimu ya mazingira inafundishwa kwa jamii ambayo inaishi katika maeneo haya.

Na. 141

**Matumizi ya Sarafu za Senti, 1, 5 na 10**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa sarafu za senti 1, 5 na 10 zinaendelea kutumika kimaanidhsi lakini hatunazo, ambapo Mashirika au Ofisi za Serikali hutoa bili zinaonyesha deni la madai ya senti, mfano shilingi 559.84 ambapo mteja hulazimika kutoa shilingi 560 na hurudishiwi senti 16 kwa kuwa hazipo; na kwa kuwa ni haki ya mteja kupewa chenji yake:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuamua sasa kwamba, sarafu hizo ziwepo au zisiwepo kuliko ilivyo sasa ili kumwondolea mteja usumbufu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA – (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli sarafu za senti 1, 5, na 10 ziko kimaandishi tu na zimepungua sana katika mzunguko kutokana na hali halisi ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kutoka na mabadiliko ya thamani ya fedha za Kitanzania, safafu hizo zimetoweka katika mzunguko kutokana na kuwa na thamani ndogo sana ukilinganisha na viwango vya bei za bidhaa na huduma mbalimbali nchini.

Katika hali hii Serikali haitegemei kuwa mwananchi anatakutana na malipo yanayomdai kutoa sarafu hizo katika manunuzi ya kila na mahitaji kutoka sokoni, madukani, kwenye ulipaji wa nauli na kadhalika. Hata hivyo, imebainika kuwepo kwa matatizo katika malipo kutoka Serikalini hususani malipo ya riba na gawiwo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaiagiza Benki Kuu kuangalia uwezekano wa kuondoa usumbufu wa malipo yenye senti kwa wananchi. Pia Serikali itahakikisha kuwa amlipo yake yanaendana na sarafu zilizoko katika mzunguko hai wa fedha nchini ili kusiwe na usumbufu kwa wananchi.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuulizwa swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ni jana tu mfanyakazi mmoja wa Dar es Salaam alinipigia simu akilalamika kuwa wateja wake wanakataa kupokea sarafu ya shilingi ishirini ambayo ni sarafu halali.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu wananchi hao ambao wanakataa kupokea sarafu ya shilingi ishirini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, sarafu ya shilingi ishirini ni sarafu halali na inatakiwa ipokelewe kwa malipo

halali. Kama kuna mtu amebainika kufanya hivyo tunaomba Mheshimiwa Mbunge atupatie huyo mtu ili Serikali ifanye utafiti nakuchukua hatua ipasavyo.

Na. 142

**Mizigo Inayoteremshwa Itakapo Bandarini**

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED**) aliuliza:-

Kwa kuwa, wafanyabiashara wengi hubadilisha sehemu za kuteremshia mizigo mara itokapo bandarini:-

Je, ni chombo gani kinachopaswa kufuatilia ili kuhakikisha kuwa katika ubadilishaji huo Serikali haipungukiwi mapato?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rahid Mohamed, Mbunge wa Wawi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, chombo kinachopaswa kufuatilia ili kuhakikisha kuwa katika ubadilishaji wa mizigo Serikali haipungukiwi mapato ni Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA*), na hususan Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa.

Mheshimiwa Spika, mizigo inayofuatiliwa ni ile ambyo imewekewa dhamana na waagizaji. Mizigo hii hailipiwi ushuru mara moja bali hupelekwa kwenye maghala maalumu (*bonded warehouses*) kwa kusindikizwa na maofiza wa Forodha kutoka bandarini. Mizigo ifikapo kwenye maghala, huhakikiwa na maofisa Forodha walio na jukumu la kufunga na kufungua maghala ya dhamana na huhifadhiwa.

Pale mfanyabiashara anapohitaji sehemu au mzigo wote (yakiwemo magari) kutoka kwenye ghala ya dhamana hulazimika kufuata taratibu zote za kiforodha kama zile za mzigo uingiapo nchini na kulipia ushuru na kodi zinazolingana na thamani ya mizigo itakayotolewa kwenye ghala.

Mheshimiwa Spika, *TRA* hufuatilia pia mzigo inayopitia katika Bandari zetu kwenda nchi za nje (*transit goods*). Taarifa ya hali ya mzigo huandikwa kila kituo hadi mzigo unaopita kituo cha mwisho kuelekea nchi husika. Pale inapobainika kuna mapungufu, chombo kilichobeba mzigo huo huzuiliwa na taratibu za kiforodha hufanyika kwa nia ya kulinda mapato ya Serikali.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu lakini nilitaka nipate uhakika katika mambo mawili, la kwanza ni kweli kwamba TRA inafanya jitihada na kwa kweli imeongeza mapato kwa njia ya udhibiti aliyoueleza Mheshimiwa Waziri. Lakini bado kuna taratibu nyingi na katika

taarifa zilizoko ni kwamba *under declaration* katika hatua hii ya kuhamisha mzigo kutoka eneo moja ikiwa pamoja na kwenye *bonded warehouses* kuna *declaration* nyingi.

Je, Waziri atatuhakikishia kwamba sasa udhibiti kamili utaweza kuwekwa ili hatua hii inayotupotezea mapato inaweza kudhibitiwa?

Swali la pili ni hasa katika mizigo inayohusu *transit goods* yaani inayopitia bandarini kwetu nchi za nje. Kwa kuwa katika taarifa ya *audit* iliyowahi kuletwa ndani ya Bunge ilionyesha kwamba mzigo uliokuwa unaenda Zambia umebembwa kontena la futi 40 kwa chombo chenye *registration number* ambayo baadaye iligundulika kwamba ni pikipiki.

Je, tunaweza kupata uhakika kwamba Serikali itaweka utaratibu wa madhubuti kabisa kuhakikisha mizigo hii ya transit, haikwepi kulipa kodi kwa njia yoyote ile ikiwa ni pamoja na udanganyifu unaofanywa na wasafirishaji?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kwanza kuna tuhuma kweli kwamba kuna *under declaration,* na vilevile kuna tuhuma pia kwamba mizigo ambayo inaandikwa kama *transit goods* mara nyingi sio ile ambayo imeandikwa. Wakati Waziri akitoa hotuba yake tulizungumzia kwamba kuna *corporate plan* mpya ambayo imeandaliwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba *TRA* inaweza kukabili matatizo hayo yote. Na *second generation* hiyo inatazamiwa kuanza mwaka huu, ni matumaini ya Serikali kwamba baadaya *second generation corporate plan* ya *TRA* matatizo haya kwa kiasi kikubwa hatuwezi kuwa na hakika na wafanyabiashara, lakini kwa kiasi kikubwa Serikali inaweza ikadhibiti.

Na. 143

**Miradi ya Maendeleo Mikoa ya Pembezoni Kusini**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA (k.n.y. MHE. SULEIMAN OMAR KUMCHAYA)** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais J. M. Kikwete alitamka kwamba, mikoa ya kusini ambayo iko pembezoni mwa nchi ipewe kipaumbele katika miradi ya maendeleo katika miradi ya maendeleo ili nayo iweze kupiga hatua za kimaendeleo:-

(a) Je, hadi sasa, ni miradi gani inayoweza kuelezwa kuwa imefanyika katika kuitikia wito wa Rais wa upendeleo?

(b) Je, Serikali inatambua wito wa Rais wa kupeleka miradi ya upendeleo kwa mikoa hiyo ni ahadi nzito kwa Taifa letu ambayo inatakiwa iwekwe ratiba maalum?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a), (b), (c) naomba kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, malengo mahsusi ya Serikali ni kuondoa umaskini miongoni mwa wananchi. Ili kufikia malengo hayo, Serikali kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, mkakati wa Taifa wa Kuondoa Umaskini (MKUKUTA), Mkakati wa Kurasimisha Mali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 imetekeleza yafuatayo:-

Kupanga mipango na kugawa rasilimali kwa kuzingatia takwimu rasmi zinazotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Kwa mfano takwimu zilizotumika katika taarifa ya Hali Uchumi wa Taifa ya 2006 zilitokana na: Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002, pato la kimkoa, vifo vya watoto walio chini ya miaka 5 na mtawanyiko wa watu (*population density*), Hali ya Umasikini kwa ujumla na ukubwa wa eneo (ukiondoa hifadhi za misitu na maeneo ya maziwa).

Kupeleka madaraka kwa wananchi kwa kupeleka rasilimali-fedha, rasilimali-watu na nyenzo za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kipindi kirefu, Serikali imekuwa na nia ya kuwekeza kwa uwianifu wa kimaendeleo baina ya mikoa. Kumekuwa na maendeleo ya kuridhisha katika utekelezaji wa lengo hili japo bado kuna tofauti kiasi. Kimsingi tofauti zilizopo katika maeneo husika na kwamba mikoa yenye ahueni ya miundombinu imeweza kuvutia wawekezaji kwa urahisi zaidi na hivyo kuwa na kasi katika ukuaji wa uchumi na maendeleo. Aidha, maeneo yenye utajiri wa rasilimali, hususan madini, misitu na samaki yameweza kupata wawekezaji kwa haraka zaidi. Miradi inayoendeshwa katika mikoa ya pembezoni katika kutimiza azma hiyo ya Serikali ni pamoja na hii ifuatayo-:

v Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kibiti-Mingoyo-Lindi-Mtwara;

v Kuendeleza mradi wa uzalishaji umeme kwa gesi ya *Mnazi Bay,* Mtwara Vijijini na kuhakikisha unasambazwa katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma;

v Kuendelea na ujenzi wa Daraja la Umoja kwenye mto Ruvuma ambalo litafungua mawasiliano na kuimarisha ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi rafiki na jirani ya Msumbiji, lakini vilevile baina ya mikoa ya Kusini yenyewe;

v Kuendelea na mpango wa ujenzi wa Barabara ya lami ya Masasi-Mangaka ambayo Serikali ya Japan imeshakubali kuigharimia. Mazungumzo yanaendelea ili Serikali ya Japan isaidie ujenzi wa barabara ya Mangaka-Tunduru. Barabara ya Tunduru-Songea-*Mbamba Bay* itajengwa kutokana na msaada wa fedha za *Millennium Challenge Account* ya *Millennium Challenge Corporation* ya Serikali ya Marekani. Barabara ya

Tunduma-Sumbawanga imetengewa Tshs. 13.1 bilioni kwa mwaka 2007/2008 za usanifu wa kina na ujenzi.

v Kuendeleza juhudi za kupeleka umeme kutoka Makambako hadi Songea na Tsh.9.58 bilioni zimetengwa mwaka 2007/2008.

v Serikali inaendelea na maandalizi ya *Special Economic Zone* katika Mkoa wa Mtwara; na

Mheshimiwa Spika, kama Mwalimu Nyerere alivyofundisha kuwa "Kupanga ni Kuchagua". Na tunapanga kwa sababu rasilimali ni chache kuliko mahitaji, hivyo lazima tupange yapi yaanze kutekelezwa sasa na yapi yafuate baada ya mwaka mmoja, miwili au mitatu na kadhalika. *(Makofi)*
Lazima kama Taifa tutambue kuwa hatuna uwezo wa kutekeleza miradi yote, ahadi zote zilizomo katika ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na ahadi za Mheshimiwa Rais katika mwaka mmoja au miwili kutokana na uhaba wa rasilimali tutatekeleza miradi hii awamu kwa awamu. huu ndiyo msingi wa kupanga maendeleo:-

Mheshimiwa Spika, swali la ni lini Serikali itaanza kupeleka miradi mikoa ya pembezoni halipo kwa kuwa Serikali imekwishaanza kutekeleza miradi kama nilivyoainisha hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hili, Serikali imeamua kutekeleza programu za Kanda za Maendeleo, *(Mtwara Development Corridor*, *Central Development Corridor* na *Northern Development Corridor*) kwa lengo la kuchochea maendeleo ya miundombinu katika maeneo na mikoa ambayo, licha ya kuwa na rasilimali nyingi za kimaendeleo, bado iko nyuma.

Aidha, Serikali imeanzisha utaratibu utakoiwezesha Sekta Binafsi kushiriki katika kuendeleza miundombinu kwa kutumia mfumo wa *Public Private Partnership* (*PPP)*. Juhudi zimeanza za kuunda mfumo muafaka wa kuendesha miradi ya *PPP* na kujenga uwezo wa ndani wa kuishauri Serikali kuweza kufikia mikakati yenye manufaa zaidi katika utekelezaji wa miradi hiyo ya *PPP* hapa nchini.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa mikoa ya Kusini wanategemea sana kilimo na mbolea ndiyo *input* kubwa wanayoitegemea katika uzalishaji, Je, Serikali imefikia wapi mpango wake wakushawishi wawekezaji kuwekeza mradi wa kiwanda cha mbolea katika moja ya mikoa ya Kusini?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, mipango ya kuwezesha ujenzi wa kiwanda cha mbolea iko katika hatua mbalimbali, kwanza kuna fikra au kuna ushirikiano tunajaribu kuujenga kati yetu na mwekezaji maarufu wa Saud Arabia ambayo ameonesha nia ya kuweza kujenga kiwanda cha mbolea hapa nchini.

Lakini vilevile uko ujumbe wa Serikali ya wafanyabiashara kutoka Qwait ambao nao wenyewe wanataka kujenga kiwanda cha mbolea Mtwara kwa kutumia gesi ya Mtwara. Tatizo limechukua muda kidogo lilikuwa namna gani ya kukubaliana bei za gesi hii ili itumike kwa kutengeneza kiwanda, sasa tunaelekea kufikia muafaka. Kwa hiyo, tukifanikiwa tutaweza kupata mradi mmoja mkubwa wa kutengeneza mbolea hapa nchini.

**SPIKA:** Naomba nimpongeze nadhani leo ndiyo mara ya kwanza anauliza swali hapa katika Bunge nadhani.

Na. 144

**Mkataba wa Watu wenye Ulemavu**

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa tarehe 31/03/2007 Umoja wa Mataifa uliridhia Mkataba wa haki za watu wenye ulemavu ambapo nchi 84 wanachama wa Umoja huo ikiwamo Tanzania zimehusika:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani tangu kusainiwa kwa mkataba huo?

(b) Je, ni lini Mkataba huo utaletwa Bungeni ili ujadiliwe na hatimaye kuidhinishwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuandaa Itifaki ya Kimataifa kuhusu Haki ya Watu wenye Ulemavu ulianza mwaka 2001 kufuatia Azimio Na.56/168 la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lililounda Kamati ya Muda wa Maandalizi ya Itifaki hiyo.

Kuanzia mwaka 2002 kumefanyika mikutano kadhaa ya mashauriano ya kikanda hadi kufikia mwaka 2006 itifaki hiyo ilipopitishwa. Kamati ya Muda tayari ilikuwa imekutana mara nane. Mhehimiwa Zulekha Yunus Haji na Waheshimiwa Wabunge kadhaa wenye ulemavu ni miongoni mwa wajumbe walioiwakilisha Tanzania kwenye kikao cha mwisho cha Kamati hii. Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Zulekha na Waheshimiwa Wabunge wenzake kwa kazi nzuri walioifanya na hatimaye kuwezesha kupitishwa kwa Itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Watu wenye Ulemavu ulifunguliwa kwa ajili ya nchi wanachama kuweka saini zao tarehe 30/3/2007. Serikali ilichukua hatua ya kuhakikisha kwamba mkataba huo unasainiwa na Tanzania tarehe hiyo ya 30/3/2007. Baada ya kusaini, hatua iliyofuata ni kuridhia mkataba huo. Nchi yetu imedhamiria kuridhia mktaba huu mapema iwezekanavyo. Ili tuweze kuridhia kunahitaji maandalizi ambayo ni pamoja na mashaurino na wadau na kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ipo katika hatua ya mashauriano na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na wadau wengine ikiwa ni hatua ya kuhakikisha kwamba mkataba huo unawailishwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa mapema iwezekanavyo.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Spika asante sana pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nilikuwa na swali la nyongeza, Je pamoja na Wizara kuuleta mkataba huo hapa Bunge ili uridhie, je, utafuatana na kutunga sheria ya utekelezaji?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ningependa nimponge Naibu Waziri wa Afya kwa majibu mazuri aliyotoa hivi punde. Tunazo Sheria Na.2 na 3 za Mwaka 1982 ambazo zinasimamia huduma kwa watu wenye ulemavu. Hizi Sheria sasa hivi zimepitwa na wakati na tulijibu swali la muongo la watu wenye ulemavu wiki iliyopita, na kusema kwamba tunafanya mapitio ili ziendane na wakati. Hii itifaki itakaporidhiwa basi yale maudhui yataingizwa kwenye sheria yetu.

Na. 145

**Kuimarisha Hospitali za Madhehebu ya Dini**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI (k.n.y. MHE. WILSON M. MASILINGI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, milipuko ya ugonjwa wa Malaria imekuwa ikitokea mara kwa mara baada ya misimu ya mvua na kusababisha vifo vingi vya watoto, akina mama na hata watu wazima wilaya ya Muleba licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali ikishirikisha na hospitali za madhehebu ya dini:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, ni busara sasa kwa hospitali zote za madhehebu ya dini katika mkoa wa Kagera zipatiwe msaada wa fedha, dawa/vifaa waganga na Wauguzi kama ilivyo kwa hospitali Teule za Wilaya ili kuondoa msongamano wa watoto katika hospitali sasa?

(b) Kwa kuwa kituo cha Afya cha Tarafa ya Nshamba bado kinajengwa kwa juhudi za wananchi na mchango wa Serikali. Je, kwanini Serikali isitekeleze Miradi ya Kitaifa

ambayo ina fedha nyingi za kupambana na Malaria, UKIMWI na kifua Kikuu kwa kujenga vitengo vya utafiti na tiba katika kituo hicho cha afya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, napenda kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Serikali imekuwa ikishirikiana na Hospitali za Mashirika ya Dini katika kutoa huduma za afya hapa nchini. Serikali inatoa ruzuku kiasi cha shilingi bilioni 54.5 kwa mwaka wa hospitali 87 za Mashirika ya Dini, zikiwemo zile za Mkoani Kagera, pamoja na Hospitali Teule za Wilaya 20.

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Wilson M. Masilingi Mbunge wa Muleba Kusini lenye sehemu (a), (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mchango mkubwa unaotolewe na hospitali za Mashirika ya dini katika kufikisha huduma za afya kwa wananchi, Serikali imeendelea kutoa ruzuku kwa hospitali za mashirika ya dini ambazo si hospitali Teule za wilaya. Aidha Serikali imekuwa ikiruhusu hospitali hizo zinunue dawa na vifaa vya hospitali kutoka katika Bohari ya Dawa ya Serikali kwa bei nafuu. Pia Serikali imeweka utaratibu kwa Halmashauri za Wilaya kutoa fedha kwa hospitali hizo kama mgao wao wa fedha za *Council Basket Health Grant* ambazo ni asilimia kumi (10%) ya fedha za *Basket* zinazokwenda kwa kila halmashauri. Ili kuzipa fedha zaidi hospitali hizo zimeingizwa katika mpngo wa kuhudumia wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Hii inaziwezesha kupata fedha zaidi kugharimia huduma. Uwezo mdogo wa Serikali ndiyo sababu kubwa ya kutozipatia hospitali hizo fedha zote zinazohitajika kugharamia huduma za afya wanazotoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watumishi Serikali bado inao watumishi wanaolipwa na Serikali lakini wanafanya kazi katika hospitali za mashirika ya dini zikiwemo za Mkoa wa Kagera.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Masilingi kwa jitihada zake za kufuatilia afya jimboni kwake na kuwapongeza vilevile wananchi wa Tarafa ya Nshamba kwa kuwa na moyo wa kujitolea ili wajitegemee. Ni kweli Serikali inatekeleza miradi mikubwa ya kitaifa na yenye fedha nyingi kama alivyoainisha. Kujenga na kuendesha kituo cha utafiti ni gharama kubwa kutokana na mahitaji ya rasilimali za aina nyingi zikiwemo wataalam, fedha vifaa maalum, majengo na kadhalika.

Vituo vilivyopo vimesambazwa katika kanda na kwa kanda ya Ziwa kituo chao cha utafiti kipo jijini Mwanza. Kwa maana hiyo haitakuwa jambo la manufaa makubwa kujenga kituo kingine cha utafiti katika kituo cha afya cha Nshamba. Hata hivyo ili utafiti ufanyike mahali popote nchini sio lazima kuwe na kituo katika eneo hilo, kinachohitajika ni wataalam toka wilayani, mkoani au kituo cha Mwanza kufanya utafiti Muleba na kama

kutakuwa na haja ya kuchukua sampuli basi zinaweza kupelekwa katika maabara ambazo tayari zipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Msafiri, bahati mbaya, leo maswali yamekuwa marefu sana na majibu mengine nayo marefu mno, basi Mheshimiwa Ruth Msafiri, swali fupi!

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza madogo na mafupi.

(a) Pamoja na kuishukuru Serikali kwa kushirikiana na mashirika ya dini ambayo yanatoa huduma ya afya katika Wilaya ya Muleba, Mkoa wa Kagera. Je, Serikali haioni kwamba kiasi inachotoa hakitoshelezi kulingana na mlipuko wa magonjwa unaojitokeza kutokana na wagonjwa kuwa wengi zaidi kuliko uwezo uliokadiriwa na Serikali?

(b) Kwa kuwa suala zima la mwelekeo wa Serikali sasa hivi ni kuimarisha vituo vya afya vilivyopo na zahanati zilizopo kabla ya kuanza kujenga mpya. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba vile vituo vya afya ambavyo vimeanzishwa katika Wilaya ya Muleba vitakamilishwa kwanza kabla ya kuanza kujenga vingine vipya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba wakati wa milipuko huwa Serikali haiachii Wilaya ya Muleba peke yake kuwahudumia wagonjwa wa malaria. Wizara huwa inatuma wataalam ikiwemo pamoja na vifaa vyote vinavyohitajika kama dawa ili kuhakikisha kwamba mlipuko huu unadhibitiwa. Kama kiasi hakitoshelezi wakati ule ambao sio wa milipuko naweza kumwelewa lakini wakati wa milipuko Serikali inakwenda na inatoa fedha za ziada ili kuweza kudhibiti mlipuko huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha vituo vya afya vilivyopo, kama tulivyofahamishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kama tutakavyoelezea pia katika hotuba yetu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, katika mpango wa maendeleo ya afya ya msingi, kabla hatujaanza na ule mpango maalum, kazi kubwa na fedha iliyotengwa katika mwaka huu ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha na kukarabati vituo vya afya, zahanati zilizopo na kuongeza watumishi kabla ya kuanza ule mpango maalum.

**SPIKA:** Mheshimiwa ingawa muda wa maswali umepita nadhani ni haki tu tupate majibu ya swali la mwisho la Wizara ya Usalama wa Raia ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Felister A. Bura.

Na.146

**Umiliki wa Silaha za Moto**

**MHE. FELISTER ALOYCE BURA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliwatangazia wananchi kwamba, wale wote wanaomiliki silaha za moto wazisajili silaha hizo kwenye vituo vya Polisi:

(a) Je, ni silaha ngapi zimeshasajiliwa nchi nzima hadi sasa?

(b) Je, ni changamoto gani ambazo Serikali imekumbana nazo katika kutekeleza zoezi hilo?

(c) Je, katika kutekeleza zoezi hilo, Serikali imebaini upungufu gani uliosababisha kuzagaa silaha za moto?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi iliamua kuzihakiki silaha zote hapa nchini kuanzia mwezi Agosti, 2006 na siyo kuzisajili kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Silaha husajiliwa mara tu mtu au Taasisi inapoomba na kupewa kibali cha kumiliki silaha hiyo.

Mheshimiwa Spika, toka kuanza kwa zoezi la kuhakiki silaha za moto zinazomilikiwa na wananchi hapo Mwezi Agosti, 2006 mpaka mwezi Mei, 2007 jumla ya silaha 52,700 zimekwishahakikiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, changamoto ambazo Serikali imekumbana nazo katika kutekeleza zoezi hili ni kama ifuatavyo:-

· Wananchi wamekuwa wakiazimana, kuuziana na kumilikishana silaha kienyeji kama vile kifaa cha kawaida cha nyumbani kwa sababu ya umri mkubwa wa umiliki au kwa kuwa wao hawahitaji tena kutumia silaha hizo.

· Wananchi wengi wameonekana kutojali leseni zao za umiliki na hata hawajui zipo wapi.

· Imeonekana wazi kwamba wamiliki wengi wa silaha hawazingatii Sheria za Umiliki wa Silaha.

· Baadhi ya wamiliki wameonekana kutoelewa alama muhimu za silaha zao ambazo zinatofautiana na silaha nyingine.

· Baadhi ya wamiliki wanapohama maeneo wanayoishi na kuhamia eneo lingine hawaendelei kulipia leseni zao. Hii inachangia kupoteza kumbukumbu za umiliki wa silaha zao na hata mapato ya Serikali.

**MHE. FELISTA A. BURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Usalama wa Raia, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza zoezi hilo mapungufu yaliyobainiwa na Serikali ambayo yamechangia kuzagaa kwa silaha za moto ni pamoja na:-

· Kugundua kuwa, baadhi ya silaha zilizokamatwa ziliibiwa kutoka kwa wamiliki halali na zingine kuingizwa nchini kupitia mipaka yetu visivyo halali.

· Fomu zilizokuwa zinatumika hazikuwa na dodoso za kutosha ili kuliwezesha Jeshi la Polisi kumfuatilia mmiliki wa silaha hiyo ili kujua namna anavyoitunza na kuitumia silaha yake pamoja na kufuata taratibu zingine kwa mujibu wa sheria za umiliki wa silaha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kubaini mapungufu hayo, Serikali imechukua hatua zifuatazo ili kurekebisha kasoro zilizojitokeza:-

§ Jeshi la Polisi limeanzisha utaratibu wa kuweka kumbukumbu za wamiliki wote wa silaha na aina ya silaha zinazomilikiwa kwenye *computer*. Aidha, zile ambazo zimebainika kuingia nchini kinyume cha sheria, Jeshi la Polisi linazifuatilia kupitia *Interpol*.

§ Jeshi la Polisi limeendesha mafunzo maalum kwa Askari wanaofanya kazi ya usajili, uhakiki na utambuzi wa silaha ili kuwawezesha kutoa elimu kwa wamiliki wa silaha pamoja na kuwawakumbusha taratibu za umiliki wa sialaha.

§Fomu za umiliki wa silaha zimefanyiwa marekebisho ambapo kupitia dodoso za fomu hiyo mpya, Jeshi la Polisi litaweza kumfuatilia mmiliki wa silaha kwa kutumia taarifa zilizopo katika fomu hiyo mpya.

**MHE. FELISTA A. BURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Usalama wa Raia, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a)Je, wananchi wale ambao silaha zao hazikuhakikiwa na wale ambao hawakufuata taratibu za kuuziana silaha, Serikali itawachukulia hatua gani?

(b) Kwa kuwa ujambazi au majambazi bado wanawaua raia wema kwa kutumia silaha za moto, je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuhakikiwa kwa silaha bado haijasaidia kupunguza ujambazi nchini na bado mikakati inahitajika zaidi katika kuhakiki silaha?

**NAIBU WAZIRI, USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, katika kipindi cha mwaka 2001-2006 silaha 9,157 zilikamatwa na watuhumiwa

3,989 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, wale wote wanaokamatwa na silaha kinyume cha sheria hupelekwa Mahakamani kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli uhakiki wa silaha sio mkakati pekee wa kumaliza tatizo la ujambazi na wizi wa kutumia silaha hapa nchini. Hii ilikuwa ni moja tu katika mbinu zinazosaidia. Kama nilivyosema, tumewagundua wengi ambao wanamiliki silaha kinyume na utaratibu na hatua zimechukuliwa. Kwa hiyo, imesaidia kwa njia moja au nyingine kupunguza wizi wa kutumia silaha hapa nchini. Ni mkakati mmojawapo mzuri na kuna mikakati mingine mingi ambayo Jeshi la Polisi linaipanga kupambana na ujambazi hapa nchini.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita kabisa. Nina matangazo na nitaanza na wageni. Ninafurahi kutangaza uwepo nadhani kwenye *Speakers Gallery*, uongozi mpya wa kampuni yetu ya ndege ya Tanzania *(ATCL)*. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Andrew Chenge na nitaomba niwataje. (*Makofi*)

Kwanza, ni Mwenyekiti wa Bodi ya *Air Tanzania Limited*, Mheshimiwa Balozi Mustafa Nyang'anyi. Karibu sana Mheshimiwa. Tunafurahi kukuona tena na karibu nyumbani ili uweze kuongoza shirika hili muhimu sana. *(Makofi)*

Pamoja na Mheshimiwa Balozi Nyang'anyi, yupo Ndugu David Mataka, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo. (*Makofi*)

Kwa haraka haraka sasa niwataje wanaofuata, Ndugu Ajay Gopnacy, Mkurugenzi wa Mauzo; Amini Mziray, Katibu na Mwanasheria wa Kampuni; George Mazura, Rubani Mkuu; Godfrey Mganyizi, Meneja Uhusiano; Paschal Norbert, Mwenyekiti wa *COTWU Airport,* Chama cha Wafanyakazi; Laurence Muhonwa, Katibu wa *COTWU, Airport* na Bonaventura Sagamilwa, Kaimu Mwenyekiti wa *COTWU ATC House. (Makofi)*

Katika kuwakaribisheni, napenda mkumbuke tu kwamba sisi Watanzania tunalipenda sana Shirika letu la ndege na tunataka lifanikiwe. Mimi nikiwa mteja wenu mashuhuri nimeanza kuvutiwa sana na jinsi huduma zinavyozidi kuwa bora zaidi.

Majuzi nikitoka Johannesburg niliongea na vijana na walisema kwamba David Mataka na Balozi Mustafa Nyang'anyi ni kiboko yao, ahsante yao. *(Makofi)*

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** *Gender imbalance*.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna wanawake.

**SPIKA:** Serikali imesikia. *(Kicheko/Makofi)*

Tuendelee. Mheshimiwa Anastazia Wambura ana wageni wake ambao ni baba yake mzazi, mzee James Wambura na mwanawe wa kwanza, Melania Werema, wale pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Feetham Banyikwa, ameniomba nitangaze kuwepo kwa Waheshimiwa Madiwani 23 wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ambao wamefuatana na Afisa Mmoja wa Habari, Radio Kwizera ya Ngara. *(Makofi)*

Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani wa Ngara na hongereni sana kwa kuwa na redio sijui ya Jimbo au ya Wilaya? Hatujaisikia sana hii nadhani masafa yake hayafiki Dodoma. Karibuni sana, tunafurahi sana kuwaona. *(Makofi/Kicheko)*

Wapo pia Wenyeviti 25 wa Serikali za Mitaa na Matawi ya CCM, Kata ya Chamwino ambao ni wageni wa Mheshimiwa Felister Bura. Ahsanteni sana. Ninyi ndio wenyeji wetu hapa, tunapenda kuwahakikishieni kwamba wengi wetu tunafurahi sana kuwa hapa. Ahsanteni kwa ukarimu wenu. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Paul Lwanji ambao ni Madiwani wanne, Mheshimiwa Ally Minja, Mheshimiwa Daniel Manyika, Mheshimiwa Rehema Chizumi na Mheshimiwa Elifasi Lwanji, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Madiwani na wataalam 11 wa mji mdogo wa Makambaku, wao ni wageni wa Mheshimiwa Jackson Makwetta. Nadhani yule mwenye kofia ya aina ya tarubushi, pengine ndio Mwenyekiti. *(Kicheko/Makofi)*

Tunao wanafunzi 75 kutoka vyuo mbalimbali nao ni kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Tumaini, Iringa, Chuo Kikuu cha *Saint Agustine,* Mwanza na Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda. Ningeomba pale walipo wasimame. Wale pale wasomi, karibuni sana. Tunafurahi sana na kipekee, naomba niwakaribishe sana wale wa Makerere Uganda, tunashukuru mmekuja kuangalia Bunge la Tanzania. Kwa wale wenyeji tunawashukuru mmevutiwa kuja kutazama jinsi demokrasia inavyoendeshwa hapa Tanzania. *(Makofi)*

Naarifiwa kwamba wako kwenye mafunzo chini ya ofisi ya Bunge, ni *orientation* ya ofisi ya Bunge. *(Makofi)*

Wako pia wanafunzi wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM),* Chuo cha Mipango Dodoma, Chuo cha Uhasibu, Dar es Salaam na Chuo cha Biashara. Ningeomba nao hao wasimame, *CBE and others,* karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mbunge wa Igalula, anao wageni Madiwani kutoka Jimbo la Igalula, leo tuna bahati sana, wawakilishi wa Kata wako wengi sana, nikishamaliza kuwataja, naomba wasimame. Mheshimiwa Diwani Kapalu ambaye ni Katibu pia wa Mheshimiwa Mbunge kwenye Jimbo. Mheshimiwa Mashaka, Mheshimiwa Ally Kowoko, Mheshimiwa Emmanuel Kigadi, Mheshimiwa Hamisi Bundara, Mheshimiwa Anna Maria Mlolwa, Mheshimiwa Asia Pigangoma, Mheshimiwa Kalunde Ally, Mheshimiwa Joyce Kiyenze na Mheshimiwa Upendo Mgombozi, wale

pale. Ahsante sana, karibuni Waheshimiwa kutoka Igalula. Hapa ndio Bungeni. Napenda kuwahakikishia kwamba Mbunge wenu anafanya kazi vizuri sana na natumaini mtaendelea kumuunga mkono ili Igalula iendelee kung'ara. Ahsante sana. Namwita Katibu kwa hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008
### Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake, Mbunge wa Kongwa, Mheshimiwa Job Ndugai, na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria, Katiba na Utawala chini ya Mwenyekiti wake, Mbunge wa Mpwapwa, Mheshimiwa George Lubeleje, kwa michango mikubwa iliyotoa wakati wa kujadili, kuchambua na mwishowe kupitisha Makadirio haya. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais imezingatia vilivyo mapendekezo ya Kamati hizo na inaahidi kuyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Januari, 2007, aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Bunge, Marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, alifariki Dunia katika ajali ya ndege iliyotokea Mbeya. Marehemu atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa wa uongozi siyo katika Ofisi ya Waziri Mkuu tu bali kwa Jimbo la Tunduru na kwa Taifa zima.

Aidha, tarehe 25/6/2007, Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, aliyefariki dunia. Naye atakumbukwa kwa umahiri wake wa kutetea maslahi ya wananchi wa Tanzania hususani vijana. Wapo vilevile wananchi waliofariki Dunia katika maafa na ajali mbalimbali nchini na wengine kujeruhiwa.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kutoa pole kwa wafiwa wote na kuwatakia afya njema waliojeruhiwa. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura kwa kushinda katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Tunduru na Mheshimiwa Yusuph Makamba, pamoja na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya kwa kuteuliwa kuwa Wabunge.

Aidha, nawapongeza waliochaguliwa kuiwakilisha nchi yetu ya Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki ambao ni Mheshimiwa Dr. Didas John Massaburi, Mheshimiwa Dr. Amani Walid Kabourou, Mheshimiwa Dr. George Francis Nangale, Mheshimiwa Sylvia Kate Kamba na Mheshimiwa Septuu Nasoro. Wengine ni Mheshimiwa Abdallah Ally Hassan Mwinyi, Mheshimiwa Dr. Said Gharib Bilal, Mheshimiwa Janet Deo Mmari na Mheshimiwa Dr. Fortunatus Lwanyatika Masha. Kuchaguliwa kwao kunathibitisha imani kubwa waliyonayo Watanzania kwao.

Halikadhalika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dk. Asha Rose Migiro kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Hii ni heshima kubwa kwa Taifa letu kupewa nafasi ya juu ya uongozi katika chombo hiki.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limekuwa likijadili taarifa kuhusu hali ya uchumi wa Taifa katika Mwaka wa Fedha 2006/2007 na hatimaye kupitisha Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2007/2008. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dk. Juma Alifa Ngasongwa, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Mheshimiwa Zakhia Hamdani Meghji, Waziri wa Fedha na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa hotuba zao nzuri ambazo zimefafanua sera za jumla za uchumi na fedha, na mwelekeo wa uchumi katika mwaka wa fedha 2007/2008. Aidha, nawapongeza na kuwashukuru kwa jinsi walivyoweza kutoa maelezo ya hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Wametujengea misingi inayotuwezesha kuwasilisha Bungeni makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutoa maelezo ya majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na utekelezaji wake kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 na matarajio ya utekelezaji katika mwaka wa fedha 2007/2008. Makamu wa Rais ana majukumu mahsusi ya kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kufuatilia utekelezaji wa siku hadi siku wa mambo yote yanayohusu Taifa. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais inajukumu la kuratibu shughuli za Muungano na Mazingira kama ifuatavyo:-

(a) Kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa siku hadi siku wa Mambo ya Muungano na yasiyokuwa ya Muungano na ushirikiano kati ya Serikali zetu mbili;

(b) Kutoa ushauri wa kitaalamu katika mambo ya Sera na Sheria ya Mazingira; na

(c) Kuratibu miradi mtambuka ya sekta ya Mazingira na ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/07, Mheshimiwa Makamu wa Rais alipata fursa ya kufanya ziara mbalimbali za ndani na nje ya Nchi. Kwa ziara za ndani za kikazi, alitembelea Mikoa 11 ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa lengo la kukagua utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii kama zilivyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Katika ziara hizo Mheshimiwa Makamu wa Rais aliwahamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii ili Tanzania iweze kuwa na uchumi

imara. Aidha, aliwataka viongozi wa Serikali kutumia muda wao kuelekeza na kutoa ushauri muafaka kwa wananchi wanaowatumikia bila ya kuchoka.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ziara za nje, tarehe 12 hadi 14 Julai 2006, Mheshimiwa Makamu wa Rais alihudhuria Mkutano wa Pili wa Wasomi kutoka Afrika na "Diaspora" uliofanyika Salvador, Brazil. Zaidi ya washiriki 3,000 walihudhuria mkutano huo kujadili mikakati ya kusaidia maendeleo ya Afrika kwa kuimarisha ushirikiano na mshikamano baina ya Afrika na jamii za watu wenye asili ya Afrika kote duniani. Katika mchango wake, Mheshimiwa Makamu wa Rais, aliwaenzi waasisi wa "*Pan Africanism"* (Mwalimu Julius Nyerere, Mzee Abeid Karume, Jomo Kenyatta, Nelson Mandela na Kwame Nkrumah) kwa harakati zao za kupigania uhuru wa Afrika na umoja wake.

Lengo la waasisi wa *"Pan Africanism"* lilikuwa ni umoja na muungano wa Afrika na kwamba Mwalimu Nyerere na Mzee Karume walianzisha utekelezaji wa lengo hilo kwa vitendo kwa kuziunganisha Tanganyika na Zanzibar, ikiwa ni hatua ya mwanzo kuelekea muungano wa Afrika.

Baada ya ukombozi wa Afrika ajenda ya sasa ni maendeleo ya uchumi na umoja wa Bara la Afrika. Kwa upande wa Bara la Afrika, kazi iliyo mbele yetu ni kuanzisha na kuimarisha mikakati ya kuhamasisha raia wa nchi za Afrika wanaoishi nchi za nje kuchangia maendeleo ya nchi za Afrika katika huduma za jamii, uwekezaji na nyanja nyingine.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Oktoba 2006, Mheshimiwa Makamu wa Rais alimwakilisha Mheshimiwa Rais katika hafla ya ufunguzi wa Kikao cha 32 cha Kamati ya Chakula ya Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa, mjini Roma, Italia. Madhumuni ya kikao hicho yalikuwa ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango wa ahadi saba za kupunguza kwa nusu ya idadi ya watu wenye njaa duniani ifikapo mwaka 2015. *(Makofi)*

Katika hotuba yake, Mheshimiwa Makamu wa Rais alielezea tatizo la vita vya wenyewe kwa wenyewe, mfumo mbaya wa uchumi na biashara Duniani, uwekezaji mdogo katika kilimo, miundombinu isiyofaa, maradhi kama UKIMWI na uharibifu wa mazingira kwamba ni baadhi ya matatizo yanayohatarisha nchi zinazoendelea kutofanikisha ahadi hizo. Tanzania imepiga hatua nzuri katika kuzitekeleza ahadi saba kupitia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA) na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 16-18 Novemba 2006, Mheshimiwa Makamu wa Rais alimwakilisha Mheshimiwa Rais katika Mkutano wa Tano wa Maendeleo ya Afrika Kuhusu Vijana, uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia. Mbali ya Mawaziri na maofisa wa Serikali, mkutano huo ulihudhuriwa pia na wawakilishi wa vijana, Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali, jumuiya zinazojihusisha na masuala ya vijana na mashirika ya Umoja wa Mataifa.

Lengo la mkutano lilikuwa ni kuwakutanisha vijana, viongozi wa Serikali na vikundi mbalimbali vya jumuiya kwa pamoja na kujadili matatizo ya vijana na changamoto za maendeleo yao. Katika hotuba yake, Mheshimiwa Makamu wa Rais alielezea jinsi Tanzania inavyoyapa kipaumbele na umuhimu wa pekee masuala ya vijana katika sera na mipango mbalimbali hususan katika nyanja za elimu, ajira, uhamiaji mjini, ushirikishwaji na huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Novemba, 2006 Mheshimiwa Makamu wa Rais alimwakilisha Mheshimiwa Rais katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika na Amerika ya Kusini, uliofanyika Abuja, Nigeria. Mkutano huo wa kihistoria ulihudhuriwa na Wakuu wa nchi 26 kutoka mabara haya mawili ya Afrika na Amerika ya Kusini. Madhumuni ya mkutano huo yalikuwa ni kuzungumzia njia za kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kati ya pande zote mbili kwa manufaa ya wananchi wote. Nyaraka mbili za "Azimio la Abuja" na "Mpango wa Utekelezaji" zilijadiliwa na kupitishwa na mkutano. "Azimio la Abuja" linaelezea dhamira ya nchi za mabara haya mawili za kuendeleza ushirikiano katika nyanja za kimataifa za kiuchumi na kijamii wakati "Mpango wa Utekelezaji" unaelezea na kufafanua hatua zitakazochukuliwa na pande zote mbili katika kudumisha ushirikiano wao kama ilivyoainishwa katika Azimio.

Mheshimiwa Spika, tarehe 19-20 Aprili 2007, Mheshimiwa Makamu wa Rais alihudhuria Mkutano Maalum ulioitishwa na Shirika la Afya Duniani *(WHO)* kujadili maradhi ya nchi za Kitropiki ambayo hayajapewa kipaumbele, uliofanyika Geneva. Madhumuni ya mkutano huo yalikuwa ni kutoa nafasi kwa nchi zilizoathirika na maradhi hayo kupata fursa ya kusikilizwa ili ziweze kupata misaada endelevu. Kwa kuzingatia jitihada zinazofanywa na Serikali ya Tanzania katika kuangamiza maradhi hayo, *WHO* waliomba hotuba ya Mheshimiwa Makamu wa Rais itoe maelekezo ya namna ya kuyadhibiti maradhi hayo *(Keynote address)*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Sura ya Pili, Sehemu ya Pili, Ibara ya 47 – 1(a) jukumu la kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kufuatilia utekelezaji wa siku hadi siku wa masuala yanayohusu Muungano yamekabidhiwa kwa Makamu wa Rais. Aidha, Sheria namba 34 ya mwaka 1994 iliyoanzisha Ofisi yake inampa jukumu jingine la kuratibu ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nia kubwa ikiwa ni kudumisha Muungano wetu kwa njia ya Amani, Upendo na Mshikamano kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu la Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2006/07, Ofisi iliendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi mbalimbali ya Serikali zetu kuhusu masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano.

Katika Sekta ya Fedha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kupata gawio la asilimia 4.5 itokanayo na misaada isiyo na masharti, misamaha ya madeni inayotolewa na wafadhili pamoja na faida ya Benki Kuu ya Tanzania ambapo mpaka kufikia Aprili, 2007, kiasi cha shilingi 22,061,080,000/= kilitolewa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Halikadhalika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikipokea sehemu

ya Kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* na Ushuru wa Bidhaa *(Excise Duty)* ambayo inakusanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatakiwa kulipwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tume ya Pamoja ya Fedha imefanya kazi nzuri ya kukamilisha taarifa ya mapendekezo juu ya vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano. Aidha, vimefanyika vikao vinne (4) vya wataalam na mawaziri katika sekta ya fedha kujadili taarifa hiyo na kutoa mapendekezo ambayo yamewasilishwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete katika Semina Elekezi kwa Viongozi wa Serikali zetu iliyofanyika Arusha mwezi Machi, 2006 alitoa maagizo ya kuwataka Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi kukutana na kujadili namna ya kutatua vikwazo mbalimbali vinavyotukabili katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Ofisi ya Makamu wa Rais iliandaa, iliratibu na kushiriki katika kikao kimoja cha Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kilichofanyika Novemba, 2006, Zanzibar. Masuala mbalimbali ya Muungano wetu yalijadiliwa na kufanyiwa maamuzi ambayo baadhi yameishatekelezwa na mengine yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, vikao hivi vya viongozi wetu wa ngazi za juu katika kujadili na kutatua vikwazo katika kutekeleza masuala ya Muungano vimeonyesha mafanikio makubwa kwani baadhi ya mambo yaliyokuwa yanaonekana kero kwa wananchi yamefanyiwa kazi na kutatuliwa.

Kati ya mambo hayo ni suala la malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili. Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanza kutumia Mtandao wa *ASYCUDA++* kuanzia mwezi Juni 2006 ambao unatumika hadi Zanzibar. Mtandao huu unamtaka mwingizaji bidhaa kutoa tamko la gharama za bidhaa anazoingiza nchini *(Self declaration)*.

Hivyo basi, Mtandao wa *ASYCUDA++* unategemea kuondosha ulipishwaji wa kodi mara mbili. Jambo muhimu sasa ni kujenga uwezo kwa watendaji ili mtandao huo uweze kutumika kikamilifu na kuondoa malalamiko ya wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sheria Na. 7 ya mwaka 2001, imefanyiwa marekebisho na Bunge lako Tukufu mwaka 2006 na tayari inatumika pande zote mbili za Muungano.

Mabadiliko hayo yanamtaja Waziri mwenye dhamana ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupata taarifa za Tume na kuziwasilisha katika Baraza la Wawakilishi.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ina Ofisi na watumishi pande zote za Muungano na wanatekeleza majukumu yao kulingana na Sheria. Jambo hili linaliletea Taifa letu sifa nzuri kwa kuwa tunaheshimu na kuzilinda haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais imeratibu urekebishwaji wa Sheria ya Mamlaka ya kusimamia Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu. Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi kwenye Bahari Kuu yamepitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwanzoni mwa Februari, 2007.

Aidha, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Kiongozi na Katibu Mkuu Wizara inayoshughulikia masuala ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) wamejumuishwa katika Kamati ya Utendaji ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu ili kurahisisha utoaji wa taarifa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, suala la Sheria ya Usafiri Majini (*Merchant Shipping Act, 2003)* katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeendelea kutekelezwa. Wizara ya Miundombinu ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilikaa kwa pamoja kuangalia namna ya kutekeleza maelekezo ya vikao vya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi.

Kanuni nane (8) za *Merchant Shipping Act***,** ya mwaka 2003 tayari zimeshapelekwa Wizara ya Mawasiliano ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili zioanishwe na kanuni za *"Zanzibar Maritime Transport Act,* 2006" kwa lengo la kuleta usimamizi usiokinzana katika masuala ya uchukuzi majini.

Aidha, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar amepatiwa *access code* na Wizara ya Miundombinu ili aweze kuona nyaraka katika mtandao wa *IMO.*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ndio mratibu wa Ushirikiano wa Kimataifa. Kwa sasa maandalizi ya miradi ya pamoja *(Joint Assistance Strategy For Tanzania -JAST)* yanafanywa kwa pamoja ili kushirikisha miradi ya Tanzania Zanzibar, ikiwa ni pamoja na miradi itakayoingizwa na Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Miradi ihusuyo Tanzania Zanzibar ambayo imeshaingizwa katika Jumuiya ni pamoja na miradi ya kuimarisha Bandari, Viwanja vya Ndege na *East Africa Power Master Plan.* Miradi mingine iliyoihusisha Tanzania Zanzibar ni pamoja na ile ya *'Millenium Challenge Account' (MCC)* na *'Agricultural Sector Development Programme' (ASDP).*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu miradi ya Muungano ambapo tunaona uanzishwaji wa miradi mingi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na inaendelea kushamiri. Serikali imechukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa miradi ya Muungano inaandaliwa na kutekelezwa katika pande zote za Muungano. Hii ikiwa ni pamoja na mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* na *Small*

*Entrepreneur Loan Facility (SELF),* ili kuweza kuweka uwiano mzuri wa maendeleo kwa pande zote za Muungano.

Aidha, Taasisi za Muungano zimejenga majengo Tanzania Zanzibar kwa ajili ya ofisi. Taasisi hizo ni pamoja na Ofisi za Bunge, Tawi la Benki Kuu ya Tanzania, Uhamiaji na Kituo cha Utafiti wa Viumbe vya Baharini. Pamoja na miradi hii, Taasisi nyingine za Muungano zimefungua Ofisi zake huko Tanzania Zanzibar ili kutoa huduma zake kwa ufanisi zaidi ambazo ni Tume ya Pamoja ya Fedha, Msajili wa Vyama vya Siasa, Tume ya Mawasiliano na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, tofauti ya mitaala kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ni moja ya matatizo yanayochangia kupunguza kiwango cha ushindani katika soko la ajira kwa wananchi watokao Tanzania Zanzibar.

Hivyo, ili kuendeleza ari na dhamira ya Muungano, Wizara zinazohusika na suala la elimu toka pande zote za Muungano zinashughulikia suala la kurekebisha Sera na mitaala ya elimu kwa lengo la kuboresha huduma na mfumo wa elimu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kufanya hivyo kutainua kiwango cha ushindani katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi linaendelea kushughulikiwa. Serikali zetu kwa kutambua umuhimu wa nishati hii kwa maendeleo ya Taifa letu, zilikubaliana kuwa kabla ya kufanya maamuzi mengine ni vema atafutwe Mshauri Mwelekezi ili aweze kushauri namna bora ya kushughulikia suala hili kama linavyoshughulikiwa katika nchi zilizoungana na zenye rasilimali ya Mafuta.

Kwa hivi sasa Wizara husika kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la mafuta *(Tanzania Petroleum Development Corperation (TPDC)* zimeandaa Rasimu ya Hadidu za Rejea ambazo zitatumiwa na Mshauri Mwelekezi katika kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais imechukua hatua za makusudi kuelimisha jamii kuhusu Masuala ya Muungano wetu. Taarifa mbalimbali za Muungano zimekusanywa kwa ajili ya kurusha hewani kupitia Redio na Televisheni na kuandaliwa kwa ajili ya makala katika magazeti na vijarida. Nakala elfu kumi (10,000) za vipeperushi kuhusu Muungano wetu zilichapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali wa Muungano.

Aidha, vipindi 18 vya Muungano vilitayarishwa na kurushwa hewani kupitia Redio Tumaini, Redio Mlimani, Redio Uhuru na Redio Tanzania kwa upande wa Tanzania Bara na Sauti ya Tanzania Zanzibar kwa upande wa Zanzibar. Halikadhalika, Shirika la Habari la Uingereza na Sauti ya Ujerumani walifanya mahojiano na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kuhusu Muungano wetu na kurushwa hewani. Aidha, taarifa hizi zilionyeshwa kupitia Televisheni ya Taifa (TVT) na Televisheni ya Zanzibar (TVZ). Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa mada za mambo ya Muungano ambazo zitaingizwa katika ukurasa wa Mambo ya Muungano na kuunganishwa katika Tovuti ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais iliwezesha safari ya wanafunzi 200 wa Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Mzumbe na Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)* waliwezeshwa kuwatembelea wanafunzi wenzao wa Vyuo Vikuu vya Tanzania Zanzibar kwa lengo la kuelimisha jamii ya rika lao kuhusu mambo ya Muungano ikiwa ni pamoja na kukuza ushirikiano na udugu. Wanafunzi hao walifanya mijadala kuhusu Muungano na kufanya kazi ya kusafisha mazingira kwa pamoja. Ziara hiyo ilikuwa ni ya mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais imeshiriki kikamilifu katika maandalizi na kuhudhuria sherehe za Muungano ikiwa ni pamoja na kufuatilia matukio mbalimbali yaliyotokea katika maadhimisho hayo yaliyofanyika Dar es Salaam, tarehe 26 Aprili, 2007. Aidha, tumeshiriki katika kutafuta wafadhili wa mashindano ya kombe la Muungano - Mufindi ambalo lilikutanisha timu za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar lenye lengo la kudumisha uhusiano kati ya wananchi wa pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais inalo jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa kunakuwepo ushirikikano kati ya Serikali zetu mbili katika nyanja zote za kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa. Ili kufanikisha jukumu hili Ofisi iliandaa ratiba ya vikao vya ushirikiano kwa ajili ya Wizara, Idara, Taasisi na Asasi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kusambaza kwa wahusika. Lengo la vikao hivi ni kujadili masuala ya kisekta, kubadilishana uzoefu, ujuzi, utaalamu, sera pamoja na uwakilishi katika vikao vya kimajimbo na kimataifa.

Vikao hivi vimekuwa vikifanyika na taarifa kuletwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kwa lengo la kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yanayofikiwa na kushauri ipasavyo. Aidha, jumla ya Wizara kumi na nne (14) za pande zote mbili za Muungano zimekutana kwa mwaka wa fedha 2006/07. Vikao hivi vimesaidia kuongeza ushirikiano baina ya pande mbili za Muungano katika sekta mbalimbali. Pamekuwepo na ushirikiano wa kuridhisha katika maandalizi ya Mipango ya pamoja ya Kitaifa kama mpango wa kuondoa umaskini Zanzibar (MKUZA), Mkakati wa kuondoa Umaskini wa Tanzania Bara (MKUKUTA), Mkakati wa Kupambana na UKIMWI na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais ilishiriki katika vikao mbalimbali na kuwasiliana na wadau wa Muungano ambapo taarifa zimekusanywa kuhusu kutatua changamoto zinazojitokeza katika Muungano wetu. Taarifa hizo zimefanyiwa uchambuzi na kujumuishwa katika Rasimu ya Mkakati wa Kuondoa Kero katika utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kuimarisha Mashirikiano kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa kazi zinafanywa kwa ufanisi na tija watumishi watano walipata mafunzo ya muda mfupi na baadhi yao kupata fursa ya kutembelea nchi zenye Muungano kama wetu kwa lengo la kupata uzoefu. Nchi walizotembelea ni Uingereza, Ujerumani, Canada na *Norway.*

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuratibu masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano katika vikao vikiwemo vya kimataifa. Ili kufikia lengo hili Ofisi ya Makamu wa Rais itashiriki katika maandalizi na kuhudhuria vikao vinavyohusiana na masuala ya Muungano. Aidha, tutakusanya taarifa kuhusiana na masuala yatakayoamuliwa katika vikao hivyo na kufuatilia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuratibu, kuandaa na kushiriki katika vikao kati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuondoa kero katika Muungano wetu. Katika kufanikisha lengo hili, Ofisi ya Makamu wa Rais itaainisha maeneo yenye kero na kuandaa vikao vya watendaji wakuu wa Serikali pamoja na Mawaziri katika Sekta husika za Muungano ili kuandaa vikao vya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi ambavyo inategemewa kuwa vitafanyika mara tatu kwa mwaka. Taarifa za vikao hivyo zitaandaliwa ikiwa ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya vikao hivyo.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kufanya tafiti kwa Mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano kwa lengo la kuimarisha Muungano litaendelea, ikiwa ni pamoja na kufanya uchambuzi wa kina wa tafiti hizo na kisha kuwasilisha mapendekezo hayo Serikalini. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais itafanya uperembaji wa utekelezaji wa majukumu kwa lengo la kuimarisha Muungano wetu. Tathmini itafanyika kwa kila robo mwaka ili kupima utekelezaji wa masuala ya Muungano ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa na kuzisambaza kwa wadau wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya malalamiko na vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano wetu yanatokana na wananchi wengi kuwa na uelewa mdogo katika masuala hayo. Ili kuongeza uelewa juu ya Muungano wetu, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu Mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano kwa wananchi wa pande zote mbili. Katika kutekeleza jukumu hili mambo yafuatayo yatafanyika:-

(a) Kuandaa majarida yanayohusu Muungano na kusambaza kwa wadau;

(b) Kuandaa makala na kuingiza katika ukurasa wa Tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais na katika Tovuti ya Taifa;

(c) Kuandaa vipindi vya masuala ya Muungano na kuvirusha hewani kupitia Redio na Televisheni;

(d) Kuandaa Warsha, Semina na mikutano kwa wadau wa Muungano, kwa lengo la kutoa elimu na kupata mawazo yao kuhusiana na masuala ya Muungano; na

(e) Kubuni na kuandaa vipeperushi na mabango yenye ujumbe kuhusu masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, Ofisi ya Makamu wa Rais ikishirikiana na wadau wa Muungano itaendelea na:-

(a) Kuainisha maeneo ya kiuchumi katika nchi yetu ambayo yakitekelezwa yataleta faida kwa pande zote mbili za Muungano;

(b) Kuratibu masuala ya Sekta ya Uchumi ili kufanywa kwa ushirikiano kwa nia ya kuoanisha uchumi wetu kwa lengo la kukuza Uchumi wa Taifa letu na kuleta matumaini zaidi kwa watanzania wote; na

(c) Kuratibu ushiriki wa pande zote mbili za Muungano katika kutekeleza Mkakati wa Pamoja wa Misaada ya Maendeleo (*JAST*). Katika kufanikisha jukumu hili, Ofisi itahakikisha kuwa mahitaji ya Zanzibar yanajumuishwa ipasavyo katika miradi ya Tanzania na mikutano ya pamoja ya mashauriano ya *JAST* itafanyika na maamuzi yatakayofikiwa yatatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuhakikisha kuwa ustawi wa kijamii, kiuchumi na kisiasa unaongezeka kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Ili kufanikisha jukumu hili Ofisi itaratibu mpango wa utekelezaji wa miradi kwa pande zote za Muungano hususan ile inayolenga kuinua hali za kiuchumi na kuboresha huduma za kijamii kwa ajili ya ustawi wa Watanzania wote. Aidha, ili kuulinda na kuudumisha Muungano wetu, tutaendelea kushiriki katika maandalizi ya sherehe za Muungano ambazo zinaadhimishwa kila mwaka ifikapo Aprili, 26.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuratibu gawio la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kufuatilia na kuhamasisha uandaaji wa utaratibu wa kudumu wa kugharimia Muungano na suala la mgawanyo wa mapato yatokanayo na vyanzo vya mapato vya Muungano ikiwa ni pamoja na misamaha ya madeni itolewayo na wafadhili na faida ya Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuratibu vikao vya ushirikiano vya Wizara, Idara na Asasi zisizo za Muungano ili kukuza ushirikiano baina ya Serikali zetu mbili kwa mambo yasiyo ya Muungano. Katika kutekeleza jukumu hili, utaratibu umeandaliwa wa kuhakikisha Wizara zisizo za Muungano zinakutana angalu mara mbili kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Idara itahakikisha inakuwa na watumishi waliopata mafunzo ya jinsi ya kushughulikia masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Hii itafanyika kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wa Idara. Aidha, ziara za mafunzo nje na ndani ya nchi zitafanyika ili kuwezesha ubadilishanaji wa uzoefu wa kitaalamu wa Kitaifa na Kimataifa wa mambo yanayohusu Muungano na yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mazingira. Katika miaka ya hivi karibuni suala la mazingira limechukua umuhimu wa hali ya juu katika jamii na Serikali duniani kote. Uharibifu wa mazingira umebainika kuwa tishio kwa maendeleo na maisha ya binadamu. Uendeshaji wa shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii na matumizi ya maliasili

kwa namna isiyozingatia athari zake kwa binadamu na kwa mazingira umesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira duniani kote.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Mazingira imeainisha matatizo ya mazingira katika maeneo makuu sita: uharibifu wa ardhi; upungufu wa miti na misitu; utowekaji wa mapori na upunguaji wa maliasili yake; uchafuzi na upungufu wa vyanzo vya maji; uharibifu wa maliasili ya majini; uchafuzi wa hewa na uchafuzi wa mazingira kwa ujumla hasa katika sehemu za makazi. Kwa sababu ya hali inayoendelea nchini ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira ya vyanzo vya maji, kuenea kwa hali ya jangwa na ukame, mmomonyoko wa ardhi na aina nyingine za uharibifu wa mazingira nchini, Serikali imeweka umuhimu wa juu katika suala la hifadhi na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, athari za uharibifu wa mazingira hazitambui mpaka kati ya nchi na nchi au Bara na Bara. Uzoefu umeonyesha kwamba uharibifu wa mazingira katika nchi jirani, au hata katika nchi za mbali unaweza kutuathiri. Hivyo basi hatuna budi kujiandaa, kujiwekea na kutekeleza mikakati ya jinsi ya kukabiliana na matatizo hayo na athari zake kitaifa, kikanda na kimataifa. Baadhi ya athari za namna hii ni zile zinazotokana na ongezeko la joto duniani, mmomonyoko wa ukanda wa Ozoni angani, kuenea kwa hali ya jangwa na ukame, matumizi na usafirishaji wa kemikali na utupaji wa taka zenye sumu baina ya nchi na nchi na upotevu wa bioanuai. Kwa kuzingatia hili, Tanzania imeridhia mikataba kadhaa ya kimataifa na ya kikanda inayohusu mazingira, mikataba ambayo Ofisi ya Makamu wa Rais inaratibu utekelezaji wake, sambamba na utekelezaji wa mikakati, programu na miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi mwaka 2006 Serikali ilipitisha Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Mkakati huu umelenga kukabiliana na uharibifu mkubwa wa mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji uliosababishwa na shughuli za kilimo kisicho endelevu na ufugaji wa kuhamahama. Uharibifu huu umechangiwa pia na ukataji wa miti ovyo kwa ajili ya kuni na mkaa, kilimo cha umwagiliaji kisichokuwa endelevu, matukio ya mara kwa mara ya uchomaji wa misitu, uchimbaji wa madini usio endelevu, na uchafuzi utokanao na mifuko ya plastiki hasa maeneo ya mijini. Hali hii imesababisha kuenea kwa hali ya jangwa na ukame, na kukauka kwa vyanzo vya maji nchini, na hivyo kuathiri shughuli za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/07, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati huu. Hadi kufikia mwezi Februari 2007, uperembaji wa utekelezaji wa Mkakati ulifanyika katika mikoa 12 ya Mbeya, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, Lindi, Tabora, Kagera, Kigoma, Morogoro na Singida. Taarifa za Utekelezaji wa Mkakati ziliandaliwa na Hati za taarifa hizo zilijadiliwa Serikalini. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendesha warsha kwa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira na kwa wadau mbalimbali ili kukuza uelewa wao wa Mkakati na ushiriki wao katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto zilizoainishwa katika Mkakati, Serikali ilitoa matamko mbalimbali. Matamko hayo ni pamoja na Tangazo la Serikali kuhusu kupiga marufuku baadhi ya mifuko ya plastiki lililotolewa na Ofisi ya Makamu

wa Rais; Tamko kuhusu Mwongozo wa Uvunaji na Biashara ya Mazao ya Misitu lililotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii; na Tamko kuhusu taratibu za kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi jingine, lililotolewa na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya migongano katika matumizi ya ardhi baina ya wadau mbalimbali, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ilipima vijiji na kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi. Hadi Machi 2007, jumla ya vijiji 133 nchini vilikuwa vimepimwa katika wilaya za Chunya (vijiji 15), Mbeya vijijini (vijiji 5), Mbarali (vijiji 9), Iringa vijijini (vijiji 5), Kilolo (vijiji 3), Mufindi (vijiji 2), Makete (vijiji 4), Kisarawe (vijiji 8), Mkuranga (vijiji 3), Rufiji (vijiji 13), Kilwa (vijiji 10), Lindi (vijiji 8), Nachingwea (vijiji 10), Liwale (vijiji 3), Mvomero (vijiji 5), Kilosa (vijiji 5), Kilombero (vijiji 5), Morogoro vijijini (vijiji 5), Ulanga (vijiji 5), Chamwino (vijiji 5) na Manyoni (vijiji 5).

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti uharibifu kwenye vyanzo vya maji utokanao na wafugaji, operesheni ya kuwaondoa wafugaji kutoka bonde la Ihefu ilianza tarehe 18 Mei 2006. Bonde hilo linakisiwa kuwa lilikuwa na ng'ombe wapatao 350,000, mbuzi 135,000 na kondoo 102,023. Hadi kufikia Machi 2007 zaidi ya asilimia 90 ya mifugo hiyo ilikuwa imeondolewa. Mifugo iliyoondolewa ilipelekwa katika wilaya za Chunya, Kisarawe, Lindi, Kilwa, na Nachingwea. Katika kudhibiti wafugaji wavamizi kutoka nchi jirani, Serikali iliendesha operesheni ya kuwaondoa kwa vipindi tofauti na kuwarudisha Rwanda na Uganda.

Mheshimiwa Spika, Mkakati unaelekeza uanzishaji wa Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti. Maandalizi ya Mwongozo wa kuendesha Tuzo ya Rais yalifanywa. Warsha tano za kikanda zimeendeshwa ili kupata maoni ya wadau mbalimbali kuhusu rasimu ya Mwongozo wa kutoa Tuzo katika ngazi mbalimbali. Warsha zilihusisha mikoa ya Kanda ya Ziwa (Kagera, Mwanza, Mara na Shinyanga), Kanda ya Kaskazini (Arusha, Kilimanjaro na Manyara), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya, Ruvuma na Iringa), Kanda ya Magharibi (Kigoma, Rukwa na Tabora) na Kanda ya Kati (Dodoma na Singida). Rasimu ya Mwongozo inaonyesha Makundi ya ushindani; Aina ya Tuzo zitakazotolewa kwa washindi wa kila kundi; Vigezo kwa ajili ya kumpata mshindi wa Tuzo kwa makundi mbalimbali kuanzia ngazi ya kaya, kijiji, kata, wilaya, mkoa na taifa; Mchakato na Ratiba ya uteuzi wa washindi na Utaratibu wa kutoa na kukabidhi Tuzo. Tuzo itatolewa kwa mara ya kwanza mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uperembaji na taarifa zilizopokelewa kutoka kwa wadau yanaonyesha utekelezaji wa Mkakati umeanza kuzaa matunda. Uoto wa asili katika bonde la Ihefu umeongezeka baada ya mifugo kuondolewa ukilinganisha na hali ilivyokuwa miaka iliyopita kwa nyakati zile zile. Matukio ya kuchoma moto misitu na nyika yanaendelea kudhibitiwa kote nchini. Wilaya mbalimbali zimeainisha vyanzo vya maji katika maeneo yao. Hali ya usafi wa miji na maeneo mbalimbali nchini inaendelea kuwa bora kufuatia kupiga marufuku baadhi ya mifuko ya plastiki na viroba vya maji na maji ya matunda vya plastiki. Pamoja na mafanikio yaliyoanza kupatikana, kuna

changamoto mpya zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mkakati kama vile ufugaji holela katika maeneo ambayo wafugaji hawakupangiwa, watendaji kutoelewa au kutotekeleza ipasavyo zoezi la kuwaondoa wafugaji. Aidha, udhibiti wa mifuko ya plastiki inayoingia nchini bado ni changamoto muhimu. Serikali imekwisha chukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/08, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kusimamia, kuratibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa Mkakati. Hati za taarifa za utekelezaji wa Mkakati zitaandaliwa. Rasimu ya Mwongozo wa Mashindano ya Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti itakamilishwa na utekelezaji wa Mwongozo utaanza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea na maandalizi ya kanuni, miongozo na viwango vya usimamizi wa mazingira chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Rasimu za miongozo na kanuni zifuatazo zimeandaliwa na ziko katika hatua za mwisho kukamilika:- Kanuni za Viwango vya Ubora wa Mazingira *(Environmental Quality Standards Regulations, 2007 - Air quality, Water quality, Soil quality);* Kanuni za Ada na Tozo chini ya Sheria (*Fees and Charges Payable under the Environmental Management Act (EMA)*, 2004, Regulations, 2007); Kanuni kuhusu Kemikali zinazoharibu Tabaka la Ozoni *(Ozone Depleting Substances Regulations,* 2007); Kanuni za Tathmini ya Kimkakati ya Athari kwa Mazingira (*Strategic Environmental Assessment Regulations,* 2007); na Miongozo ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira *(Environmental Impact Assessment Guidelines).* Kanuni za Kupiga Marufuku Uingizaji, Usambazaji, Uuzaji, Ununuzi na Utumiaji wa Mifuko ya Plastiki ziliandaliwa na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais itakamilisha maandalizi ya miongozo na kanuni nilizozitaja. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais itaandaa kanuni na miongozo ifuatayo:- Kanuni za Wakaguzi wa Mazingira *(Environmental Inspectors Regulations),* Kanuni za Nyenzo za Kiuchumi kwa ajili ya Kutunza Mazingira *(Environmental Economic Instruments Regulations),* Miongozo ya Wakaguzi wa Mazingira *(Envrionmental Inspectors Guidelines),* pamoja na Miongozo ya Usimamizi wa Taka *(Guidelines for the management of waste).* Kanuni hizi zitasaidia pia katika utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji. Ripoti ya kwanza ya Hali ya Mazingira nchini inakamilishwa na maandalizi ya Ripoti ya Pili yataanza mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa fedha wa 2006/07, Ofisi ya Makamu wa Rais ilikamilisha maandalizi ya Programu ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira *(Environmental Management Act – Implementation Support Programme).* Programu hii ni ya miaka mitano, kuanzia 2007/2008 hadi 2011/2012 na bajeti yake ni dola za Marekani milioni 40.7. Utekelezaji wa Programu utahusisha Wizara na Taasisi 16 zifuatazo:- Ofisi ya Makamu wa Rais, ambayo ndio mratibu; Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Wizara

ya Viwanda, Biashara na Masoko; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo; Wizara ya Miundombinu; Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana; Wizara ya Nishari na Madini; Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Wizara ya Maji; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Wizara ya Mambo ya Ndani; Wizara ya Maliasili na Utalii; na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*).

Tayari Serikali ya *Denmark* imekubali kusaidia dola za Marekani milioni 6.14 katika utekelezaji wa Programu hii. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali ya *Denmark* itatoa dola za Marekani milioni 2.6 ili kuanza utekelezaji wa awamu ya awali *(inception phase).*

Mheshimiwa Spika, Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mabwawa na Mito. Tatizo la uchafuzi na uharibifu wa mazingira ya bahari, ukanda wa pwani, maziwa, mabwawa na mito ni kubwa. Uharibifu huu umesababisha kupungua kwa kina cha maji kwenye maziwa na mabwawa, kukauka kwa mito, kuongezeka kwa mmomonyoko wa ardhi, kuongezeka kwa tabaki na uchafuzi katika maziwa, mito na mabwawa, kuongezeka na kusambaa kwa magugu maji, kupungua kwa rasilimali za bahari, maziwa, mabwawa na mito. Matokeo yake ni kupungua kwa lishe bora, ongezeko la migogoro itokanayo na matumizi ya rasilimali za majini, upungufu wa uzalishaji umeme utokanao na maji na kukwamisha juhudi za kupambana na umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kudhibiti changamoto zilizopo. Hatua hizi ni pamoja na utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali. Miradi hii ni pamoja na: Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria *(Lake Victoria Environmental Management Project);* Mradi wa Hifadhi wa Bonde la Mto Nile *(Nile Trans-boundary Environmental Action Project);* Mradi wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ya Pwani na Bahari *(Tanzania Coastal Management Partnership Project);* Programu ya Hifadhi na Maendeleo ya Ukanda wa Pwani wa Tanga (Tanga *Coastal Zone Conservation and Development Programme);* na Programu ya Hifadhi ya Ukanda wa Pwani wa Kinondoni (Kinondoni *Coastal Area Management Programme).* Pamoja na juhudi hizi, bado uharibifu wa mazingira unaendelea, na jitihada zaidi zinahitajika. Bado yapo maeneo mengi ya maziwa, mabwawa na mito nchini ambayo hayana programu, miradi au mikakati ya hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais ilianza maandalizi ya Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mabwawa na Mito. Wadau mbalimbali walishirikishwa ikiwa ni pamoja na:- Wizara za Maliasili na Utalii; Maji; Maendeleo ya Mifugo; Kilimo, Chakula na Ushirika; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa); Nishati na Madini; Miundombinu; Viwanda, Biashara na Masoko; Usalama wa Raia; Mipango, Uchumi na Uwezeshaji; na Katiba na Sheria, Sekta binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Warsha za kikanda za kujadili rasimu ya Mkakati ziliendeshwa zikijumuisha mikoa 15. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais

iliendesha semina kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira ili kupata mchango na maoni yao.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais itakamilisha maandalizi ya Makakati huu. Baada ya kupitishwa na Serikali, Mkakati utasambazwa kwa wadau kwa ajili ya utekelezaji. Elimu itatolewa kwa wadau ili waielewe nafasi yao katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika. Tarehe 5 - 6 Aprili, 2007, Tanzania ilipata heshima ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa kwanza wa Mawaziri wa Nchi zinazounda Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika *(Lake Tanganyika Authority)* uliofanyika mjini Dar es Salaam. Mkutano huu ulihudhuriwa na Mawaziri wanaoshughulikia masuala ya mazingira katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Tanzania na Zambia. Aidha, Mkutano huo ulitanguliwa na vikao viwili vya wataalamu vilivyofanyika mjini Bujumbura, Burundi , tarehe 28 Februari, 2007 na jijini Dar es Salaam tarehe 3 - 4 Aprili, 2007.

Katika Mkutano huo, Mawaziri walitia saini Tamko la pamoja la Dar es Salaam (Dar es Salaam *Declaration)* kuhusu kuanzishwa rasmi kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika *(Lake Tanganyika Authority).* Mamlaka hii imeanzishwa kwa mujibu wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa *Tanganyika (The Convention on the Sustainable Management of Lake* Tanganyika). Lengo kuu ni kuhakikisha kwamba mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika yanahifadhiwa, na rasilimali zake zinatumika kwa njia endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano nilioutaja, Mawaziri walikubaliana kwamba Bujumbura, iwe makao makuu ya Mamlaka. Dk. Henry Mwima kutoka Zambia aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa kwanza wa Mamlaka kwa kipindi cha miaka mitatu (3). Aidha, Mawaziri waliamua nafasi za Wakuu wa Idara zigawanywe kwa uwiano wa nchi kama ifuatavyo:- Mkurugenzi wa Mazingira (Burundi); Mkurugenzi wa Uvuvi (Tanzania); Mkurugenzi wa Fedha na Utawala (*DRC*); na Mkurugenzi wa *Monitoring and Evaluation* (Zambia).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais itaanza kuratibu utekelezaji wa miradi mitatu (3). Miradi hii ni:- Mradi wa kuhifadhi mazingira ya Bonde la Ziwa *(catchment*) kwa msaada wa Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(Global Environment Facility - GEF*) wa shilingi bilioni 2.2 kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*); Mradi wa Usimamizi wa Majitaka katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji kwa msaada wa *GEF* wa shilingi milioni 300,000 kupitia *UNDP* na mkopo toka *NORDIC Fund* wa shilingi bilioni 6; na Mradi wa uendelezaji wa uvuvi na hifadhi ya mazingira ya ziwa Tanganyika kwa mkopo wa shilingi bilioni 7.4 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*. Kwa upande wa Tanzania Ofisi ya msimamizi wa Ziwa Tanganyika itakuwa Kigoma-Ujiji.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Mto *Nile*. Ofisi ya Makamu wa Rais inaratibu kitaifa programu ya hifadhi ya mazingira ya Bonde la mto

*Nile*, inayotekelezwa pia na nchi tisa zilizo katika bonde hili. Nchi hizo ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*DRC*), Burundi, Rwanda, Uganda, Kenya, Sudani, Ethiopía, Misri, na Tanzania. Programu hii ni ya miaka mitano na ilizinduliwa mwezi Mei, 2004. Makao makuu ya programu hii yako mjini *Khartoum*, Sudan. Kila nchi husika inayo ofisi ya uratibu kitaifa. Programu hii inalenga katika kujenga uwezo na mfumo wa ushirikano wa kusimamia, kuhifadhi na kulinda mazingira ya bonde la mto *Nile* kufuatana na matarajio na dira ya pamoja ya taasisi ya ushirikiano ya Bonde hili. Programu ina vipengele muhimu vifuatavyo:-

Ushirikishaji jamii kwenye hifadhi ya ardhi, misitu na maji kwa ajili ya kugharamia miradi midogo midogo ya wananchi; kutoa elimu ya mazingira kwa umma; hifadhi ya ardhi na bioanuai; na ufuatiliaji wa hali ya ubora wa maji katika bonde la mto *Nile*. Ofisi ya mratibu wa kitaifa wa miradi midogo midogo iko katika Jiji la Mwanza. Programu inafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(GEF)* kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*), Benki ya Dunia na Shirika la Maendeleo la Canada (*CIDA*). Hadi kukamilika kwake mwaka 2008 Programu inatarajiwa kugharimu dola za Marekani milioni 3.6

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 kazi zifuatazo zilifanyika:- Miradi midogo midogo 25 ya kuhifadhi mazingira na kuondoa umaskini yenye thamani ya dola za Marekani 629,649 ilitekelezwa na taasisi za kijamii zisizo za kiserikali kwenye wilaya za Misenyi, Bukoba vijijini, Muleba, Misungwi, Magu, Ukerewe, Bunda, Musoma vijijini na Tarime.

Aidha, jumla ya dola za Marekani 18, 576 zilitolewa kwa shule katika wilaya zilizotajwa hapo juu kwa ajili ya kuendesha miradi midogo midogo ya hifadhi ya mazingira. Warsha ya kikanda iliyojadili athari za sera za maendeleo kwa mazingira ilifanyika Dar es Salaam na washiriki walitoka kwenye nchi zote zilizo kwenye bonde la mto Nile.

Warsha ya walimu kutoka shule za sekondari za Bwiru Wasichana, *Lake*, Nganza Wasichana, Rugambwa, Karagwe, Bukoba, Nansio, Biashara ya Shinyanga *(SHYCOM)*, Maswa Wasichana na Seminari ya Makoko, kuhusu matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano ilifanyika. Warsha ya wanahabari ilifanyika ambapo mtandao wa kitaifa wa wanahabari wa Nile ulianzishwa. Aidha, semina ya wabunge wa nchi zilizomo katika bonde la *Nile* ilifanyika Entebbe na Bunge lako Tukufu liliwakilishwa.

Mheshimiwa Spika, mashindano ya insha na uchoraji kwa wanafunzi wa shule za sekondari yalifanyika na washiriki wawili, mmoja kutoka Seminari ya Makoko (insha) na mwingine kutoka Sekondari ya Bukoba (uchoraji), walishinda zawadi za kikanda (nchi 9) na kukabidhiwa zawadi huko Entebbe.

Programu iliwezesha wanafunzi wawili wa Shahada ya Uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kufanya tafiti zao nchini Kenya na Ethiopía. Tanzania ilishiriki katika mikutano na warsha mbalimbali za kikanda zilizofanyika kwenye nchi nyingine zilizomo katika bonde la mto *Nile*. Vilevile, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na

Mafunzo ya Ufundi, Programu ilichapisha nakala 2,500 za mwongozo wa ufundishaji wa somo la mazingira kwenye shule za sekondari.

Nakala hizo ziligawiwa kwa shule mbalimbali za Kanda ya Ziwa. Programu pia iliandaa maadhimisho ya wiki ya mazingira ya *Nile* sambamba na maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2007/2008 shughuli zifuatazo zitatekelezwa:- kuendeleza tafiti na mipango ya usimamizi wa ardhi oevu na bioanuai; kuendelea kuratibu utekelezaji wa miradi midogo midogo ya jamii na shule na kutoa elimu kwa jamii juu ya mazingira ya bonde la mto *Nile*. Aidha, kwa kushirikiana na taasisi nyingine, Programu itapima ubora wa maji kwenye bonde hilo na kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za mradi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha maandalizi ya Programu ya Kitaifa ya Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi *(National Adaptation Programme of Action on Climate Change* - *NAPA*), katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais ilifanya tathmini ya athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta za Afya, Kilimo na Maji. Lengo la tathmini hii lilikuwa ni kupata uelewa zaidi wa athari za mabadiliko haya katika sekta hizo na kuainisha maeneo ya vipaumbele ya miradi ya kuhimili athari hizo. Tathmini hii ilifanyika kwa ufadhili wa Serikali ya *Denmark*.

Mheshimiwa Spika, kupitia mfumo wa Miradi ya Ushirikiano chini ya Itifaki ya Kyoto *(Clean Development Mechanism – CDM*) miradi miwili ilipitishwa ya kupunguza kiwango cha hewa mkaa *(Carbon dioxide)* angani. Miradi hii ni:- Mtoni *Landfill Electricity Generation Project;* na *Wind Energy Project,* Singida na Makambako.

Mradi wa Mtoni *Landfill Electricity Generation Project* ni mradi wa miaka 10, unatekelezwa na Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na kampuni ya *Stabile Globus* ya Italia na utatoa umeme wa Megawati 2.5. Mradi huu unatarajia kupunguza hewa mkaa yenye thamani ya dola za Marekani milioni mbili kwa mwaka. Mradi wa Singida na Makambako ni wa uzalishaji Nishati kwa Upepo. Mradi huu ni wa miaka kumi, utazalisha megawati 200 kwa ajili ya gridi ya Taifa na mapato kutokana na mauzo ya hewa mkaa itakayopunguzwa angani, *"carbon credits",* ni zenye thamani ya dola za Marekani milioni 4.5 kwa mwaka. Mradi unamilikiwa na kampuni ya Tanzania ijulikanayo kama *Wind E Tanzania Ltd.* na upo katika hatua ya awali ya maandalizi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais itaratibu utekelezaji wa miradi ya kipaumbele iliyobainishwa katika Programu ya kitaifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Miradi hii itafadhiliwa na *UNEP* na *GEF*. Ofisi ya Makamu wa Rais pia itafanya mapitio ya Mwongozo wa Uwekezaji katika miradi ya *CDM* nchini na itaendelea kuhimiza miradi ya *CDM* na kukuza weledi kwa wadau mbalimbali kuhusu changamoto za mabadiliko ya tabianchi kwa ujumla. Aidha, miradi ya kujenga uwezo wa taasisi na asasi kubaini, kubuni na kutekeleza miradi ya *CDM* itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Kupambana na kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame hususan, shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali (*NGOs*) na Vikundi vya kijamii (*CBOs*). Kwa ushirikiano na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania *(Journalists Environmental Association of Tanzania – JET*), utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha uwezo wa serikali za mitaa katika kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame nchini ulikamilika. Mradi huu ulilenga katika kuzisaidia wilaya tisa kukuza weledi na kutunza kumbukumbu zinazohusiana na shughuli na mipango ya kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame.

Wilaya hizo ni: Singida, Manyoni, Iramba, Magu, Kwimba, Misungwi, Shinyanga, Kishapu na Meatu. Ofisi ya Makamu wa Rais inakamilisha taarifa kuhusu kuenea kwa hali ya jangwa na ukame nchini. Taarifa hii itakuwa mchango wa Tanzania kwenye taarifa ya pamoja ya Umoja wa nchi za Afrika kuhusu kuenea kwa hali ya jangwa na ukame Barani Afrika itakayowasilishwa kwenye Mkutano wa Kumi na Saba wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais, itaendelea na shughuli za kuratibu utekelezaji wa mkataba huu pamoja na kutathmini utekelezaji wa miradi midogo inayotekelezwa na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali na Vikundi vya Jamii. Ofisi ya Makamu wa Rais itafanya tathmini kwa wilaya tisa (9) zilizofaidika na mradi wa kuimarisha uwezo wa serikali za mitaa katika kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu mradi wa Ushirikishwaji wa Wanachi katika Kuhifadhi Maliasili na Usimamizi wa Mazingira, unaotekelezwa kwa msaada wa Serikali ya Marekani. Kazi zifuatazo zilitekelezwa:- kuandaa na kuzindua utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo ya zao la mwani *(Seaweed Development Strategic Plan)* kwa ajili ya maeneo ya Pwani; Kuandaa Mpango wa Wilaya wa Usimamizi wa Maeneo ya Pwani *(District Integrated Coastal Management Action Plan)* kwa ajili ya Wilaya za Rufiji, Mafia na Kilwa; na kuzindua utekelezaji wa Mpango Shirikishi wa Hifadhi ya Vyanzo vya Maji na Usafi wa Mazingira ya maeneo ya bonde la mto Pangani na mto Wami. Aidha, matengenezo ya barabara yenye urefu wa kilomita 100, nyumba za watumishi 12 na vituo 2 vya kufikia wageni yalifanyika katika Hifadhi za Taifa za Tarangire na Manyara. Mradi pia umesaidia vijiji vinavyozunguka hifadhi hizo na eneo la akiba la Ugalla kusimamia maeneo yao ya hifadhi za jamii.

Maeneo hayo ni Burunge, Uyumbu na Ipole. Jumla ya vijiji 30 vimetambuliwa katika Wilaya za Mpanda, Urambo, Uyui na Sikonge ili vianzishe hifadhi za jamii za pamoja *(Wildlife Management Areas)*. Mradi umesaidia vijiji katika Wilaya za Monduli na Simanjiro, kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Vijiji hivyo ni Lolkisale, Naitolya na Emboret. Vilevile, mafunzo yalitolewa kwa wataalamu wawili wa TANAPA na wananchi wa vijiji 19 kuhusu kuzuia ujangili na masuala ya hifadhi na kilimo endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:- kuendelea kusaidia mafunzo na vifaa kwa ajili ya kuzuia ujangili katika maeneo ya Mradi; matengenezo ya barabara katika maeneo ya hifadhi na yale yanayozunguka hifadhi za Tarangire na Manyara; maandalizi ya mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji katika wilaya za Simanjiro na Monduli; na utekelezaji wa mpango shirikishi wa hifadhi ya vyanzo vya maji na usafi wa mazingira ya maeneo ya bonde la mto Pangani na Mto Wami. Chini ya Mradi, Ofisi ya mradi itaendelea kusaidia uboreshaji wa maisha ya wananchi katika maeneo ya pwani kwa kutumia fursa zilizopo bila kuathiri mazingira, ikiwa ni pamoja na ufugaji wa mwotika *(milk fish),* ufugaji wa nyuki katika mikoko, uanzishaji wa zao la paplika na utayarishaji mzuri wa mazao ya samaki ili kupata soko bora.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu mchakato wa utoaji wa Tuzo hii muhimu katika utunzaji wa Mazingira nchini. Mheshimiwa Rais alipokuwa anatoa tuzo kwa mshindi wa 2005/2006 alielekeza kuwa suala la kuingia katika shindano kwa ajili ya Tuzo lisiwe la hiari, badala yake makampuni yote ya uchimbaji madini yakaguliwe na kutathminiwa. Hivyo katika mwaka 2006/2007 makampuni yote yalikaguliwa na kutathminiwa.

Mchakato wa kumpata mshindi wa Tuzo hiyo unakamilishwa. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuratibu mchakato wa kuwapata washindi wa Tuzo kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira na Kuondoa Umaskini,katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kusaidia mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (*NGOs*) katika kutekeleza miradi mbalimbali inayolenga kuhifadhi mazingira na kuondoa umaskini chini ya mradi wa *Multilateral Environmental Agreements (MEAs*).

Jumla ya miradi ishirini na tano ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ilipokelewa. Kati ya miradi hiyo, miradi kumi ilipitishwa na kupatiwa fedha chini ya Mfuko wa kusaidia miradi midogo midogo ya vikundi vya jamii unaofadhiliwa kwa pamoja chini ya mradi wa *MEAs* na Programu ya Mazingira na MKUKUTA. Vikundi vilivyopatiwa fedha chini ya Mfuko huu ni kutoka mikoa ya Ruvuma, Iringa, Mwanza, Dodoma, Mtwara, Singida, Pwani, Mara, Kagera na Morogoro. Miradi hii imegharimu jumla ya shilingi milioni 142.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi iliyopata ufadhili. Aidha, awamu ya pili ya Programu ya Mazingira na MKUKUTA inaandaliwa na utekelezaji wake unatarajiwa kuanza katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha. Katika kipindi hiki tutaendelea pia na uratibu wa shughuli za Kamati ya Wadau wa Mazingira ambayo hujumuisha pia wafadhili *(Environmental Working Group).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utekelezaji wa Itifaki ya Cartagena, katika kipindi cha 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais ilitoa mafunzo kwa wadau mbalimbali juu ya Muundo na Mwongozo wa usimamizi wa viumbe na bidhaa ambavyo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki. Muundo *(National Biosafety Framework)* na Mwongozo *(National Biosafety Guidelines)* ulisambazwa kwa wadau mbalimbali.

Vilevile Kamati ya Kitaifa *(National Biosafety Committee)* iliundwa. Kamati ina wajumbe kutoka sekta mbalimbali, vyuo vya elimu ya juu, asasi za serikali na zisizo za serikali. Warsha mbili za mafunzo kwa wataalamu wapatao 50 kutoka sekta na vyuo vya elimu ya juu, asasi za serikali na zisizo za serikali, ziliendeshwa. Tovuti ilianzishwa ili kuboresha ubadilishanaji taarifa hapa nchini na nje ya nchi kuhusu viumbe, bidhaa na viumbe ambavyo vinasaba vyake vimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki. Tovuti itawezesha wadau kupata taarifa mbalimbali juu ya matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais ilipata heshima ya kuwa mwenyeji wa mikutano miwili ya kimataifa ya kubadilishana uzoefu kuhusu usimamizi wa mazingira dhidi ya athari za bioteknolojia ya kisasa. Mkutano wa kwanza ulihusisha nchi kutoka kanda ya Afrika Mashariki na Kati. Nchi hizo ni:- Burundi, Comoro, *Djibout*, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ethiopia, Eritrea, Kenya, Sudani, Rwanda, Uganda, *Cameroon*, Chadi, Sao *Tome* na *Principe*, *Gabon, Equitorial Guinea*, Jamhuri ya Afrika ya Kati, na Tanzania. Mkutano wa pili ulihusisha nchi kutoka Bara la Asia, Afrika, na nchi kutoka Bara la Ulaya ya Mashariki na Kati. Nchi hizo ni:- Jamhuri ya *Czech, Cambodia, Moldova, Lithuania, Vietnam, Estonia, Mauritius, Tunisia*, Kenya, Uganda, *Cameroon,* Namibia, India, na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi wa Mazingira dhidi ya Athari za Biotekinolojia ya Kisasa, hususan kujenga uwezo wa taasisi na wadau ili kutambua bidhaa, mazao na viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki. Aidha, utoaji wa elimu na kukuza weledi kwa wadau mbalimbali kuhusu usimamizi wa mazingira dhidi ya athari ya biotekinolojia ya kisasa utaendelea. Kanuni kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa zitakamilishwa na kusambazwa kwa wadau. Mfumo, Mwongozo na Kanuni kuhusu usimamizi wa mazingira dhidi ya bioteknolojia ya kisasa utatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na kusambazwa kwa wadau mbalimbali. Ili kuboresha uwezo wa wadau katika upashanaji habari kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa, mafunzo yataendelea kutolewa. Aidha, wadau watawezeshwa kupata vitendea kazi kwa ajili ya utafiti na kutambua bidhaa, mazao na viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki na kompyuta kupitia mradi huo kulingana na uwezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Programu ya Usafi wa Mazingira, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira *(UNEP),* na Kituo cha Uzalishaji Bora Tanzania (CPCT), iliendesha semina ya kimataifa kuhusu uzalishaji bora na matumiziendelevu iliyofanyika Arusha, Novemba 2006. Madhumuni ya semina yalikuwa ni kuwahamasisha

washiriki kuhusu dhana ya uzalishaji bora na matumizi endelevu. Washiriki walijadili mikakati na mbinu mbalimbali za kuinua dhana hii katika sekta za kilimo, utalii, nishati na masuala ya usimamizi wa taka. Wataalamu 130 walishiriki katika semina hii. Wataalamu hao walitoka *Austria, Benin, Costa Rica*, Misri, Ethiopía, Ujerumani, Ghana, *Finland*, Ufaransa, India, Italia, Kenya, *Lebanon*, Marekani, M*auritius, Mexico, Morocco*, Msumbiji, Uholanzi, *Níger,* Nigeria, Urusi, Rwanda, *Senegal, Slovakia*, Afrika Kusini, *Sri Lanka, Sweden,* Tanzania, Tunisia, Uganda, Zambia, na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Kituo kiliendelea kuratibu shughuli za Sekretarieti ya *"Roundtable on Sustainable Consumption and Production"* katika Bara la Afrika. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea na ukarabati wa jengo la ofisi za Kituo ambao unafanyika kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, shughuli zingine zilizofanyika ni:- Kufanya tathmini ya uzalishaji bora na matumizi bora ya nishati katika kiwanda cha karatasi kilichopo Moshi; Kutayarisha ripoti ya hali ya uchafuzi wa mazingira unaotokana na viwanda katika Manispaa ya Morogoro, na kuendesha warsha ya kukuza ufahamu wa dhana ya uzalishaji bora na matumizi endelevu kwa wadau 40 wa Bonde la Ziwa Victoria kutoka mikoa ya Kagera, Mara na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, washiriki walitoka idara na taasisi za serikali, Halmashari za Majiji na Manispaa, mamlaka za maji, viwandani, mashirika yasiyo ya kiserikali, vyama vinavyoshughulikia masuala ya viwanda, makampuni yanayojishughulisha na uchimbaji madini na miradi inayohusiana na usimamizi wa mazingira. Aidha, Kituo kilitayarisha Mpango wa utekelezaji kwa ajili ya kuboresha mazingira katika kiwanda cha nguo cha Karibu *Textile Mill Ltd.*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kukarabati jengo la ofisi za Kituo na kununua samani kwa ajili ya ofisi hiyo. Kituo kitafanya shughuli zifuatazo:- kuandaa na kuendesha semina ya kitaifa juu ya mafanikio ya utekelezaji wa mbinu za uzalishaji bora; kutayarisha ripoti ya uchafuzi wa mazingira kutokana na shughuli za viwanda kwa ajili ya Manispaa zinazohitaji huduma hiyo; kufanya tathmini ya uzalishaji bora na matumizi bora ya nishati na kutayarisha mipango ya utekelezaji wa hifadhi ya mazingira katika viwanda vinavyohitaji huduma hizo; na kutekeleza mradi wa kukuza ufahamu wa dhana ya uzalishaji bora na matumizi endelevu kwa wadau mbalimbali katika Bonde la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa *Montreal* unaohusu kusitisha matumizi ya kemikali zinazomong'onyoa tabaka la hewa ya Ozoni angani. Mkutano wa wafanyabiashara wanaoingiza kemikali zinazodhibitiwa na Mkataba wa *Montreal* ulifanyika Dar es salaam mwezi Agosti 2007. Katika Mkutano huo, wafanyabiashara hao walielimishwa kuhusu majukumu ya nchi katika kudhibiti matumizi ya kemikali zinazoharibu tabaka la hewa ya Ozoni; na wajibu wao ikiwa ni pamoja na kukuza uingizaji wa kemikali mbadala nchini. Ofisi ya Makamu wa Rais iliendesha semina ya

wadau mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam katika kuadhimisha siku ya Ozoni Duniani ambayo hufanyika tarehe 16 Septemba kila mwaka.

Semina ililenga kuelimisha wadau kuhusu umuhimu wa tabaka la hewa ya Ozoni na bidhaa zenye kemikali zinazoharibu tabaka hilo, hali ya utekelezaji wa majukumu yetu chini ya Mkataba wa *Montreal.* Washiriki waliwakilisha Idara za Serikali, shule, karakana zinazohudumia viyoyozi na majokofu na vyombo vya habari. Jumla ya wadau 80 walishiriki. Aidha, warsha tatu za mafunzo za kikanda ziliendeshwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma kwa mafundi mchundo wanaohudumia viyoyozi na majokofu. Katika mafunzo hayo mafundi walielimishwa mbinu bora za kuhudumia vifaa vyenye kemikali zinazodhibitiwa na Mkataba wa *Montreal*. Mafunzo yalitolewa kwa vitendo jinsi ya kunasa na kurejeleza gesi kwenye vifaa hivyo ili kupunguza matumizi ya gesi mpya na kuimarisha biashara zao.

Washiriki wa warsha hizi walitoka mikoa ya Arusha, Tanga, Morogoro, Zanzíbar, Dar es Salaam, Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Dodoma, Tabora, Kilimanjaro, Singida, Iringa na Kigoma. Jumla ya mafundi mchundo 65 walinufaika na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008 shughuli zifuatazo zitafanyika:- Kukuza weledi wa umma kuhusu mbinu za kulinda tabaka la hewa ya Ozoni kwa kuhusisha vyombo mbalimbali vya habari; kutoa mafunzo kwa mafundi mchundo wa majokofu na viyoyozi kuhusu njia bora za kuhudumia vifaa hivyo ambazo haziathiri tabaka la Ozoni; na kuelimisha wadau kuhusu kanuni za kusimamia uingizaji na matumizi ya gesi zinazoharibu tabaka la hewa ya Ozoni. Hatua hizo zitaisaidia Tanzania kutekeleza majukumu yake chini ya Mkataba wa *Montreal*, hususan kusitisha matumizi ya kemikali aina ya *"Chlorofluorocarbons* (*CFCs*)" ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa *Basel* unaohusu udhibiti wa usafirishaji na utupaji wa taka za sumu na taka nyingine baina ya nchi na nchi na Mkataba wa Bamako ambao unazuia uingizaji wa taka za sumu barani Afrika. Mkataba wa *Basel* umeweka taratibu za kimataifa za kudhibiti usafirishaji na utupaji wa taka za sumu na za kawaida baina ya nchi zinazozalisha taka za aina hii na zile zinazopokea kwa madhumuni ya kurejereza au kuziharibu. Katika kipindi hiki, Ofisi ya Makamu wa Rais ilianza maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa usimamizi wa taka nchini kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu kishiriki cha masuala ya Ardhi na Usanifu Majengo (*UCLAS)*; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; na Mashirika yasiyo ya kiserikali. Mkakati huu utakuza mbinu mbalimbali za kupunguza utoaji wa taka mahali zinapozalishwa na kudhibiti madhara kwa afya na kwa mazingira katika michakato ya usimamizi wa taka za aina mbalimbali. Majukumu ya wadau mbalimbali yatabainishwa.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba Bunge lako Tukufu katika Kikao cha Sita, mwezi Februari 2006 liliridhia Mkataba wa kuundwa kwa Kituo cha Kanda ya

Afrika cha Usimamizi wa taka kilichopo Pretoria, Áfrika Kusini. Kituo kinaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Mtanzania ambaye amesimamia mchakato wa uanzishaji wa Kituo hiki tangu mwaka 2000. Kituo kinafanya kazi chini ya Mkataba wa *Basel*. Shuguhuli kuu za Kituo ni kutoa mafunzo na kueneza teknolojia salama katika usimamizi wa taka. Hadi sasa nchi tano zimeridhia Mkataba wa kuundwa kwa Kituo hiki. Nchi hizo ni: Botswana, Nigeria, Namibia, *Mauritius* na Tanzania. Kituo kinatarajiwa kuhudumia nchi 21 za Kiafrika zinazozungumza lugha ya Kiingereza na nchi nyingine ambazo zitapenda kupata huduma ya kituo hiki. Nchi hizi ni Afrika Kusini, Botswana, Eritrea, Ethiopía, Gambia, Ghana, Liberia, Kenya, Lesotho, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Nigeria, Rwanda, *Sychelles*, *Swaziland,* Tanzania, Uganda, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2006/07 Kituo kilifanya shughuli zifuatazo:- kuhamasisha nchi nyingine kuridhia Mkataba wa kuundwa kwa Kituo hicho; kuboresha mpango wa kazi wa Kituo ikiwa ni pamoja na kuingiza shughuli za kuinua ushirikiano na mikataba mingine ya kimataifa inayohusu masuala ya kemikali za hatari na zile zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu; kuandaa maandiko ya miradi mbalimbali na kuiwasilisha kwa wahisani; kuendesha warsha ya mafunzo kuhusu usimamizi wa taka zenye sumu kwa maofisa wa Idara na Taasisi za Serikali; na kuendesha semina ya kuhamasisha viongozi wa ngazi za juu serikalini kuhusiana na usimamizi wa taka zenye sumu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais itafanya shughuli zifuatazo:- kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka nchini; kuratibu shughuli za Kituo na kuandaa programu ya mafunzo kwa wadau mbalimbali kuhusu usimamizi wa taka zenye sumu na taka za kawaida kutokana na shughuli za sekta ya Afya, Viwanda na Usafirishaji. Kituo kitafanya shughuli zifuatazo:- kuboresha mkakati wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za kituo; kuandaa maandiko ya miradi kwa kushirikiana na nchi husika na kuiwasilisha kwa wahisani; na kuendesha mafunzo ya kuimarisha ushirikiano na programu za kimataifa na za kikanda zinazotekelezwa chini ya mikataba mbalimbali ya kimataifa kuhusu kemikali. Shughuli nyingine ni kuandaa programu ya kanda ya mafunzo kuhusu usimamizi wa kemikali na taka za sumu; na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mkataba wa *Basel* na kuiwasilisha Sekretarieti ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taka za Mifuko ya Plastiki, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) iliendelea kuratibu utekelezaji wa tamko la serikali la kupiga marufuku utengenezaji, uagizaji, uuzaji, ununuzi na matumizi ya mifuko ya plastiki laini na ile ya kufungia maji na maji ya matunda. Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria iliandaa kanuni za kutekeleza Tamko hilo. Kanuni hizi zimeanza kutumika kuanzia 1 Oktoba, 2006. Katika uperembaji wa utekelezaji wa Tamko hilo uliofanyika katika baadhi ya Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji, ilibainika kuwa mifuko laini bado inatengenezwa nchini katika baadhi ya makampuni ya bidhaa za mifuko ya plastiki.

Makampuni hayo yameagizwa kusitisha uzalishaji wa bidhaa hiyo mara moja. Utengenezaji wa mifuko ya kufungia maji umesitishwa. Aidha, miji imeanza kuwa safi baada ya mifuko na viroba vya maji na maji ya matunda kuondoshwa katika soko na matumizi ya mifuko laini kupungua. Hata hivyo, Halmashuri za Miji hazijaweka miundombinu ya kurejeleza taka, japokuwa jamii imeendelea kuhamasishwa kushiriki katika ukusanyaji na urejelezaji wa taka. Hivyo, asilimia kubwa ya taka zinazokusanywa mijini hutupwa katika madampo ambayo hayajaandaliwa kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji kuboresha usimamizi wa taka kwa kutumia mikakati na mbinu mbalimbali za kulinda mazingira ikiwa ni pamoja na kuzitumia kuzalisha nishati na kuzirejeleza ili kutengeneza bidhaa mbalimbali. Ofisi ya Makamu wa Rais itafanya tathmini ya utekelezaji wa hatua za udhibiti wa taka za plastiki kwa nia ya kuchukua hatua za ziada itakapobidi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mazingira wa Dunia *(GEF)* unafadhili shughuli za mazingira katika maeneo sita ambayo ni: kudhibiti upotevu wa bioanuai; mabadiliko ya tabianchi; maji ya kimataifa; kumomonyoka kwa tabaka la Ozoni; uharibifu wa ardhi; na kemikali zinazodumu muda mrefu kwenye mazingira *(Persistent Organic Pollutants - POPs*). Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais, ilipokea miradi 52, kuichambua na kuipitisha kwa ajili ya ufadhili wa Mfuko wa *GEF* wa kufadhili miradi midogo midogo unaosimamiwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP)* hapa nchini. Jumla ya miradi ya mazingira 72 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.5 ilipata ufadhili kutoka Mfuko huu. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ilibainisha miradi mikubwa na ya kati ya kipaumbele kwa ajili ya ufadhili chini ya mfumo mpya wa uendeshaji na ugawaji wa fedha za *GEF (GEF Resource Allocation Framework).*

Mheshimiwa Spika, katika mfumo huu mpya, Tanzania imetengewa dola za kimarekani shilingi milioni 12.8 katika eneo la bioanuai na shilingi milioni 4.8 katika eneo la mabadiliko ya tabianchi kwa kipindi cha miaka minne ijayo. Tayari jumla ya miradi 9 ya vipaumbele katika eneo la bioanuai imebainishwa kwa ajili ya ufadhili chini ya mfumo huu. Maeneo ambayo yatafaidika na miradi hii ni pamoja na: Bonde la Ziwa Nyasa; Usangu; Hifadhi ya Taifa ya Saadani; Hifadhi ya Rungwe; Hifadhi ya Taifa ya Kitulo, na Milima ya *Livingstone*; Bonde la mto Kagera; Singida; na Ukanda wa Pwani, ikiwa ni pamoja na Zanzibar. Katika eneo la mabadiliko ya tabianchi bado maeneo ya kipaumbele yanaainishwa kwa kushauriana na *GEF* na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Ofisi ya Makamu wa Rais pia iliendesha mikutano miwili ya kitaifa kuhusu *GEF* kwa lengo la kufafanua mfumo mpya wa uendeshaji, dira na mikakati mbalimbali ya *GEF* ili kukuza weledi kuhusu shughuli za Mfuko huu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kusimamia na kuratibu shughuli za *GEF* nchini kwa kuhamasisha na kushauri vikundi kuandaa miradi kwa ajili ya ufadhili wa *GEF* na kufanya uperembaji wa

miradi iliyopata ufadhili wa *GEF* katika mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Mwanza, Iringa na Arusha.

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu linavyofahamu, suala la mazingira ni ajenda pana, yenye sura mbili: hifadhi ya mazingira na kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Ushirikishwaji wa wananchi, na kuinua kiwango cha elimu na uelewa wa wananchi katika kuhifadhi mazingira ni suala muhimu. Serikali inasisitiza dhana hii ya msingi ya maendeleo ya watu kuletwa na watu wenyewe, na makundi yao katika kuongoza juhudi za kuhifadhi mazingira ya nchi yetu. Kipimo cha mafanikio katika ajenda hii muhimu lazima kijumuishe kiwango cha ushiriki wa wananchi wenyewe. Masuala ya mazingira yanagusa sekta, maisha na shughuli nyingi za watu binafsi, vikundi, taasisi, makampuni na mashirika mbalimbali ya Serikali na yasiyo ya Serikali. Juhudi za pamoja ndio msingi wa mafanikio katika hifadhi ya mazingira. Sheria zitatumika kwa wale wanaoharibu mazingira na usimamizi wa sheria hizo utaboreshwa. Hata hivyo, suala la msingi kuliko yote ni kwa kila mwananchi kushiriki katika shughuli za hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni pamekuwa na ongezeko la mwamko kwa baadhi ya wananchi na vikundi mbalimbali vya jamii kuhusu athari za uharibifu wa mazingira na kutaka kushiriki katika shughuli za hifadhi ya mazingira. Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kushirikiana na Wizara na taasisi mbalimbali, kuimarisha na kukuza ushirikishwaji wa wananchi, ikiwa ni pamoja na kuwapatia maarifa, ujuzi na stadi za kuwawezesha kuyaelewa na kuyatawala vema mazingira kwa manufaa yao wenyewe, Taifa na kwa faida ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 5 Juni kila mwaka, Tanzania huungana na nchi nyingine kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Mwaka huu, kauli mbiu ya Siku ya Mazingira Duniani Kimataifa ilikuwa **"**Kuongezeka kwa joto duniani na kuyeyuka kwa barafu" na kitaifa ilikuwa **"**Hifadhi ya Mazingira; Panda miti na kuitunza**".** Kimataifa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka huu yalifanyika nchini *Norway* na kitaifa yalifanyika mkoani Mtwara. Maudhui ya ujumbe huu kitaifa yalikuwa kuelimisha na kuhamasisha wananchi wote juu ya utunzaji wa mazingira hususan kupanda miti, hasa ile ya asili, na kuitunza, kuhifadhi misitu na uoto wa asili. Ujumbe ulilenga kuelimisha na kuhamasisha wananchi vijijini, mijini, kuepuka na kudhibiti uchomaji moto wa misitu na ukataji miti kiholela na uchafuzi wa mazingira. Sherehe za kitaifa zilifanyika kwa shughuli mbalimbali, nchi nzima kwa kipindi cha wiki moja, hadi siku ya kilele tarehe 5 Juni. Shughuli hizo ni pamoja na upandaji na palizi ya miti, mafunzo mbalimbali kuhusu mazingira, warsha na mashindano ya nyimbo na ngonjera ili kukuza weledi juu ya umuhimu wa hifadhi na usafi wa mazingira, na utoaji wa zawadi kwa washindi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru wote walioshiriki katika maadhimisho haya. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa uongozi wa Mkoa wa Mtwara kwa kukubali kuwa mwenyeji wa maadhimisho hayo kitaifa na kwa wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Watanzania wote kwa ushiriki wao.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa pili tangu Sheria ya Mazingira Namba 20 ya Mwaka 2004 ianze kutekelezwa. Katika kipindi hiki Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, limeendelea kutekeleza kazi zake kama zilivyoainishwa katika sheria hiyo. Kwa mujibu wa sheria hiyo, majukumu makuu ya Baraza ni kusimamia utekelezaji wa sheria, kufanya mapitio ya taarifa za tathmini ya athari kwa mazingira ya shughuli za maendeleo, kuanzisha na kutekeleza mipango ya mazingira na utafiti, na kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/07, Baraza liliendelea kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira. Baraza liliandaa Rasimu za Mwongozo wa Ukaguzi wa Maeneo Mbalimbali *(Site Specific Inspection Procedures),* Mwongozo wa Kitaifa wa Uchunguzi wa Mazingira *(National Investigation Manual),* Miongozo ya Kuchukua Hatua za Kisheria *(National Prosecution Procedure),* na Miongozo mingine *(Environmental Monitoring Tools)* itakayotumika kama nyenzo kwa Maafisa Wakaguzi wa Mazingira *(Environmental Inspectors).*

Baraza lilikagua viwanda 18 katika miji ya Dar es Salaam, Morogoro, Kibaha, Arusha, Moshi, Bukoba, Tanga na Mwanza kubaini hali halisi ya uchafuzi wa mazingira unaotokana na viwanda na kutoa ushauri jinsi ya kuondokana na uchafuzi huo. Katika kipindi cha mwaka 2006/07, Baraza lilishirikisha wenye viwanda vitano (5) vya chuma vilivyoko Dar es Salaam kuanzisha utaratibu wa kuandaa Mpango bora wa Udhibiti wa Mazingira *(Environmental Management System)* katika viwanda vyao ili kuhakikisha wanazalisha bidhaa zao kwa ubora zaidi bila ya kuathiri mazingira. Pia Baraza lilifanya utafiti wa awali kuhusu chanzo cha uchafuzi wa mfereji wa maji ya mvua (utokanao na maji taka) eneo la Mikocheni, Dar es Salaam na kuchua hatua za kukabiliana na uchafuzi huo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/07, Baraza lilisimamia utekelezaji wa kanuni iliyopiga marufuku matumizi ya baadhi ya mifuko ya plastiki laini na ile ya kufungia maji na maji ya matunda kwa kutoa elimu kwa wananchi kupitia magazeti na vipindi maalumu vya mahojiano kwa njia ya redio na televisheni juu ya athari za kiafya na mazingira zinazotokana na taka za plastiki.

Baraza lilifanya ukaguzi wa kushitukiza kwa baadhi ya viwanda na maduka makubwa yaliyopo Dar es Salaam kubaini hali ya utekelezaji wa kanuni hii. Utafiti huo ulibaini kuwa baadhi ya wafanyakazi walipoteza kazi na viwanda kupoteza mapato. Hata hivyo, kitendo hiki cha kupiga marufuku kimezaa matunda mazuri kwa kupungua kwa taka za plastiki katika mazingira. Baraza linaendelea kushirikiana na wenye viwanda kutafuta mifuko mbadala.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/07, Serikali ilisaini mkataba na Benki ya Dunia kuhusu kuondoa Madawa Chakavu *nchini (Africa Stockpiles Programme-ASP),* Baraza limeanza utekelezaji. Ili kudhibiti uchafuzi wa Bonde la Mto Msimbazi, Baraza lilianza kutekeleza mradi wa utafiti na udhibiti wa vyanzo vya uchafuzi wa bonde hilo. Baraza liliendelea kuratibu mradi wa tathmini ya uchafuzi wa hewa *(Air Quality Monitoring)* katika jiji la Dar es Salaam kwa kukusanya taarifa

(takwimu) kuhusu uchafuzi wa hewa katika maeneo ya Tandika, Kariakoo, Mwenge na Gerezani kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2007/08, Baraza litaendelea na utekelezaji wa Programu ya miaka minne ya kuondosha mlundikano wa madawa chakavu ya kilimo. Baraza litaendelea na mradi wa tathmini ya uchafuzi wa hewa unaofanyika katika jiji la Dar es Salaam kwa ushirikiano na Halmashauri za Manispaa. Pia Baraza limepanga kufanya ukaguzi wa viwanda vilivyopo katika miji ya Mwanza, Musoma, Tanga na Mbeya na kuchukua hatua za kudhibiti uchafuzi wa mazingira utokanao na viwanda hivyo. Vilevile Baraza litaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kudhibiti Uchafuzi wa Bonde la Mto Msimbazi na kuhimiza uzingatiaji wa upigaji marufuku wa Serikali kuhusu matumizi ya mifuko ya plastiki. Pindi watakapoteuliwa Wakaguzi wa Mazingira *(Environmental Inspectors)* watapewa mafunzo kuhusu kanuni za ukaguzi wa mazingira kwa ajili ya udhibiti wa uchafuzi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira (*TAM*), Baraza lilifanya mapitio ya taarifa 45 za Tathmini ya Athari kwa Mazingira *(TAM)* na kutoa ushauri. Hati 22 za miradi ya uwekezaji zilitolewa ili kuhakikisha uwekezaji endelevu. Miradi iliyopewa Hati ni ya uchimbaji madini, viwanda vya minofu ya samaki, nishati, utafutaji na uchimbaji wa gesi na mafuta, ujenzi wa barabara na ujenzi wa hoteli na vivutio vya kitalii. Zaidi ya miradi 100 ilisajiliwa na ipo katika hatua mbalimbali za mchakato wa mapitio ili hatimaye kutolewa uamuzi.

Taarifa 5 za ukaguzi wa mazingira *(Environmental Audit Reports)* zilipitiwa na ushauri wa namna ya kuboresha masuala ya mazingira wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo ulitolewa kwa kushirikiana na sekta za Maji na Nishati. Baraza lilifanya uchambuzi wa masuala ya kuzingatiwa na pia kutoa miongozo wakati wa utekelezaji wa miradi inayohusu sekta hizo. Pia Baraza lilitoa mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (*TAM*) hususan katika kuandaa miongozo na kuelimisha wadau juu ya umuhimu wa tathmini ya athari. Aidha, Baraza liliendesha mafunzo katika wilaya ya Mbarali na kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kama hayo katika wilaya za Mafia, Rufiji na Kilwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2007/2008, Baraza linatarajia kufanya mapitio ya taarifa zaidi ya 100 za Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kushauri ipasavyo. Vilevile litapitia taarifa za ukaguzi wa mazingira na kutoa ushauri wa kuboresha mazingira wakati wa utekelezaji wa miradi. Mapitio ya fomu za usajili wa miradi, taarifa za awali na mipango ya usimamizi wa mazingira na masuala ya jamii yataendelea kufanyika kwa lengo la kudhibiti athari kwa mazingira zinazoweza kusababishwa na shughuli za maendeleo. Baraza pia litafuatilia maagizo yaliyotolewa katika hati za *TAM* kwa miradi 22. Kwa kushirikiana na sekta mbalimbali na Serikali za Mitaa, Baraza litaandaa miongozo ya tathmini ya athari ya kisekta na ile ya kutumika wakati wa kufanya uchambuzi wa masuala ya kuzingatiwa wakati wa kutekeleza miradi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza mipango ya mazingira na utafiti, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Baraza liliboresha mpango wa Taifa wa utafiti wa masuala ya mazingira *(National Environmental Research Agenda- NERA*) kutokana na maoni ya wadau katika ngazi za wilaya, vijiji na warsha ya kitaifa iliyohusisha wadau mbalimbali kutoka taasisi za kitafiti. Utekelezaji wa mpango huu utaanza katika kipindi cha mwaka 2007/2008. Kipindi cha mwaka 2006/2007, Baraza liliandaa rasimu ya miongozo itakayotumika katika kutambua maeneo tete *(environmental hotspots).* Rasimu hiyo itaboreshwa katika kipindi cha mwaka 2007/2008 na Baraza litaanza kuainisha na kuweka mikakati ya kuhifadhi maeneo hayo. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 utafiti wa awali *(reconnaissance survey)* ili kuainisha maeneo oevu yaliyoathirika katika ukanda wa Kusini magharibi (Rukwa) na ukanda wa Magharibi (Kagera na Kigoma) ulifanyika.

Mheshimiwa Spika, Baraza pia lilifanya utafiti wa awali juu ya hali ya milima nchini. Aidha, utafiti wa kina wa ikolojia ulifanyika katika safu za milima ya *Livingstone* iliyoko wilaya za Rungwe, Makete, Ludewa na Mbinga wakati wa kipindi cha mvua. Utafiti huu utakamilika mwaka 2007/2008 kwa kufanya Tathmini ya Mifumo ya Kiikolojia ya Milima ya *Livingstone* – Ruvuma wakati wa kipindi cha kiangazi kwa ufadhili wa mradi wa Umasikini na Mazingira *(Poverty Environment Linkage Project).*

Katika kipindi cha mwaka 2007/2008 Baraza litaandaa miongozo mbalimbali ikiwemo ya kusaidia utafiti wa milima na ya kuhifadhi mito na kingo zake, pamoja na kufanya utafiti katika milima itakayoainishwa kwa kutumia miongozo itakayoandaliwa.

Mwaka 2006/2007 Baraza liliendelea kusimamia utekelezaji wa mkakati wa uhifadhi wa mazingira ya maeneo ya pwani, kwa kuendelea kuzisaidia wilaya za Bagamoyo, Pangani na Mkuranga kutekeleza mikakati yao kupitia Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Pwani (*TCMP-SUCCESS*). Shughuli hizo zitaendelea kutekelezwa katika mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2007/2008, kupitia Mradi wa Usimamazi wa Mazingira ya Pwani (*MACEMP*), Baraza litaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu katika Wilaya za Rufiji, Kilwa na Mafia katika kutekeleza mipango ya Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani (*Integrated Coastal Environment Management Action Plan)*. Baraza pia litakusanya taarifa zitakazotumika kuandaa ripoti ya hali ya mazingira ya pwani (*State of the Coast Environment Report).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/07, Baraza kwa kushirikiana na wadau wengine, liliendesha kongamano la kisayansi na maonyesho juu ya rasilimali za pwani na Bahari. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Baraza litaandaa na kuendesha kongamano la nne la kisayansi nchini. Pia Baraza litaandaa warsha katika ngazi ya wilaya kuhusu mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi *(adaptation to climate change).* Pia Baraza litaainisha na kukubaliana kuhusu viashiria vitakavyosaidia ufuatiliaji *(monitoring)* wa mifumo ikolojia na mazingira. Aidha**,** Baraza litashiriki katika awamu ya pili ya mradi wa hifadhi ya Ziwa Victoria (*LVEMP).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2006/2007, Baraza kwa kupitia Mradi wa Kihansi (*LKEMP*) liliendelea kuratibu, kufadhili na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kuhifadhi Mazingira na Bioanuwai ya Bonde la Kihansi *(Updated Environmental Management Plan)* na Mpango wa Kuhifadhi Eneobonde la Mto Kihansi *(Landscape-Wide Conservation Plan)* unaolenga kuhifadhi vyanzo vyote vya maji ya Mto Kihansi na rasilimali za misitu katika wilaya za Kilolo, Mufindi na Kilombero. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Baraza litaendelea kuratibu na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mkakati na mipango endelevu ya kuhifadhi rasilimali na viumbe adimu katika Korongo la Kihansi na eneobonde la Mto Kihansi kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya husika na wadau wote. Baraza litaratibu uandaaji na utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa Kihansi.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa changamoto zinazoikabili nchi yetu ni uelewa mdogo wa wananchi kuhusu masuala ya mazingira. Ili kukuza uelewa huu, Baraza lilitoa elimu ya mazingira kwa kutembelea maeneo mbalimbali na kujadiliana na wadau jinsi ya kukuza uelewa na kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira. Wadau hao ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, watendaji wa Wilaya, Madiwani na mashirika yasiyo ya kiserikali katika wilaya kadhaa za mikoa ya Mbeya, Shinyanga, Morogoro, Kilimanjaro, Tabora na Kigoma.

Baraza liliandaa warsha ya Wanahabari 40 ili kukuza uelewa wao katika kuandika habari za mazingira. Baraza pia lilihamasisha na kutoa elimu kwa umma kwa kuandaa vipindi 24 vya televisheni, 15 vya redio na kuandika makala 18 katika magazeti. Pia Baraza lilichapisha na kusambaza kalenda 3,000, vipeperushi 15,000 na fulana 3,000 ili kueneza ujumbe wa namna ya kutunza na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Baraza lilishirikiana na Shirika la Posta kuandaa na kuzindua stempu za mazingira, liliendesha mashindano na kutoa zawadi kwa washindi wa Wizara tatu zilizofanya vizuri katika kufanikisha utunzaji wa mazingira mijini na shule za msingi zilizoandika insha nzuri kuhusu mazingira. Wizara hizo ni Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii, Maji na Mambo ya Ndani. Aidha, Baraza lilishiriki katika maonyesho na maandamano yaliyoandaliwa na Mikoa ya Mtwara, Iringa na Dar es Salaam. Pia Baraza lilishiriki maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika Machi, 2007.

Katika kipindi hicho Baraza liliimarisha huduma za maktaba kwa kuongeza vitabu na majarida na kuhudumia wateja zaidi ya 800. Tovuti ya Baraza iliboreshwa kwa kuingiza taarifa nyingi zaidi, Tovuti ilitumiwa na zaidi ya wadau 1,200. Aidha, ripoti ya mapendekezo ya namna ya kuandaa mfumo wa mawasiliano (*Central Environmental Information System*) iliwasilishwa.

Mwaka 2007/2008, Baraza litashiriki kikamilifu katika maadhimisho ya siku ya mazingira Duniani, siku ya Wanawake, Wakulima, Ardhi Oevu, na Wiki ya Maji.

Baraza liliandaa warsha kwa mikoa iliyoathiriwa na wakimbizi ambayo ni Kigoma, Rukwa na Kagera. Baraza pia limeandaa Rasimu ya Mkakati wa Kukabiliana na Uharibifu uliosababishwa na wakimbizi hao.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2007/2008 Baraza litaandaa na kusambaza machapisho mbalimbali. Baraza litatayarisha vipindi 30 vya televisheni na redio kupitia vyombo vya habari; makala 25 zitachapishwa katika magazeti; na litatoa elimu kwa umma kwa kupitia Maktaba na Tovuti. Kwa kupitia Tovuti yake (*www.nemctan.org*), Baraza litaainisha miradi yote iliyopatiwa vyeti vya *TAM*, viwanda vilivyochukuliwa hatua za kisheria, ripoti za utafiti, na machapisho mbalimbali ya Baraza.

Pia Baraza litakamilisha maandalizi ya programu ya kitaifa ya elimu kwa umma kuhusu mkakati wa kuhifadhi mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, na litatembelea mikoa ya Iringa, Mwanza, Rukwa, Pwani, Mtwara na Lindi ili kushirikiana na Halmashauri husika kukuza uelewa wa masuala ya utunzaji mazingira na maendeleo endelevu.

Baraza litaandaa warsha tatu zitakazohusisha wadau mbalimbali ili kupata ushauri na mapendekezo ya namna ya kuboresha utoaji wa elimu ya mazingira kwa umma na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utawala na maendeleo ya watumishi, Baraza linaendelea na jitihada za kupata makazi yake ya kudumu kwa kutengewa viwanja vilivyopo eneo la Goba wilaya ya Kinondoni. Sehemu ya bajeti ya 2007/08 itatumika kwa ajili ya kulipa fidia kuhusiana na viwanja hivyo.

Baraza pia limelenga kuwafikia wadau wake ili kubaini matatizo yahusuyo usimamizi na uhifadhi wa mazingira na kuharakisha huduma kwa kuanzisha uwakilishi katika kanda *(zonal nodes)*.

Mheshimiwa Spika, nidhamu ya watumishi wa Baraza imeendelea kudumishwa kwa kukuza weledi wao katika suala zima la utawala bora. Miongoni mwa semina zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2006/07 ni pamoja na: Mapambano dhidi ya janga la ukimwi; Utawala Bora na Mkakati wa Kuzuia Rushwa sehemu za kazi; Tathmini ya utendaji kazi na motisha kwa watumishi.

Kuhusu mafunzo, Baraza limeendelea kufadhili baadhi ya watumishi na pia kutafuta ufadhili kutoka asasi mbalimbali. Watumishi tisa wanasomea shahada za elimu ya juu (*Ph.D* na uzamili) na watumishi wawili wanasomea shahada ya kwanza. Pia Baraza limeendelea kushiriki katika michezo ili kuimarisha afya za wafanyakazi na mahusiano.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2006/2007, Baraza lilizingatia masuala ya utawala bora hasa matumizi ya fedha na mali ya umma kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 na Sheria ya Fedha *(Public Finance Act)* ya mwaka 2001. Katika mwaka wa fedha wa 2007/08, Baraza linategemea kujenga uwezo zaidi wa

wafanyakazi katika usimamizi wa fedha, Sheria ya manunuzi na kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa ndani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2006/07, Baraza limekabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa bajeti hii.

Changamoto hizo ni pamoja na ufinyu wa ofisi, hali amabayo imesababisha watumishi kufanyia kazi katika majengo manne tofauti, uhaba wa wataalamu kuweza kukidhi majukumu yanayolikabili kwa mujibu wa Sheria mpya ya Mazingira, upungufu wa vitendea kazi, na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 inatekelezwa, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2006/2007, imeajiri watumishi 30 ili kujaza nafasi zilizokuwa wazi. Watumishi 25 wa kada tofauti wamepandishwa vyeo kwa kuzingatia miundo ya Utumishi wa Umma na Watumishi 17 walithibitishwa kazini.

Mheshimiwa Spika, katika kulinda, kudumisha na kuendeleza haki za wafanyakazi, Ofisi ya Makamu wa Rais iliandaa vikao viwili vya Baraza la wafanyakazi kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Kikao cha kwanza kilifanyika Arusha, Novemba, 2006 ambapo masuala kama vile mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, umuhimu wa Umoja wa Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya *(TUGHE*) na Baraza la Wafanyakazi, UKIMWI na masuala mbalimbali yanayohusu wafanyakazi pamoja na utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais, yalijadiliwa.

Kikao cha pili ambacho kilikuwa kikao maalumu kilifanyika katika ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam, Mei, 2007, kwa lengo la kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendeleza mapambano dhidi ya janga la UKIMWI. Kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (*TACAIDS*), Ofisi iliandaa jumla ya warsha tatu kwa watumishi wake zenye lengo la kuwakumbusha, kuwaelimisha na kuwashirikisha katika mapambano dhidi ya UKIMWI sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwaongezea watumishi uwezo wa kielimu na utendaji kazi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mwaka wa fedha 2006/2007, imeweza kugharimia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wapatao 43 ndani na nje ya nchi. Watumishi 30 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na 13 mafunzo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais wanakuwa na afya bora, wana ushirikiano mzuri na Wizara nyingine, pamoja na kuimarisha utendaji wao kazini, kwa mwaka 2006/2007 wamewezeshwa kushiriki katika mazoezi na mashindano ya michezo mbalimbali yaliyoandaliwa na Shirikisho la Michezo ya Wizara (SHIMIWI). Watumishi 56 walishiriki katika mashindano ya SHIMIWI yaliyofanyika mwezi Septemba 2006, Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kiwanja Na. 10 Mtaa wa Luthuli, Dar es Salaam unaendelea. Jengo halikuweza kukamilika mwezi Septemba, 2006 kama ilivyotarajiwa. Hii ilisababishwa na ongezeko la gharama, ujenzi wa jengo lingine, na mvua za masika. Shughuli ya ujenzi inatarajiwa kukamiika Januari, 2008.

Mheshimiwa Spika, matayarisho ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais huko Zanzibar yataanza mwaka wa fedha 2007/2008. Hatimiliki ya kiwanja imepatikana na tayari kazi ya michoro na utafiti wa udongo imekwishafanyika. Kiwanja kipo katika eneo la Tunguu, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mwaka wa fedha 2007/2008, itaendelea kuratibu, kusimamia na kushughulikia masuala yote ya Watumishi yahusuyo ajira, maslahi ya watumishi, nidhamu, mafunzo, kuendeleza utawala bora, mapambano dhidi ya UKIMWI na kuhakikisha kuwa watumishi wanapata vitendea kazi ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, katika masuala yahusuyo fedha, kwa mwaka wa fedha 2006/07 tumeweza kufanikisha kutoa taarifa za kifedha kutokana na mgao tuliopewa na Wizara ya Fedha kwa wakati. Taarifa hizo zimeonyesha mlingano halisi wa Bajeti na mwenendo wa matumizi kwa kila muhula kwa kutumia mfumo wa *"Integrated Financial Management System".*

Hesabu zetu ziliandaliwa katika viwango vya Kimataifa vya Uhasibu *(International Public Sector Accounting Standards).* Ofisi ya Makamu wa Rais, imepata Hati Safi ya Usahihi na Masuala ya Msisitizo kwa Mafungu yote mawili ambayo ni Fungu 26: Makamu wa Rais na Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais kwa taarifa ya fedha ya mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kimefanikiwa kufanya kazi za uchunguzi maalumu wa matumizi ya fedha na ununuzi wa vifaa vya Ofisi na kutoa ripoti kwa wakati. Aidha, kimeratibu, kimesimamia na kuongoza shughuli za ukaguzi wa ndani ya Ofisi kwa ujumla.

Katika kuleta ufanisi wa kazi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Kitengo kimekuwa kikitoa ushauri wa kitalaamu kuhusu kufuata na kutekeleza kanuni na misingi ya Kanuni za fedha za Umma za mwaka 2004 na Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2007/2008, Kitengo kitafuatilia na kuhakikisha kuwa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya Ofisi zitatumika kwa ajili ya malengo yaliyokusudiwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Sera na Mipango ni Idara mpya katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa mwaka wa fedha 2006/2007 majukumu ya Idara ya Sera na Mipango yamekuwa yakitekelezwa kupitia Kifungu cha Idara ya Utawala na Utumishi kwa kuwa haikuwa na kifungu. Aidha, Idara ilitekeleza majukumu yake ya kuratibu, kutathmini na kushauri juu sera, miongozo na mikakati mbalimbali ya Serikali ili kuboresha na kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Sera na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, imekusudia kuendelea kuratibu uandaaji na utekelezaji wa sera, mikakati, mipango na miradi mtambuka ya Kitaifa na Kimataifa hususan katika masuala ya Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, inatambua umuhimu wa kutoa habari, elimu na mawasiliano kwa umma katika kuunganisha, kuhabarisha na kuelimisha jamii juu ya masuala ya Muungano na Mazingira.

Kitengo cha Habarí katika mwaka wa fedha 2006/2007, kiliratibu vipindi vya Televisheni na Radio kwa upande wa Tanzania Zanzíbar na Tanzania Bara kuhusiana na mambo ya Muungano na Mazingira sawia. Kitengo kiliandaa vipeperushi, kuweka picha za kumbukumbu za matukio, kutoa taarifa mbalimbali kwenye vyombo vya habari kwa kushirikiana na viongozi, wataalamu na wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi katika kutekeleza majukumu yake. Pamoja na hayo, Kitengo kiliweza kuandaa mikakati ya Habari, Elimu na Mawasiliano kwa umma kuhusu masuala ya Mazingira na Muungano. Mikakati hii imeanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano kitaratibu, kitaelimisha na kitahabarisha umma kuhusu sheria, sera, kanuni, mikakati na mambo mengine yanayohusu masuala ya Muungano na Mazingira endelevu. Kitengo kitashirikiana na Wataalamu wa Idara, Vitengo na Wadau wa Ofisi ya Makamu wa Rais ili kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi na kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo napenda kuchukua nafasi hii, kwanza kabisa, kumshukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dk. Mohamed Shein, kwa uongozi wake thabiti na maelekezo yake yaliyowezesha Ofisi yetu kutekeleza vizuri majukumu yake. Namshukuru Mheshimiwa Samwel Sitta, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Anna Makinda, Naibu Spika kwa kuongoza Bunge hili Tukufu. Napenda pia kumshukuru na kumkaribisha Bi. Ruth H. Mollel, ambaye ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais. Nawashukuru vilevile Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Miradi na Wafanyakazi wote wa Ofisi kwa kujituma na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza

Bwana Sazi Salula aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu Wizara ya Sheria na Katiba. Pia napenda kumshukuru Bwana Abubakar Rajabu, aliyekuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais ambaye amestaafu, kwa mchango wake mkubwa katika utumishi wa umma. Namtakia kila la heri. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa Wahisani mbalimbali ambao wameendelea kuisaidia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kugharamia miradi mbalimbali katika kuratibu utekelezaji wa Mikakati ya Muungano, Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira na kupambana na ugonjwa wa UKIMWI.

Wahisani hao ni pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia maendeleo *(UNDP*), Shirika la Maendeleo la Marekani (*USAID)*, Shirika la Umoja wa Maifa la Mazingira *(UNEP*), Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*GEF)*, *International Development Agency (IDA), Danish International Development Agency (DANIDA), Food and Agriculture Organization (FAO*), Asasi zisizo za Kiserikali (AZISE), Vyombo vya Habari, Wananchi na Wadau wengine kwa kushirikiana vyema na Ofisi hii katika kutekeleza majukumu yake. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Prof. Mark James Mwandosya, anawashukuru kwa dhati Wananchi wa Rungwe Mashariki, kwa imani kubwa na ushirikiano waliompa katika kutekeleza majukumu yake katika kipindi chote cha Ubunge wake. Mheshimiwa, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), anawashukuru Wananchi wa Jimbo la Kwahani, Zanzibar, kwa imani na ushirikiano mkubwa wanaoendelea kumpa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 26: Makamu wa Rais - katika mwaka wa fedha 2007/2008, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya *Tshs*. 2,465,419,000/= kwa ajili ya kugharamia Matumizi yakawaidaya Makamu wa Rais. Kati ya fedha hizo,*Tshs*. 466,263,000/= kwa ajili ya mishahara ya watumishi na *Tshs.* 1, 999, 156,000/= kwa ajili ya matumizi mengine.Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais - katika mwaka wa fedha 2007/2008, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya matumizi ya jumla ya Tshs. 35,490,349,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Tshs. 681,982,000/= ni mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Tshs. 633, 502,292/= ni ruzuku ya mishahara ya Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*). *Tshs*. 27,338,623,000/= ni kwa ajili ya mgawo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, *Tshs.* 5,782,287,190/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengine ya Ofisi ya Makamu wa Rais, na Tshs. 1,053,954,518/= ni ruzuku ya matumizi mengineyo ya *NEMC.* Kiasi cha *Tshs*. 13, 611, 700,000/= kinaombwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha hizo za ndani ni Tshs. 3,818,500,000/= na fedha za nje ni Tshs. 9,793,200,000/=. Nasahihishwa hapa kwamba matumizi mengine ni shilingi 1,999,156,000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, sasa tutamsikiliza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira au Mwakilishi wake.

Anakuja Mheshimiwa Anastazia James Wambura kwa niaba ya Kamati, natumaini Mheshimiwa Wambura Baba bado yupo kule juu.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Bado yupo! *(Makofi).*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA (k.n.y. MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1) ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2004), nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 26 - Makamu wa Rais na Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa salamu za rambirambi kwa ndugu, jamaa na familia ya Mzee Chifupa kutokana na kifo cha kijana wao mpendwa, aliyekuwa Mbunge wa CCM kupitia tiketi ya vijana, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, kilichotokea tarehe 26 Juni 2007. Msiba wa marehemu Amina Chifupa umepokelewa kwa masikitiko makubwa kwa Watanzania wengi kila pembe ya nchi. Katika uhai wake, marehemu alionyesha umakini mkubwa wa kazi yake kama Mbunge. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina!

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira ambao ndio waliochambua Bajeti hii, nao ni: Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Bahati A. Abeid, Mheshimiwa Halima Mamuya, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Riziki O. Juma, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Mheshimiwa Emanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Abdukarim E. Shah, Mheshimiwa Salim Khamis Salim, Mheshimiwa Mohamed R. Soud, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Juma S. Nh'unga, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa. Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, na Mheshimiwa Anastazia Wambura.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata maelezo ya kina toka kwa Mheshimiwa Waziri, ambaye alieleza kwamba Makadirio ya Matumizi ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2007/2008 yamefuata mfumo wa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na yamezingatia Dira, Mwelekeo na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Utekelezaji wa Ahadi za

Serikali Bungeni na Maagizo ya Kamati za Bunge. Aidha, katika maelezo yake alielezea kuhusu mafanikio na matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji, kazi zitakazotekelezwa na maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha uliopita Kamati yangu ilitoa ushauri na maagizo katika maeneo mbalimbali hasa yanayohusu Mazingira. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kiasi kikubwa imeyafanyia kazi maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika imeshauri na kutoa maagizo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais ilitengewa jumla ya sh. 32,734,990,000/=. Hata hivyo, Ofisi hii ilichangia kiasi cha sh. 2,300,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya dharura ya Serikali. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2007 Ofisi hiyo ilikuwa imepewa kiasi cha sh. 29,857,502,776.60/= ambayo ni asilimia 91 ya fedha iliyotengwa.

Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 3,003,000/= kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia Aprili, 2007 kiasi cha shilingi 4,627,977/= kimekusanywa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

(i) Kuratibu shughuli za utekelezaji wa Sera ya Mazingira. Baadhi ya shughuli hizo ni:- Taarifa ya Utekelezaji wa ahadi za Serikali Bungeni imeandaliwa; Ufuatiliaji wa Kampeni ya Taifa ya upandaji Miti ilifanyika na taarifa imeandaliwa; Taarifa kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kuhusu Mazingira iliandaliwa na ushauri ulitolewa kwa mashirika yasiyo ya Kiserikali kuhusu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira.

(ii) Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira imekamilisha programu ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, na sasa ipo tayari kwa utekelezaji tu, Bajeti ya programu hii ni kiasi cha dola milioni 40.7 kwa kipindi cha miaka mitano. Mfadhili (Serikali ya *Denmark)* amekubali kuchangia kiasi cha Dola za Marekani milioni 6.14.

(iii) Maandalizi ya Kanuni kuhusu Kemikali zinazoharibu Ukanda wa Ozoni (*Ozone Depleting Substance*); viwango vya ubora wa mazingira (*Environmental Quality Standards*); ada na tozo zilizoainishwa kwenye Sheria ya Mazingira (*Fees and Charge Regulations*); na Tathmini ya Mazingira kimkakati (*Stretagic Environmental Assessment* - SEA) zimeanza: Kanuni za usimamizi wa mifuko laini ya plastiki na viroba vya kufungia maji, maji ya matunda na maziwa ziliandaliwa na kupitishwa; Uandaaji wa Kanuni na miongozo kuhusu wakaguzi wa Mazingira umeanza.

(iv) Mkakati wa kuhifadhi mazingira ya Ardhi na vyanzo vya maji nchini uliendelea kutekelezwa. Uperembaji wa utekelezaji wa mkakati umefanyika katika Mikoa 9, hadi kufikia mwezi Februari, 2007 Mikoa iliyohusika ni Mbeya, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, Lindi, Tabora na Kagera: Idara ya Mazingira iliandaa Taarifa na Hati za utekelezaji wa Mkakati ziliwasilishwa kwenye Kamati ya Mazingira ya Baraza la

Mawaziri; Aidha, madodoso ya aina mbalimbali yaliandaliwa kwa ajili ya zoezi la kuperemba utekelezaji wa mkakati kulingana na majukumu ya wadau.

(v) Rasimu ya hatua za mkakati wa kuhifadhi Mazingira ya Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mabwawa na Mito imeandaliwa na hati ya rasimu ya mkakati huo iliandaliwa na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Mazingira ya Baraza la Mawaziri.

(vi) Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ikishirikiana na nchi jirani, zimeandaa programu ya hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika. Kikao cha kwanza cha Mawaziri husika kimefanyika pamoja na kikao cha Wataalam wa Nchi husika. Aidha, mchakato wa ajira kwa Wafanyakazi wa *Lake Tanganyika Authority* (LTA) umekamilika.

(vii) Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira imeratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira ambayo Tanzania ni Mwanachama yakiwemo:- Maadhimisho ya Siku ya Ozoni Duniani yaliyofanyika Dar es Salaam, Tanzania (16 Septemba, 2006). Wadau mbalimbali kutoka Idara na Taasisi za Serikali na Mashirika yasiyo ya Kiserikali walishiriki; Mradi wa Kujenga uwezo wa Taasisi katika utekelezaji wa Mkataba wa *Montreal* kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 ulioandaliwa kwa ajili ya ufadhili na kuwasilishwa katika Sekretarieti; Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa kuunda Kituo cha Kanda cha Afrika cha Usimamizi wa Taka Sumu na nyinginezo (Mkataba wa *Basel*) liliandaliwa na kupitishwa na Bunge mwezi Februari, 2007; maandalizi ya Ripoti ya Pili ya Utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabia ya Nchi yameanza, na uchambuzi wa kina wa athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Sekta za Kilimo, Afya, na Maji umefanyika kwa ufadhili wa *DANIDA*, na ripoti ya uchambuzi huu inakamilishwa: katika kutekeleza Itifaki ya *KYOTO*, mradi mmoja kuhusu uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi taka za dampo la Mtoni-Dar es Salaam unasubiri kuidhinishwa. Mradi huu unategemewa kuzalisha kiasi cha Umeme upatao *Megawatt* mbili pointi tano (2.5Mw) kwa mwaka na kuingizwa katika gridi ya Taifa.

Mengine yaliyokuwemo katika utekelezaji wa Mkataba huo ni: Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*GEF*) umeendelea kufadhili miradi mbalimbali inayohusu utunzaji wa mazingira. Kuanzia Julai 2006, jumla ya miradi 52 ilipokelewa ikapitiwa na kupitishwa kwenda *GEF* kwa ufadhili; Ripoti ya Hali ya Mazingira Nchini kwa mwaka 2006 imeandaliwa na kuwasilishwa HAZINA kukidhi mahitaji ya Wafadhili chini ya (*Performance Assessment Frame Work* – PAF); Mkakati wa Usimamizi wa Taka nchini umeanzishwa na kikao cha wataalam toka Sekta mbalimbali kilifanyika. Sekta zilizohusika ni Kilimo, Maji, Viwanda, Elimu ya Juu, Nishati, Madini, Miundombinu na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini lilifanya baadhi ya mambo yafuatayo:-

(a) Katika kuendeleza mipango ya mazingira na utafiti Baraza limefanya utafiti wa awali wa kuainisha maeneo oevu yaliyoathirika (*Degraded wetlands)* katika ukanda wa Kusini Magharibi (Rukwa) na ukanda wa Magharibi (Kagera na Kigoma).

(b) Katika kudhibiti na kuzuia uchafuzi wa mazingira:- Baraza lilikagua viwanda 18 katika Miji ya Dar es Salaam, Morogoro, Kibaha, Arusha, Moshi, Bukoba, Tanga na Mwanza ili kubaini hali halisi ya uchafuzi wa mazingira unaotokana na viwanda hivyo na kutoa ushauri jinsi ya kuondokana na uchafuzi huo. Pia Baraza liliandaa mwongozo wa Kitaifa wa uchunguzi wa Mazingira (*National Investigation Manual and National Prosecution Procedure)* ili kuweza kufanya ukaguzi unaostahili na kuchukua hatua za kisheria; Sheria ndogo ya kupiga marufuku mifuko ya plastiki na ile ya maji, maji ya matunda na maziwa ilitangazwa na Mheshimiwa Waziri kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 , Kifungu cha 239(4) na kuanza kutumika tarehe 01 Oktoba, 2006.

(c) Katika kuhakikisha shughuli za maendeleo haziathiri mazingira, Baraza limesajili na kuhakiki miradi 100, kutoka katika maeneo ya madini, hoteli za kitalii, barabara na viwanda mbalimbali. Miradi 15 ilipewa hati ya tathmini ya athari ya mazingira (EIA) na Mheshimiwa Waziri.

(d) Katika kuhamasisha umma na kusambaza taarifa za mazingira Baraza limetoa elimu kwa wadau kwa njia ya vyombo vya Habari, Warsha, Makala, mtandao wa tovuti, makongamano na mikutano.

(e) Kwa kushirikiana na Wafadhili, Baraza limeendelea kutekeleza shughuli za miradi mbalimbali ikiwemo: Mradi wa *MACEMP;* Mradi wa utafiti na udhibiti wa uchafu wa bonde la Mto Msimbazi; Kusimamia utekelezaji wa mradi wa Kihansi.

Mheshimiwa Spika, kituo cha uzalishaji bora na hifadhi ya mazingira kimeweza kutekeleza baadhi ya shughuli zifuatazo:- kufanya tathmini ya uzalishaji bora na matumizi bora ya nishati (*Cleaner Product Assessment)* katika viwanda vinne vilivyoko katika Miji ya Dar es Salaam (1), Moshi (1) Morogoro (2); kutoa mafunzo, kutayarisha Semina, na kuendesha warsha kwa wadau mbalimbali katika masuala yanayohusu uzalishaji bora na hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo Kamati iliainisha matatizo mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Upungufu wa fedha katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Makamu wa Rais, (Idara ya Mazingira, *NEMC,* na Kituo cha uzalishaji bora na hifadhi ya Mazingira *(CPCT*).

(ii) Uhaba wa Watumishi, vitendea kazi na kutokuwa na Ofisi moja kwa wafanyakazi wote.

(iii) Baadhi ya Idara na vitengo havina kifungu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yanayowakabili hivyo vinategemea kifungu cha Idara ya Utawala na Utumishi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendeleza utawala bora, kuhakikisha taratibu zote za Utawala na Utumishi zinafuatwa kulingana na Sheria, miongozo na Kanuni za Utumishi wa Umma.

(ii) Kuwaendeleza watumishi kitaaluma na mapambano dhidhi ya Ukimwi.

(iii) Idara ya Mazingira itaendelea kutekeleza mkakati wa kuhifadhi Mazingira ya Ardhi, vyanzo vya maji, Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa na Mito.

(iv) Baraza litaendelea kutoa ushauri kwa Serikali na wadau wengine katika kuhifadhi mazingira na kutekeleza majukumu yake kwa Mujibu wa Sheria Mama ya Mazingira. Pia litashiriki katika michakato ya Kitaifa na Kimataifa inayohusu mazingira, kuandaa kanuni, viwango na miongozo muhimu ya kutekeleza Sheria ya Mazingira hasa katika masuala ya utafiti, usambazaji taaarifa na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira.

(v) Kituo cha uzalishaji bora na hifadhi ya mazingira kitandelea kutoa huduma za kitaalamu hasa katika masuala ya uzalishaji bora na matumizi endelevu ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu iliunga mkono Tamko la Serikali la tarehe 1 Aprili, 2006 kuhusu hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji nchini:

(a) Kamati ilishauri kuwa Serikali itafute maeneo kwa ajili ya Wafugaji wanaohamishwa kutoka kwenye maeneo ambayo ni vyanzo vya maji.

(b) Hata hivyo, Kamati yangu imebaini kwamba zoezi zima la kuwahamisha Wafugaji katika eneo la Ihefu halikufanyiwa utafiti wa kutosha hasa kule ambako mifugo ilikohamishiwa.

(c) Zoezi zima lilileta athari kwa mazingira, familia na kuleta umaskini kwa wafugaji.

(d) Vilevile yapo malalamiko kwamba maeneo mengi ya Kusini yana Ndorobo na majani yasiyofaa kwa malisho ya mifugo. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti wa kina kwenye maeneo husika kwa manufaa ya kuboresha ufugaji katika Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka jana 2006/2007, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 9.4. kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati wa kutunza mazingira nchini. Hata hivyo, kasi ya utekelezaji wa Mkakati huo ilikuwa ndogo kutokana na fedha kuchelewa kufika kwenye sekta husika. Fedha ziliwekwa kwenye Matumizi Mengine *(OC*) na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kupunguzwa. Hivyo basi Kamati yangu inaishauri Serikali kwamba fedha za Bajeti 2007/2008 zilizotengwa kwa ajili ya

Mkakati zitumike kama ilivyokusudiwa bila kupunguzwa. Aidha, kasi ya uperembaji wa mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji iongezeke.

Mheshimiwa Spika, tarehe 3 Aprili, 2007 Kamati yangu ilifanya ziara katika baadhi ya Viwanda vinavyozalisha mifuko ya plastiki vilivyopo jijini Dar es Salaam, kujionea utekelezaji wa agizo la Serikali la kupiga marufuku uingizaji na utengenezaji wa mifuko ya Plastiki yenye unene chini ya *Microns* 30:

(a) Kamati ilibaini kwamba bado kuna ukiukwaji wa agizo la Serikali, kwani bado mifuko ya aina hii inaonekana Nchini. Aidha , mazingira ya baadhi ya viwanda ni machafu na hayaridhishi. Kamati yangu inaishauri Serikali kuchukua hatua kali kwa wenye viwanda pindi wanapobainika kukiuka agizo hili. Pia wenye viwanda wajitahidi kuweka mazingira ya usafi, ndani na nje ya viwanda vyao.

(b) Baraza liongeze kasi katika ukaguzi wa viwanda Nchini.

(c) Kamati yangu inashukuru Serikali kwa kuongeza ushuru wa bidhaa kwa mifuko ya *plastic* kutoka asilimia 15 hadi 120 ili kupunguza matumizi ya mifuko hiyo na kuzuia uchafuzi wa mazingira. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutenga kiasi cha kutosha cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati wa kutunza mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inalipongeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini kwa kusimamia na kuhakikisha kuwa mazingira yanatunzwa ipasavyo. Hata hivyo, Kamati inalishauri Baraza kufungua Ofisi za Kanda ili kuongeza ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mtaa wa Lithuli) na kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais huko Tunguu, Zanzibar haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2007/2008 ya Ofisi ya Makamu wa Rais, yameandaliwa kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yanayotarajiwa kufikiwa katika utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Baada ya uchambuzi wa kina Kamati inakubaliana na Makadirio ya Bajeti ya Makamu wa Rais, Fungu 26, jumla ya shilingi 2,465,419,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya punguzo la 17.3 % kutoka Fungu 31, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeidhinishiwa kiasi cha shilingi 35,490,349,000/= kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na Mishahara.

Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi 1,315,484,292/= ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi na shilingi 6,836,241,708/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Ofisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepata mgawo wa kiasi cha shilingi 27,338,623,000/=. Hivyo ,Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Fedha zinazoombwa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Katibu Mkuu wake na Watumishi wote wa Ofisi hii na Taasisi ama Mashirika yaliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Tumepata elimu wakati wa Semina mbalimbali na tulipotembelea shughuli zao. Kamati inawashukuru sana na kuwatakiwa mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu kwa ushauri na busara zao zilizomwezesha Mwenyekiti kuiongoza Kamati hii, michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka na Makatibu wa Kamati hii , Ndugu Lawrence Makigi na Michael Kadebe kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja hii.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO (k.n.y. MHE. GEORGE MALIMA LUBELEJE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA ):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu taarifa ya Utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano ya mwaka 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kan. Na. 81(1), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, baada ya kuipatia Kamati yangu kazi ya kujadili Makadirio ya Ofisi hii, Kamati iliikamilisha kazi hii katika kikao chake kilichofanyika ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam, tarehe 8 Juni, 2007 kwa kupokea maelezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008 na Utekelezaji wa majukumu yaliyopo katika Ofisi hiyo kwa mwaka wa Fedha 2006/2007. Maelezo hayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Daktari Hussein Mwinyi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, ilitengewa jumla ya shilingi 22,344,213,000.00, kiasi hicho kikijumuisha gawio la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar la asilimia 4.5. Hata hivyo, kiasi hicho kimekuwa kikiongezeka kulingana na misaada isiyo na masharti na faida inayopata Benki Kuu ya Tanzania. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2007, Ofisi ya Makamu

wa Rais, Muungano ilikuwa imepokea sh. 22,543,955,205.66 na kutumia jumla ya sh 23,497,718,962.62 ziilizoongezeka kutokana na Hazina kuongeza kiasi cha gawio la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika kipindi hicho kiasi cha sh. 369,109,412.10 kilipunguzwa kukabiliana na dharura za Kitaifa hususan tatizo la njaa lililolikumba Taifa na ukarabati wa miundombinu kutokana na uharibifu uliofanywa na mvua.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mgao wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, fedha hizo zilitumika kwa ajili ya kukusanya taarifa mbalimbali zinazohusiana na masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano kutoka kwa wadau wa Muungano; kuandaa nakala elfu kumi za vipeperushi na kuvisambaza kwa wadau mbalimbali wa Muungano, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar; kukusanya, kuchambua na kuingiza katika mfumo wa elektroniki taarifa mbalimbali za Muungano; kuandaa na kushiriki vikao vya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi, Novemba, 2006; kuandaa vikao vitano vya Waheshimiwa Mawaziri wa sekta za Muungano SMT na Mheshimiwa Waziri Mkuu na vikao vitatu vya Makatibu Wakuu wa sekta za Muungano na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki pia Kamati ilielezwa juu ya mafanikio na matatizo mbalimbali yaliyojitokeza. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni utekelezaji wa masuala yanayohusu Muungano na yasiyo ya Muungano. Matatizo yaliyokuwepo ni pamoja na mazingira duni ya kufanyia kazi ya Ofisi binafsi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais na makazi yake, uhaba wa fedha, upungufu wa watumishi, ofisi na vitendea kazi duni ambavyo viliathiri utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita Kamati iliishauri Serikali ya Muungano wa Tanzania kuweka wazi utaratibu wa mgawo wa fedha za msamaha wa madeni (*Bilateral and Multilateral Debt Relief Initiative*). Pamoja na mambo mengine, Serikali ilieleza kwamba Tanzania imeendelea kufaidika na msamaha wa madeni kutoka kwa wafadhili na kwamba Benki Kuu ya Tanzania ndiyo inawajibika kulipa kwa Serikali zote mbili fedha zinazotokana na msamaha wa madeni. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kupata mgao wa asilimia 4.5. Pili, Kamati iliishauri Serikali kuona uwezekano kwa Tume ya Haki za Binadamu kufanya kazi Zanzibar. Kamati ilijulishwa kuwa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu ya Mwaka 2001 imekwisharekebishwa na tayari inatumika pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Serikali zilizotolewa Bungeni wakati wa vikao vya Bunge la Bajeti 2006/07. Ahadi hizo zilihusu, pamoja na mengineyo, kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais lililopo Mtaa wa Lithuli *Plot No.*10 ifikapo Septemba, 2006; kuanza kwa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais huko Tunguu-Zanzibar; kuanzisha mfumo wa mawasiliano ambao utatumika katika tafiti mbalimbali zitakazohusu mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali zote mbili kwa lengo la kuondoa matatizo mbalimbali ya Muungano yaliyopo na yatakayojitokeza.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2007/2008, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, inakusudia kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kumwezesha

Mheshimiwa Makamu wa Rais kutekeleza kazi zake kwa ufanisi; kuendelea kuratibu masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano katika vikao mbalimbali vikiwemo vya kimataifa; kuratibu, kuandaa na kushiriki katika vikao kati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi angalau mara tatu kwa mwaka; kufanya tafiti kwa mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano kwa lengo la kuimarisha Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, inaomba jumla ya shilingi 28,024,804,100/=. Kati ya fedha hizo sh. 27,860,000/= kwa ajili ya mishahara, sh. 658,321,100.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na sh. 27,338,623,000/= gawio la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa makazi ya Ofisi ya Makamu wa Rais hayalingani na hadhi yake, Kamati inashauri kuwa Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga makazi hayo Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu, Kamati yangu ilifanya ziara Zanzibar, Januari, 2007 kukagua miradi mbalimbali ya Muungano na kuguswa sana na mazingira duni ya kufanyia kazi ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Pili, kwa kuwa wapo baadhi ya wananchi wamekuwa na mtazamo tofauti kuhusu nafasi ya Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kamati inashauri kuwa elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi wa pande zote kuwaeleza kwa kina juu ya nafasi ya Zanzibar kuhusu Jumuiya hiyo mbali ya kwamba sasa hivi kuna Tume ya Taifa ya kukusanya maoni kuhusu suala hilo.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii fupi imezungumzia kiasi cha fedha kilichotengwa na utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, kwa mwaka wa Fedha wa 2006/2007. Taarifa hii pia imegusia mafanikio na matatizo yaliyojitokeza katika kipindi hicho. Aidha, imeelezea kwa kifupi utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Rais ambao uligusa maeneo makuu mawili: Mgao wa Fedha kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na suala la Tume ha Haki za Binadamu kufanya kazi Zanzibar. Zaidi ya hayo, imetoa taarifa ya ahadi zilizotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi hicho na utekelezaji wake. Mwisho, Taarifa imezungumzia kiasi cha fedha kinachoombwa na shughuli zilizopangwa kufanyika na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano), kwa mwaka wa Fedha 2007/2008 na maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kwa kuwasilisha Taarifa ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008. Vilevile namshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Vitengo, kwa kushirikiana vema na Kamati wakati wote tulipochambua Makadirio ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri waliyofanya na kukamilisha Taarifa ya Kamati mapema ilivyowezekana. Naomba niwatambue kama ifuatavyo: Mheshimiwa George Malima Lubeleje,Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Shoka Kh. Juma, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim Yussuf

Mohammed, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, na Mheshimiwa Dk. Wilbrod P. Slaa.

Pia nawashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Charles Mloka, Ernest Zulu na Emanuel Mpanda, kwa kuratibu vikao vya Kamati na kutayarisha Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kukubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. Makofi)

**MHE. RIZIKI O. JUMA – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kusoma naomba niseme kwamba taarifa yangu hii ambayo naitoa naomba inukuliwe kama ilivyo katika makabrasha.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa Maoni ya Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, kama inavyoelekezwa na Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2004, Ibara ya 43 (5) (b) (c) na 81 (1).

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa pole kwako wewe binafsi, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote na familia ya Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Kwa kweli ni msiba mzito uliotukumba lakini kazi ya Mungu haina makosa. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ailaze pema peponi roho ya marehemu na awape subira wafiwa wote.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kutoa mtazamo wa Kambi hii, shukrani zangu za dhati kwa uongozi mzima wa chama changu, Chama Cha Wananchi (*The Civic United Front* – CUF) pia kwa viongozi wangu wa Kambi chini ya Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa kwa ushirikiano wao wanaonipatia na imani yao kwangu.

Aidha, nampongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi, kwa kuendelea kuitumikia vyema nafasi aliyokabidhiwa na Watanzania kupitia uteuzi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la fahari kwamba wananchi wa Tanzania tumesherehekea miaka 43 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar hivi karibuni. Tunajivunia Muungano wetu kama mfano pekee wa Muungano uliodumu Barani Afrika. (*Makofi*)

Hata hivyo, wakati tukisherehekea, bado tumegubikwa na malalamiko ya kasoro kati ya pande hizi mbili za Muungano wetu. Hili linatokana na kero nyingi kujitokeza, huku utatuzi wake ukienda mrama na kuwepo kwa mashaka makubwa kutoka kila upande.

Mheshimiwa Spika, wananachi na viongozi mbalimbali waliozungumzia Muungano wakati wa sherehe hizo, walisema wakati umefika kwa kero zake kutatatuliwa kwa kuwashirikisha wananchi wenyewe na sio kwa viongozi kukaa peke yao kwa kujifungia na kujiamulia kama vile masuala haya ni yao wao tu.

Mheshimiwa Spika, kero za Muungano zinazopigiwa kelele na wananchi ni nyingi na zinagusa maeneo tofauti kulingana na upande wananchi hao wanakotoka. Mathalan, upande wa Tanzania Bara, wananchi wengi wanaendelea kulalamikia

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Rizik, naomba ukae kwanza. Taarifa unayoisoma haiko mezani hapa kwa Spika na ni kiyume cha utaratibu. Kwa hiyo, sijui imekuwaje! Leo naona Mheshimiwa Chacha Wangwe ameshika jukumu la kuongoza Upinzani, sasa tusubiri kidogo tutatue hili kwa sababu...!

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, itakuja sasa hivi.

**SPIKA:** Sasa mmezibadili maana ilitakiwa ziwe *tabled*. Haipo hapa sijui upande wa Serikali mna taarifa yoyote? Kiongozi wa Shughuli Dr. Ngasongwa hana! Kuna kasoro ilitokea. Hebu nishauriane na Katibu, ni kinyume kabisa huwezi kuendelea kusoma kitu ambacho hata Spika hana habari nacho.

Mheshimiwa Riziki endelea! Inaelekea ni makosa ya Ofisi yangu kwamba nakala za kutosha zilikuwa hazijachapishwa. Kwa hiyo, si kosa lako. Endelea wakati huo zitakuwa zinaletwa na muda wako tumeuokoa usidhani umepunjwa muda..

**MHE. RIZIK O. JUMA – MSEMAJI WA UPINZANI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAMBO YA MUUNGANO:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kero za Muungano zinazopigiwa kelele na wananchi ni nyingi na zinagusa maeneo tofauti kulingana na wananchi hao wanakotoka, mathalani upande wa Tanzania Bara wananchi wengi wanaendelea kulalamikia uwakilishi mkubwa unaopewa Zanzibar ambao hauna uwiano na idadi ya watu wake na ukubwa wa visiwa hivyo na pia wanalalamikia Wazanzibari kushikilia nafasi upande wa Tanzania Bara kwa taasisi ambazo hazihusu mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar, malalamiko ni mengi hasa katika uwanja wa uchumi na mgawanyo wa rasilimali kiasi kwamba wananchi walio wengi wanahisi kuwa Muungano huu umekuwa kikwazo kwa ustawi na maisha ya wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba. Wananchi wengi wanapigia kelele suala la vikwazo vya biashara kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, ambavyo vimekuwa vikidumaza uchumi wa Zanzibar pamoja na maisha ya wananchi wake. Haya yalikuwa ndio maoni ya wananchi waliyoyatoa katika vipindi vya televisheni na redio katika shamra shamra za kuadhimisha miaka 43 ya Muungano. Haya hayapaswi kupuuzwa ikiwa kweli tunakusudia kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, chombo cha kusimamia na kukusanya kodi ni *TRA* kwa pande zote za Muungano lakini wafanyabiashara wa Zanzibar wanapoingiza bidhaa Tanzania Bara wanachukuliwa kama vile wanatoka nchi za nje. Pamoja na ahadi nyingi za kushughulikia kero za usaliji wa magari, hadi leo gari za ZNZ zinalipishwa US$25 kwa mwezi kama ni gari inayotoka nchi za nje. Hivi ni kwa nini Serikali inaruhusu hali hii indelee? Je, kuna dhamira ya kweli ya kutatua kero za Muungano?

Mheshimiwa Spika, kero nyingine ambayo imeleta kitendawili kikubwa katika Muungano wetu ni suala la rasilimali za nchi kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar, ambapo suala la nishati za mafuta, gesi na madini limekuwa tatizo kubwa. Kwa mfano, hadi sasa ni mafuta na gesi tu ndiyo yaliyoorodheshwa katika masuala ya Muungano na hivyo kuja kunufaisha uendeshaji wa shughuli za Muungano, lakini madini na maliasili nyingine hazihusiki na masuala ya Muungano. Hali hii imewafanya wananchi wengi kulalamika kwamba sio haki suala la mafuta kuingizwa katika mambo ya Muungano huku madini kama vile dhahabu, almasi, *Tanzanite* na mengine yakibaki kutokuwa ya Muungano na kunufaisha Tanzania Bara pekee. Zaidi ya hayo, gesi ambayo inadaiwa kuwa ni ya Muungano imeanza kuvunwa miaka kadhaa nyuma, lakini hakuna hata shilingi moja iliyovuka bahari kwenda Zanzibar kutokana na nishati hiyo ya Muungano. Zanzibar inaambulia asilimia 4.5 ya misaada kana kwamba haichagii katika mapato ya Muungano. Ili kuondoa tatizo hili ushauri uliotolewa na Waziri Kivuli wa Fedha wa kutumia asilimia 15 ya mapato iwe mgao wa Zanzibar utekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kuna suala jingine la ZFA kuwa mwanachama wa FIFA. Kwa chama hicho cha michezo kuwa mwanachama wa FIFA ni faida kwa Taifa na ni kupunguza utegemezi wa ZFA kwa TFF. Kama sio siasa na ubinafsi usio na msingi, ule mgao ambao FIFA inatoa kwa nchi mwanachama ili kuendeleza soka, basi kwa maana pana na rahisi kwetu tungekuwa tunapata mara mbili, yaani ZFA na TFF. Hivyo basi tungekuwa na uwezo mzuri wa kuandaa timu zetu katika ushiriki wa kimataifa.Tunajinyima fursa wenyewe wakati *UK, Scotland* inaingia katika mashindano ya Kimataifa kama Taifa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kambi ya Upinzani kwamba Muungano wetu una kasoro za msingi na za kimaumbile ambazo sasa zimepewa jina la kero. Kasoro kubwa ni kule kuendelea kudharauliwa na kuvunjwa kwa Mkataba wa Muungano *(Articles of Union*) ambao kisheria ulipaswa kuwa ndiyo msingi wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar. Hivi sasa vipengele kadhaa vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano vinapingana na masharti ya Mkataba huo. Mfano ulio wazi ni kule kumwondolea Rais wa Zanzibar wadhifa wake wa Makamu wa Rais, jambo ambalo lilikuwa ni sehemu muhimu ya Makubaliano ya Muungano, kufutwa kwa "*The Exchange Control Decree of Zanzibar"* kwa kutumia Sheria Na.22 ya 1965 ambayo Bunge halikuwa na madaraka ya kufuta sheria hiyo (*Sec*.24) na kadhalika. Kasoro hizo kutatuliwa kwake ni lazima Katiba yetu ambayo ndio dira na mwongozo wetu, kuandikwa upya kwa kuwashirikisha Watanzania wote wa Tanzania Bara na wa Zanzibar. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tunazungumzia kuimarisha Muungano wetu lakini tafsiri inayotolewa na Serikali za CCM katika suala hili inapotosha dhamira yenyewe. Ili kulielewa hili, naomba ninukuu kauli alizozitoa Rais Mstaafu wa Zanzibar, Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi, katika kitabu chake, *The Partner-ship*. Naomba kunukuu: "Kosa moja ambalo linaendelea kufanywa ni lile la kudhani kwamba kuimarisha Muungano kuna maana moja ya kuhaulisha shughuli zisizokuwa za Muungano (kwa upande wa Zanzibar) ziwe za Muungano na kwamba Chama na Serikali ya Muungano wanaweza kufanya hivyo bila ya kuzingatia Katiba wala hisia au matakwa ya Zanzibar. Dhana hizo ama ni za kupotosha kusudi kwa sababu wanazozielewa wenyewe wanaofanya hivyo, au ni kutoelewa Katiba. Vyovyote vile ilivyo ni mashaka. "Kisheria shughuli yoyote isiyo ya Muungano haiwezi kufanywa iwe ya Muungano bila ya ridhaa ya Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Tanzania Bara au na Serikali ya Muungano kwa niaba ya Tanzania Bara. Mpango wa Serikali ya Muungano kuwakilisha pia Tanzania Bara umeleta fadhaa na wasiwasi wa kutosha katika miaka kadhaa, hasa ya hivi karibuni. "Muungano au umoja hauwezi kuimarika kwa upande mmoja kutwaa madaraka ambayo ni ya pande mbili za umoja huo. Ikiwa wote tutatekeleza wajibu wetu, haki haitakuwa mbali kuonekana, na kila upande utakuwa na utaridhika na haki yake." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, huu ni ushahidi wa wazi kuwa pamoja na viongozi wakuu wa Muungano, kama alivyokuwa Mzee Jumbe, kuupenda Muungano lakini waliona kasoro za wazi za utekelezaji wa Muungano wenyewe zaidi ya miaka 20 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, katika Awamu ya Tatu na ya Nne ya Serikali ya Zanzibar, mbali ya mambo ya Muungano kuongezeka, juhudi za kusawazisha kasoro hizo ziliendelea kwa vikao vya pamoja baina ya Serikali ya Muungano na ya Zanzibar. Vikao hivi vikiongozwa na Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi.

Mheshimiwa Spika, katika Awamu ya Tano ya Serikali ya Zanzibar, Serikali ilichukua hatua nyingi zaidi kuliko awamu yoyote kushughulikia kasoro za Muungano. Rais wa wakati huo wa Zanzibar, Dk. Salmin Amour, hakuwa akificha hisia zake za kutoridhishwa na utekelezaji na msimamo wake ulikuwa wazi, kudai marekebisho katika maeneo kadhaa hasa katika masuala ya uchumi, kupunguzwa mambo ya Muungano yasiyo ya lazima na suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, pia na Awamu ya Sita ya Serikali ya Zanzibar inajulikana wazi kwa msimamo wake juu ya suala la uchimbaji wa mafuta; msimamo ambao iliurithi kutoka Awamu ya Tano na ambao unaungwa mkono na Wazanzibari walio wengi. Mbali ya suala hilo, iliunda Kamati ya Wataalamu katika siku za mwanzo za kuingia madarakani, ambayo ilichambua kasoro za Muungano na kupendekeza mambo ya kupunguzwa au kuongezwa na utaratibu wa kuendesha masuala ya Muungano kisera, kiutawala na katika kutunga sheria za Muungano.

Mheshimiwa Spika, pendekezo moja mahsusi la Kamati hiyo, ambalo linaungwa mkono pia na Kambi ya Upinzani ni kwamba Bunge la Tanzania liwe na sehemu mbili

(2) yaani "*Lower House*" itakayoshughulikia mambo ya Tanzania Bara na ambapo wabunge wa Zanzibar hawatoshiriki na "*Upper House*" ambayo itashughulikia mambo ya Muungano tu na itakuwa na uwakilishi sawa baina ya Tanzania Bara na Zanzibar. Tunatoa changamoto kwa Serikali kulifanyia kazi pendekezo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa uelewa wetu kulingana na Katiba na mapendekezo ya kamati hizo ni kuwa jambo lolote ambalo siyo la Zanzibar basi ni la Muungano kwa misingi kuwa hakuna Serikali ya Tanganyika, vinginevyo kama ni tofauti maana yake kuna Serikali ya Tatu ambayo kikatiba haipo lakini kihisia ipo na imejificha nyuma ya mgongo wa Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika kujaribu kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya Muungano, Kamati zipatazo 12 zimeundwa ingawa mapendekezo yake mengi hayajazingatiwa hadi sasa pamoja na kutumia fedha nyingi za walipa kodi. Miongoni mwa kamati zilizoundwa na Serikali ya Zanzibar kutafuta ufumbuzi wa kero za Muungano baina ya mwaka 1990 na 2003 ni hizi:- (1) Kamati ya Baraza la Mapinduzi (Kamati ya Amina) ya 1992; (2) Kamati ya Rais ya Kupambana na Kasoro za Muungano (Kamati ya Shamhuna) ya 1997; (3) Kamati ya Rais Kuchambua Ripoti ya Jaji Kisanga (Kamati ya Salim Juma Othman); (4) Kamati ya Kuandaa Mapendekezo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya Kero za Muungano (Kamati ya Ramia) ya 2000; (5) Kamati ya Baraza la Mapinduzi juu ya Sera ya Mambo ya Nje; (6) Kamati ya Rais ya Wataalamu juu ya Kero za Muungano ya 2001; (7)Kamati ya Baraza la Mapinduzi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;(8) Kamati ya Mafuta; (9) Kamati ya Madeni baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano wa Tanzania; (10) Kamati ya Suala la *Exclusive Economic Zone (EEZ);* (11) Kamati ya Masuala ya Fedha na Benki Kuu; na (12) Kamati ya Rais ya Masuala ya Simu (1996 –1999).

Mheshimiwa Spika, mbali ya juhudi za kuunda kamati kama hizo na hata kuajiri wataalamu mbalimbali ili kutafuta suluhisho la kero mbali mbali za Muungano, kwa upande wa Zanzibar, hakuna suluhisho la kweli lililowahi kupatikana, zaidi kilichopatikana ni kuendelea kutumia fedha za walipa kodi wa Zanzibar tu. Suluhisho la kweli ni kuwa na Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali ya Muungano nako kumewahi kuundwa kamati mbalimbali, pengine kwa nia hiyo hiyo ya kupata suluhisho la kero za Muungano. Miongoni mwa hizo ni: -(a) Kamati ya Mtei; (b) Tume ya Nyalali; (c) Kamati ya Shellukindo; (d) Kamati ya Bomani; (e) Kamati ya Shellukindo 2 ya kuandaa Muafaka juu ya Mambo ya Muungano baina ya SMZ na SMT; (f) Kamati ya *'Harmonization'* na*;* (g) Kamati ya Masuala ya Simu (Kamati ya Kusila).

Mheshimiwa Spika, mbali na Kamati hizo, SMZ na SMT zimefanya vikao vya pamoja visivyopungua 80 katika ngazi mbalimbali ili kuzungumzia kero za Muungano. Vilevile Serikali hizi mbili mwaka 1994 ziliomba msaada wa Shirika la Fedha la Dunia (*IMF*) ili kuzishauri kuhusiana na Benki Kuu, mgawano wa misaada na uhusiano wa kifedha (*inter-govermental fiscal relationship*). Huku juhudi hizo zikiwa hazijazaa matunda ya kuridhisha na kuonekana, tarehe 14 Novemba, 2000, wakati Rais Mkapa alipokuwa akizindua Bunge, aliahidi tena kuzipatia ufumbuzi kero za Muungano ndani ya

siku sitini (60). Ukweli ni kwamba mpaka ameondoka madarakani, hilo limekuwa ni hadithi ya 'Kusadikika', maana siku 60, mara 60 zimepita bila mafanikio yoyote na hadi leo tunaendelea kuzungumzia kero zilezile. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua zote zilizoambatana na masikitiko ya viongozi wa juu, manug'uniko ya wananchi wa pande zote mbili juu ya uendeshaji wa Muungano na ahadi nzito za viongozi wa juu Serikalini kuondoa kasoro za Muungano, sote ni mashahidi kwamba kero au kasoro hizo zingalipo pale pale na pengine kuzidi.

Mheshimiwa Spika, kero zilizozungumziwa mwaka 1984 katika vikao vya pamoja, ndizo kero au kasoro hizo hizo zilizozungumzwa katika ripoti ya Shellukindo ya 1992 na katika muafaka baina ya SMT na SMZ wa mwaka 1994 na kuzungumzwa tena katika Kamati ya Wataalamu ya SMZ ya 2001. Suala la kujiuliza ni kwa nini juhudi zote hizo zimeshindwa? Jibu ni kuwa Muungano una kasoro za kimaumbile na za kuzaliwa nazo, ukiacha ukweli wa kutokuwepo kwa nia safi miongoni mwa wenye dhamana ya kuzitatua kero hizo. Sasa je, ni kikwazo gani kinazuia Mkataba wa Muungano kutazamwa upya kwa ajili ya uboreshaji zaidi?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inadhani jibu si kwamba kero au kasoro hizo zimezoeleka au kuwa ni sehemu ya Muungano tu; jibu ni kutokuwepo kwa dhamira njema kwa wale walio na mamlaka. Vinginevyo, tunapaswa tujiulize zaidi kiini cha tatizo. Wengi wana maoni kuwa kiini cha tatizo ni mfumo wa Serikali mbili (2). Ingawa mfumo huo kweli umechangia lakini hilo bado ni jibu rahisi kwa suala gumu. "*It is an over-simplified answer to a very complicated question*."

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu ulihusisha baadhi ya mambo tu kama ilivyo kwenye orodha ya Mambo ya Muungano. Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaeleza wazi kuwa Bunge halina mamlaka ya kutunga sheria kwa mambo ya Zanzibar yasiyokuwa ya Muungano. Hivyo, kanuni ya msingi ni kuwa pande hizi lazima ziwe na kauli sawa kuhusiana na Mambo ya Muungano katika sera, utawala na sheria. Pia ziwe na kauli sawa katika kuongeza na kupunguza mambo ya Muungano huo na Katiba iweke bayana jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, kushindwa kwa Katiba yetu kutoa majibu kwa masuala ya msingi kuhusiana na Muungano ni kielelezo kuwa Muungano huu una kasoro za kimaumbile za kukosa kanuni za msingi na mipaka ya kila upande. Nini kifanyike kusahihisha hali iliyopo sasa?

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli huo, Kambi ya Upinzani inapendekeza mambo yafuatayo yazingatiwe ili kuimarisha Muungano wetu:-

(1). Lazima viongozi tubadili utamaduni wa kuona kwamba Muungano huu ni baina ya mkubwa na mdogo (*a big brother - small brother relationship*) au kuuona ni uhusiano wa ndoa ambapo mmoja ni mume na mwingine ni mke. Tukubali ukweli

kwamba Zanzibar na Tanganyika zilikuwa nchi mbili huru zilizokubali kupunguza baadhi ya madaraka yake kwa faida ya umoja huo.

(2). Kuyapokea kwa moyo safi malalamiko ya muda mrefu ya pande zote mbili na kuyatafutia ufumbuzi kwa nia njema.

(3). Kuupitia upya Mkataba wa Muungano kwa nia ya kuuimarisha na sio kumdhoofisha au kumnufaisha mshiriki mmoja wa Muungano dhidi ya mshiriki mwengine.

(4). Ijulikane wazi kwamba mjadala wa kero au kasoro za Muungano si wa wengi dhidi ya wachache (*majority versus minority*), bali uwe ni mjadala wa wawakilishi wa Zanzibar na wa Tanzania Bara.

(5). Mjadala huo upewe muda *(time limit)* wa angalau kuzimaliza zile kero zilizopo.

(6). Kero za Muungano zitatuliwe kwanza kabla ya hatua ya kuiingiza Tanzania katika Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya mapendekezo haya ni kuwaeleza Watanzania, kupitia Bunge lako Tukufu, kwamba sisi katika Kambi ya Upinzani, tunaamini kuwa kama kuna nia njema ya kisiasa, mgogoro wa Muungano ni mwepesi mno na wala hautaki miujiza itoke mbinguni kuweza kupatiwa ufumbuzi. Sisi wenyewe tunaweza kubadilisha kila kitu na kuufanya Muungano huu kuwa kweli Muungano wa heshima, umoja na mshikamano baina yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena na tena kwamba kitu pekee kinachohitajika hapa ni nia njema kutoka kwa watawala wetu. Tumekuwa na uzoefu mbaya sana wa kuweka ahadi na; au sheria, kisha kutekeleza kinyume chake, ambayo ndio mambo yanayogharimu hatima ya Muungano wetu. Ukosefu wa nia njema kila siku unatupeleka kubaya. Hii ni aibu kwa viongozi wa Taifa hili, maana ahadi na sheria si maandishi tu, bali ni uamuzi na utashi wa makusudi wa mhusika kuheshimu maandiko hayo kwa vitendo. Ukosefu wa nia njema ni donda ndugu kwa viongozi wa Tanzania kwani hakukua na sababu ya Zanzibar kutokuwa mwanachama kamili wa Afrika Mashariki kama ilivyokuwa kabla ya kuvunjika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki 1977. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama changamoto, naomba niliulize Bunge lako Tukufu, ni nani aliyewapangia viongozi wa nchi zetu tatu (3) za Afrika Mashariki, yaani Tanzania, Kenya na Uganda kuanzisha Bunge lenye Wabunge 27, kila nchi ikitoa idadi sawa ya Wabunge tisa (9) tu? Kwa nini wawe tisa (9) tu wasiwe arobaini (40) au hamsini (50) kulingana na ukubwa wa nchi mwanachama na idadi ya wananchi wake? Jibu ni kwamba hakuna miujiza yoyote ile, isipokuwa hayo yalikuwa ni maamuzi ya makusudi ambayo yameheshimiwa na wahusika kwa lengo la kujenga umoja wa usawa na haki.

Mheshimiwa Spika, lakini nchi tatu hizi bado zina Mabunge yao nje ya Bunge hilo. Si hivyo tu, bali pia udugu ulio nao nchi hizi tatu hauwezi kulinganishwa na udugu

tunaoutetea na kuupigia kelele kati ya watu wa Zanzibar na wa Tanzania Bara. Nakusudia kusema kwamba Wazanzibari na Watanzania Bara, ni ndugu zaidi kuliko tulivyo Watanzania na wenzetu wa nchi nyingine za Afrika Mashariki. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, kwa nini sisi tulio ndugu zaidi tumeshindwa kwa kipindi cha miaka 43 kuweka mfumo wa hiari na maridhawa wa kuendesha Muungano huu? Wazungu wa Afrika Kusini, waliowauwa Waafrika na kujenga uhasama muda mrefu, waliposema yaishe, yaliisha.

Mheshimiwa Spika, mbona hapa kwetu 'kero za Muungano' haziishi? Kinachokosekana hapa Tanzania ni nia njema tu ya utashi wa kisiasa. Hivi kwani nani angekuja kutuzuia kama tutasema "Watanganyika chagueni Bunge lenu na Wazanzibari chagueni Bunge lenu, na baada ya hapo Mabunge hayo yachaguwe wabunge kumi (10) kutoka kila upande ili wawe Wabunge wa Muungano?" Hilo linawezekana na wala mbingu hazitaanguka, wala bahari kuchemka, lakini shuruti litanguliwe na nia njema.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya kuwa na nia njema, uongozi wa Tanzania vile vile unakosa mfumo wenye daraja za kihekima kusimamia na kutatua matatizo ya kitaifa.

Wenzetu wa Afrika Kusini, baada ya uhasama wa muda mrefu, wamejiwekea daraja ya mwisho ya kutatua matatizo ya kitaifa ambayo ni **"***Supreme Constitutional Court"* chombo ambacho hakiingiliwi na wanasiasa na maamuzi yake hayana siasa. Huko hata Rais atahojiwa au kuulizwa kulikoni! Hapa kwetu hadi leo hatujaweka Mahakama ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwamba hapa petu Tanzania hata Rais anapokuwa amekiuka Katiba au sheria za nchi hakuna wa kumwambia "sivyo" au "huwezi kuendelea kufanya hivyo." Tunamngojea mpaka anaacha madaraka ndipo tunaanza kumwandama wakati "ameshatumaliza". Kazi yetu Watanzania ni kuwasifu marais wawapo madarakani na kuwatukuza huku tukilalamika chini ya miti.

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunataka kumaliza kero za Muungano, lazima Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete na viongozi wenzake wa Chama Cha Mapinduzi wabadilike; na nafasi ya kufanya hivyo wanayo. Lazima kuanzia sasa wawe na siasa nyingine kuelekea Zanzibar, kwa upande mmoja, na wabadilishe siasa za ndani ya Tanzania Bara, kwa upande mwingine. Lazima waitazame Zanzibar kwa jicho jipya la kuwa nayo ni nchi...!

**SPIKA:** Mheshimiwa Rizik nitakuachia umalize lakini dakika zako itabidi Mheshimiwa Suzan Lyimo masuala ya Mazingira afupishe kwa kiwango hicho hicho.

**MHE. RIZIKI O. JUMA – MSEMAJI WA UPINZANI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Ahsante nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, iliyokubali kwa hiari yake kupunguza baadhi tu ya madaraka yake kwa Jamhuri ya Muungano na pia watambue Watanzania Bara nao wana haki ya kuwa na Serikali yao kwa mambo yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima zote kwako na kwa chombo hiki kitukufu, Kambi ya Upinzani inamshauri Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, aelekeze ari, nguvu na kasi yake mpya katika kutatua kasoro au kero za Muungano kwa kuchukua ushauri uliotolewa na Watanzania mbali mbali ili tufanikiwe kuupa dawa Muungano wetu.

Ukweli ni kwamba, kwa utitiri wa Tume na Kamati ambazo nchi hii ilishawahi kuziunda huko nyuma kushughulikia matatizo ya Muungano huu, Mheshimiwa Rais hana tena haja ya kuunda Kamati na Tume nyingine ambazo zinakula pesa nyingi za walipa kodi, ilhali wanajiuliza maswali ambayo majibu yake tayari yamo kwenye makabrasha ya kamati na tume zilizopita nyuma. Kumbe kitu kidogo na cha pekee anachohitajika kukifanya Mheshimiwa Rais, ni kuyasoma makabrasha hayo na kuyafanyia kazi yaliyopendekezwa kwa uadilifu na moyo wa kuijenga Tanzania imara yenye Zanzibar imara kwa upande mmoja, na Tanzania Bara imara, kwa upande mwingine.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, nitoe uhakikisho wa upande wa Kambi ya Upinzani kwamba tuko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa karibu na kwa muda wote ili kuijenga nchi hii. Tanzania ni yetu sote na hakuna mwenye hatimiliki ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, Muungano ni mzuri. Ni umoja, ni nguvu. Tuupalilieni unawiri, uimarike, wala tusiupige teke kwa kuvitupa visiwa vya Zanzibar mbali sana katikati ya Bahari ya Hindi. Tukifanya hivyo, vinaweza kuzama. Vikizama, Muungano utakuwa wapi?

Mungu Ibariki Afrika! Mungu ibariki Tanzania!

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa, Visiwa vya Zanzibar haviwezi kupigwa teke wala haviwezi kuzama. Namwita sasa Mheshimiwa Suzan Lyimo. Mheshimiwa Suzan naona una mtindo mpya wa nywele ambao kwa taarifa yako umezua utata hapa Bungeni. Kuna baadhi wanasema kwamba sasa unapendeza zaidi na baadhi wanasema sio. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO (k.n.y. MSEMAJI WA UPINZANI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuwasilisha hotuba hii. Kwa niaba ya Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, kama inavyoelekezwa na Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2004, Ibara ya 43 (5) (b) (c) na 81 (1).

Mheshimiwa Spika, kabla sijasoma hotuba yangu, nami niungane na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa wazazi wa marehemu Amina Chifupa aliyetutoka hivi karibuni. Mungu ampumzishe kwa amani. *Amin!*

Mheshimiwa Spika, aidha nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi, na Naibu Spika, Mheshimiwa Anne S. Makinda, kwa jinsi mnavyoliendesha kwa busara Bunge letu hili Tukufu. Aidha, nampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Professa Mark Mwandosya, kwa jinsi anavyoshughulikia masuala ya mazingira kwa umakini mkubwa. Vilevile nawapongeza viongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kuniteua kwa mara ya pili kuwa msemaji wa Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa mazingira katika uhai wetu, na madhara makubwa ya uharibifu wa mazingira katika sekta ya madini, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Tanzania, Bwana Ludovick Utouh amechaguliwa na Ofisi ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Duniani *(Intosai)* kuongoza Kamati ya Dunia kufanya Ukaguzi wa mazingira. Hii ni heshima kubwa sana kwa Nchi yetu. Kambi ya Upinzani inachukua fursa hii kutoa pongezi zake za dhati kwa Ndugu Ludovick Utouh, kwa uteuzi huo ambao kwa njia moja au nyingine unafuata mkondo wa kazi aliyoifanya Mheshimiwa Ntagazwa.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Mazingira ilipitishwa mwaka 1997 kuiwezesha Serikali kupambana na uharibifu wa mazingira. Ni jambo la Busara japokuwa kuna wachache ambao wametumia sera hii vibaya, Mazingira ni uchumi, hivyo basi mazingira ndio njia mbadala ya kupiga vita umasikini katika jamii zetu. Mazingira ni dhana pana sana lakini kwa ufupi ni jinsi ya kutunza ardhi kwa ustawi mzuri wa mimea kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mkataba wa *Basel* ambao unahusu udhibiti wa utupaji wa taka za sumu na usafirishaji wake baina ya nchi na nchi (1989), kituo cha Teknolojia na Uendeshaji Endelevu wa Viwanda *(CPCT*) kilianzishwa mwaka 1995. Madhumuni ya kuanzishwa kwa kituo hiki ni kuhamasisha na kujenga uwezo wa viwanda na wadau wengine nchini katika teknolojia na mbinu za uzalishaji bora na matumizi endelevu.

Mheshimiwa Spika, japokuwa Tanzania ni mwanachama wa mkataba huo lakini kuna mambo ambayo Watanzania wanaona kuwa Serikali inayafanya kwa makusudi kwenda kinyume na mkataba huo wa *Basel.* Tunayasema haya kwa kuwa Serikali ilitoa kibali kwa kiwanda cha kutengeneza nguo cha Karibu *textile* ambacho kimejengwa katika makazi ya watu jambo ambalo ni kinyume cha sheria na taratibu kwani mabaki yatokanayo na mchakato wa uzalishaji una athari na ni sumu kwa mazingira na viumbe hai. Ushahidi uliowazi ni maji yenye sumu yanayotoka katika kiwanda hicho na kuachiwa kutiririsha taka hizo kwenye Mto Kizinga ulioko Mbagala-DSM. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iweke suala hili wazi, je, Serikali inatimiza wajibu wake katika kusimamia mkataba huu wa *Basel*?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe taarifa rasmi hapa Bungeni kuhusu shughuli zinazofanywa na Kampuni ya *Gulf Park Petroleum* iliyopewa maghala ya kilichokuwa kiwanda cha mbolea Mkoani Tanga. Maghala hayo yapo katika eneo la makazi ya watu. Japokuwa ni ukweli usiokuwa na ubishi kuwa Serikali ilikuwa imefanya makosa kwa kutoa kibali cha kujenga kiwanda cha mbolea katika makazi ya kuishi wananchi (*Raskazoni area*-Tanga).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria mpya ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, Baraza limepewa majukumu ya kusimamia na kudhibiti uchafuzi wa mazingira, kupitia na kudhibiti tathmini ya athari kwa mazingira. Sheria inalipa Baraza kwa kushirikiana na sekta zote mamlaka ya kusimamia na kuratibu masuala ya mazingira na kuwachukulia hatua za kisheria wanaoharibu au kuchafua mazingira. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tathmini mpaka sasa toka kuanzishwa kwa sheria hiyo mpya ni wachafuzi wangapi wamechukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, taslia ya madini ni mojawapo katika waharibifu wakuu wa mazingira. Kemikali nyingi zinazotumika katika usafishaji wa dhahabu ni hatari kwa mazingira na viumbe hai kwa ujumla. Utaratibu unaotumiwa na makampuni ya madini katika kuhifadhi na kuteketeza taka sumu hizo umekuwa na tatizo kubwa sana hasa kwa wananchi wanaoishi katika vijiji vilivyo jirani na migodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, chini ya sheria ya madini ya mwaka 1998, kuna kifungu kinachomhitaji mwombaji wa leseni ya kuchimba madini, katika utaratibu mzima wa kuomba leseni, moja ya sharti ni lazima ionyeshe mpango wao wa kutunza na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria hiyo ya madini ya mwaka 1998, kifungu cha 39(1) (d) kinachomtaka Waziri mwenye dhamana kabla ya kutoa idhini ya leseni, kwanza, lazima aidhinishe mpango wa mkakati wa kutunza na kuhifadhi mazingira kama ambavyo unaonyeshwa na kampuni husika; je, Serikali inafuatilia kama makampuni ya uchimbaji wa dhahabu wanafuata na kutimiza masharti hayo? Kama hawafuati, Serikali imekwisha chukua hatua gani?

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Mtakuja linalotumiwa na mgodi wa Geita kwa ajili ya kumwaga taka hatari zenye kemikali, linatiririsha maji maji yenye sumu kwa wananchi wanaokaa pembezoni mwa vijito vinavyo tumiwa na wananchi wanaoishi pembezoni mwa mgodi huo. Mbaya zaidi wakazi wa kijiji cha Nyakabale wamepoteza mifugo yao kutokana na mifugo hiyo kunywa maji katika malambo yaliyochimbwa kwa ajili ya mifugo hiyo. Tunaitaka Serikali itoe kauli kuhusu hasara iliyopatikana na ambayo inaendelea kutokea kwa wakazi wa Kijiji hicho katika wilaya ya Geita.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa zilizopatikana hivi karibuni toka Wilaya ya Tarime kuandikwa katika gazeti la Mwananchi Toleo Na.02574 la tarehe 30 Juni, 2007, Tarafa ya Ingwe, Kata ya Nyarukoba, kuhusu kuzuka kwa ugonjwa wa ajabu ulioua mifugo 1,440 ambao unadaiwa kuwa hatari kuliko ule wa Bonde la Ufa, kulingana na mazingira ya kata hiyo ambayo ni jirani kabisa na Mgodi wa *North* Mara, na kwa

matatizo yaliyojitokeza Geita kwa wananchi kupoteza mifugo yao kutokana na taka za sumu zitokazo mgodini, Kambi ya Upinzani inaona ugonjwa huu unawezekana ni *"spillage"* ya maji ya sumu toka mgodini. Tunaitaka Serikali kwanza itoe tathmini yake juu ya udhibiti wa taka sumu zitolewazo na mgodi na jinsi gani wananchi walioathirika na taka hizo watakavyofidiwa.

Mheshimiwa Spika, madhara mengine ambayo yanatarajiwa kutokea ni yale yanayosababishwa na Mgodi wa *North* Mara kutupia taka zenye sumu katika mto Tigita ambao ni tawi la mto Mara unaoingia Ziwa Viktoria. Hapa tujaribu kujiuliza ni watu wangapi wanatumia maji na samaki kutoka katika Ziwa Victoria. Tafiti zilizofanywa na chama cha wanasheria wa mazingira Tanzania (*LEAT*) zinazoonyesha ni jinsi gani migodi inavyohatarisha usalama wa mazingira na pia kutoa tahadhari ya madhara ya kushindwa kuteketeza taka sumu toka katika Migodi kulingana na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, chini ya Mkataba wa Bioanuwai, Serikali imetekeleza miradi mikubwa ya kupambana na matatizo ya mazingira ikiwa ni pamoja na Programu ya Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira katika eneo la Ziwa Victoria ulioanza mwaka 1997. Katika utekelezaji wa Mkataba wa Vienna –unaohusu kulinda Tabaka la Hewa ya Ozoni angani wa mwaka 1985 na Itifaki yake ya *Montreal* inayohusu kemikali zinazoharibu Tabaka la Ozoni, la mwaka 1987. Pamoja na mambo mengine tabaka la ozoni linaharibika kwa kiasi kikubwa kutokana na kufyeka misitu yetu bila kuwa na mkakati madhubuti wa kurudishia miti hiyo inayofyekwa.

Mheshimiwa Spika, sifa kuu katika shughuli za uchimbaji madini ni uharibifu wa mazingira. Kama inavyoeleweka lengo kuu la kuhifadhi misitu yetu ni kutunza na kulinda tabaka la hewa ya Ozoni. Kambi ya Upinzani imesikitishwa na kitendo cha Serikali cha kutoa karibu nusu ya hifadhi ya msitu wa Taifa wa Geita kwa kampuni ya Kuchimba dhahabu ya *Geita Gold mine*. Aidha, Serikali inakwenda kinyume na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1997 na Itifaki ya Kyoto ya mwaka 1997 wa kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame. Kambi ya Upinzani inataka kauli ya Serikali, wananchi wanaozunguka hifadhi hiyo ya msitu wa Geita wamenufaika vipi ?

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/06 mapato ya Serikali kutoka katika Hifadhi zetu za Taifa 14, ilikuwa ni *Tshs*.45.6 bilioni. Kati ya fedha hizo hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ilichangia *Tshs*.19.7bilioni. Mazingira ya mlima wetu ambao ni moja ya urithi wa Dunia na ambayo yanatuingizia kiasi kikubwa cha fedha kama Taifa yameharibika vibaya sana na hii ni sababu kubwa inayosababisha theluji ya mlima Kilimanjaro kuyeyuka.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya mlima yanaharibika kwa sababu kuu kuwa njia zinazotumika kupanda na kushuka Mlima Kilimanjaro ni zile zile tangu enzi za Mjerumani. Mojawapo ya njia za kuunusuru mlima wetu ambao ni hazina yetu ni kufungua njia zingine mbadala na kufunga zile za zamani ili mazingira yaweze kurudia katika hali yake ya uasilia.

Kama tutafuata ushauri huu wa kuzifunga njia zinazohatarisha mazingira ya mlima na kufungua mpya kama kuzifanyia njia mzunguko, kutasaidia kuhifadhi mandhari ya mlima jambo ambalo litaihakikishia Serikali kuwepo kwa hazina ya mapato yake.

Kambi ya Upinzani ina uhakika kama bonde la Usangu limefanyiwa jitihada za makusudi, vilevile inawezekana Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ikafanyiwa mkakati endelevu wa kunusuru mazingira yanayouzunguka. Kurudisha ualisia wa Mlima Kilimanjaro ni uhakika wa kuiongezea nchi yetu kipato.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka utaratibu wa kwamba kabla ya kutoa leseni ya aina yoyote kwa uanzishwaji wa kiwanda au shughuli ya uchimbaji madini ni lazima Ofisi ya Makamu wa Rais ifanye tathmini ya uharibifu wa mazingira unaoweza kujitokeza katika shughuli husika (*environment impact assessment*).

Hili litasaidia sana kwani pamoja na mambo mengine hawa ndio watakaokuwa katika nafasi nzuri ya kutumia zile *"Rehabilitation Bond"* zinazowekwa na makampuni ya madini kwa mujibu wa sheria ya madini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha na nashukuru kwa kunisikiliza. Ahsante. (*Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Suzan Lyimo pia umeokoa na muda na umesoma kwa ufanisi nakupongeza. Sasa Waheshimiwa Wabunge katika orodha yangu ninao wachangiaji watatu, Col. Saleh Farrah, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir na Mheshimiwa Dr. Mzeru. Kwa hiyo, tutaanza na Col. Saleh Farrah. Hayupo! Basi Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir yeye yupo. Ahsante.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuwa mmoja kati ya wachangiaji wa Hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais wa Tanzania. Kabla sijaendelea naomba kuiunga mkono hoja hiyo mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ruhusa ingawa leo asubuhi ulisema kwamba, hizi rambirambi kidogo tupunguze, lakini naona sikuwafanyia haki wapiga kura wangu wa Jimbo la Matemwe, kwa sababu nao wamepiga simu kunipa rambirambi na kupitia kwangu kuzileta kwako kwa vifo vilivyotokea vya Marehemu Juma Jamaldin Akukweti na vile vile Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia. Kwa niaba yao, naomba mzipokee rambirambi hizo. Hawa walikuwa wenzetu na tumefanya nao kazi kwa karibu lakini Mwenyezi Mungu imefika wakati amewachukua, tunawaombea awalaze mahali pema peponi. *(Amen)*

Vile vile naomba kutoa rambirambi zangu kwa familia ya Marehemu Stephen Kazi, ambaye alikuwa Mbunge katika Bunge lililopita. Amefariki akiwa kazini akilihudumia Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo nataka kusema kwamba, Tanzania tumebahatika sana kuwa na Muungano. Muungano ambao katika Afrika ni wa pekee uliodumu. Kulikuwa kuna Muungano ambao baadhi yetu tumeshuhudia wa Sene-gambia ulivunjika. Tukashuhudia Muungano wa Libya na Egypt vile vile umevunjika, lakini Tanzania miaka 43 tuko na bado tunaendelea na Muungano wetu. Tunaomba Mwenyezi Mungu, aubariki Muungano huo. Lakini kingine tulichokuwa tumebahatika ni kwamba, baadhi yenu, Mheshimiwa Spika, ukiwa ni mmoja kati yao, lakini vile vile kuna Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru na baadhi yao, nafikiri hata Mheshimiwa Juma Ngasongwa, walikuwa ni watu ambao wamefanya kazi na waasisi wa Muungano huu kwa karibu zaidi. Hawa tunashuhudia leo kwamba, tunao na wamerithi busara na hekima walizotumia waasisi wa Muungano huu na kwamba, leo tuko nao pamoja hapa tunazungumzia suala hili.

Mheshimiwa Spika, hilo ni jambo la kushukuru, lakini niseme tena vilevile kwamba, Mheshimiwa Rais wa Tanzania ni mmojawapo kati ya Wajumbe wa Tume za mwanzo zilizochaguliwa kushughulikia masuala ya Muungano wa Chama cha CCM baada ya Afro-Shiraz na TANU, chini ya uongozi wa Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Marehemu Abedi Amani Karume, kuunganisha nchi hizi kama Serikali. Lakini vile vile kuunganishwa nchi hizi kwa vyama vya siasa. Muungano ni lazima kwa hali zote tuulinde na kama si Muungano tusingekuwepo hapa tulipo leo.

Mheshimiwa Spika, tuna vijana ambao ni mahiri, makini na wachapakazi, ambao sasa hivi ni viongozi wakubwa katika nchi hii; Rais wa Tanzania, Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar, Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi. Hayo yanayozungumzwa kama ni kero za Muungano kwa upeo, nataka niseme kwamba, sijui kama ni kweli kero za Muungano. Kuna masuala ambayo ni makubwa zaidi yamefanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu chini ya Uongozi wa Rais wa Tanzania, ambayo ni makubwa, mazito na yanataka uamuzi ambao ni wa kufa na kupona, yamefanywa katika nchi hii katika kipindi hiki cha Awamu ya Nne. Ninajiuliza kumbe hii ni kweli kwamba, suala la magari ya Zanzibar (ZNZ), kuingia Bara ni kero ya Muungano; ni kweli hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni suala la kukaa na kuamua kusema kwamba, haya magari mengine ndiyo limekwisha. Dhamira lazima iwepo katika jambo lolote lile na mifano tumeoneshwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kipindi cha miaka karibu miwili. Kujenga shule zaidi ya 1,000 za sekondari katika nchi hii ni mifano mikubwa na ni maamuzi ambayo ni makubwa kabisa yamefikiwa. Tunakuja leo suala la magari au suala la bandari, bidhaa kutoka Zanzibar kuingia Bara ni kero ya Muungano na yanawekwa katika kujumuisha kero za Muungano. Naiomba Serikali ya Muungano na namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa nguvu zake zote, suala hili aliondoshe. Sisi vijiweni au katika maskani tunaokaa Zanzibar, tunaulizwa maswali yanakuwa mengi kuliko majibu tuliyonayo katika hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba suala la *TRA,* kwa maana ya mizigo kutoka Zanzibar na suala la magari kutoka Zanzibar, haya tusiyajumuishe katika kero za

Muungano. Waliotangulia hapa walizungumzia suala la mafuta, wamezungumza suala ya madini, lakini hivi kweli sisi tukashindwa nchi hii kuweza kutatua masuala haya?

Mafuta yapo Tanzania, madini yapo Tanzania na sisi ni Viongozi wa Tanzania, Bunge lipo hapa, Baraza la Wawakilishi liko Zanzibar, tukatafute *experts* kutoka nje watutafutie. Tutagawana vipi mali zetu? Haiwezekani, haiji na wala haiingii akilini.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Waziri wa Mambo ya Muungano na kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, masuala haya tungeomba yakamilishwe katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja. Haya masuala yanatusababishia wakati mwingine Zanzibar kusutwa, kuambiwa kwamba sisi tunakuja huku hatuna tunachokizungumza, tunaonekana tunafuata tu kuingia katika Bunge hili. Kama kweli tunathamini Muungano uliokuwepo na tunathamini waliokuwa wameanzisha Muungano huo na kwamba Muungano si jambo la mchezo. Kuna nchi na nchi, si za Afrika wala za Ulaya, zinazoweza kufanya kitu kikubwa kama hiki, basi masuala haya tunaomba yashughulikiwe na yakamilishwe. Kushindikana kwake, tunaomba suala hili tuleteeni katika Bunge hili tuweze kulishughulikia.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Naomba radhi kwa Mheshimiwa Ibrahim Sanya, alikuwa ni mwombaji wa kwanza kabisa kuchangia. Aliomba tangu jana lakini sasa nilipopata maombi ya leo sikuweza kumtaja. Ninaona basi kama yupo tayari achangie na wakati huo huo ajiandae Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka. Mheshimiwa Sanya wewe kwa urefu wako pengine ungetumia chombo hiki hapa.

**MHE. IBRAHIM M. SANYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa heshima hii uliyonipa. Mimi nataka nianze kuelezea historia fupi ya Zanzibar, baada ya Mapinduzi tulipoungana na Tanganyika, tuli-*form* kitu kinachoitwa Tanzania. Uchumi ulivyokuwa na Zanzibar ilivyoanguka kiuchumi; ni vipi Serikali ya Muungano inaweza ikaisaidia Zanzibar kuondokana na kero hizi ambazo zaidi zinasababishwa na wananchi wa Zanzibar? *(Makofi)*

Zanzibar baada ya Mapinduzi, kwanza *population* ilikuwa ndogo, ilikuwa na watu laki tatu. Uchumi ulikuwa mkubwa kutokana na zao la karafuu kuwa na soko zuri katika Soko la Dunia. Tukahimili mambo mengi sana na hakuna kiongozi shujaa aliyekuwa na *vision* kama kiongozi wa mwanzo wa Zanzibar, Hayati Mzee Abedi Amani Karume. Alifanya mambo ya maajabu mengi sana Zanzibar ambapo hata katika nchi nyingi za Afrika hawakuweza kuyafanya. Tulijenga viwanja vya kisasa vya michezo, barabara zilitengenezwa mbilimbili, kutokana na *population* iliyokuwepo ambapo hadi leo zinawasaidia watu milioni moja wa Visiwa vya Unguja na Pemba. Aliweka televisheni ya rangi ambapo kwa Kusini mwa Jangwa la Sahara ilikuwa *number one*. Mwaka 1974 tulitazama *World Cup* kwa kutumia televisheni ya rangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya, yaliyoandikwa yameandikwa akaondoka. Ikaja awamu ya pili, tukaendeleza tukanunua meli yetu mpya kutoka Japan kwa milioni 63, *MV Maendeleo* na *MV Mapinduzi* milioni 28, tukajenga Hoteli ya Bwawani kwa zaidi ya

shilingi milioni saba. Wakati ule fedha ilikuwa na thamani. Tuliingia katika Muungano kwa imani kubwa kabisa kwamba, ninyi mko karibu nasi na tuna historia nzuri na nchi ya Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, uchumi ulivyo sasa hivi, juzi nilikuwa naangalia kwenye vyombo vya habari, nikaona *inflation* ni asilimia 11.4. Wazanzibar wanaumia kiuchumi na kinachowaumiza ni gharama za usafirishaji, uzalishaji umekuwa mdogo, kusuasua kwa kutengeneza Bandari, kitu ambacho ndiyo uti wa mgongo, baada ya kuamua kufanya hivyo kutokana na kuanguka kwa zao la karafuu. Zao la karafuu lilipoanguka, tukaamua kutafuta *alternative*, hakukuwa na jinsi nyingine isipokuwa biashara. Awamu ya pili ilipoondoka ikaingia ya tatu. Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, alifanya kazi nzuri akishirikiana na Mheshimiwa Seif Sharrif Hamad, tukubali ukweli tunazungumzia historia. *(Makofi)*

Wakafungua milango ya kibiashara mwanzo kuliko hata ninyi huku Bara. Tukaruhusu watu kuhodhi fedha za kigeni, ambacho kilikuwa kitu cha maajabu kwa nchi hii. Tukafungua milango ya biashara, watu waka-*import* na tukaifanya bandari ikawa *very active* kwa uchumi wa Zanzibar. Matokeo yake ni nini? Zanzibar ikainuka katika kipindi kifupi tu tukaiona *purchasing power* namna ilivyokuwa na *circulation* ya pesa na watu namna walivyojazwa kwa *formula* ya kufungua bandari tu.

Hawakuishia hapo, wakasema sasa twende katika sekta nyingine ya utalii, tukafungua milango ya utalii kwa vile *the only place in Africa, which has virgin beaches* ni Zanzibar na watu walivyogundua hivyo wakaonesha imani ya kuja kufungua mahoteli. Watalii walipoanza kuja Zanzibar ikawa ni *source of income* kwa Serikali ya Zanzibar. Bandari ya Zanzibar wakati tunateremsha mizigo, wafanyabiashara wa Zanzibar wakaonesha hamu ya kuitumia na mizigo ikawa inashuka pale. Baadae mizigo hiyo ikawa inahaulishwa inakuja Bara. *(Makofi)*

Bara nao wakawa wanafanya biashara kutokana na mizigo ya Zanzibar, kabla ya wao kufungua milango ya biashara. Sijui ni kwa sababu gani ikawa Bara sasa napo kuna usumbufu wa mizigo inayotoka Zanzibar, kama ilivyo magari leo, wakaanza sasa kutoza ushuru mara mbili? Wafanyabiashara wakajiuliza; hivi tulete biashara Zanzibar tutozwe ushuru, tuchukue gharama za kupeleka Bara kwa ndugu zetu nako tutozwe ushuru; tufanye nini; tuhamie Bara moja kwa moja? Wakaondoka Zanzibar wakaiua kiuchumi bandari yetu wakahamia Tanzania Bara. Kwa dhamira nzuri na tunakuombeni mpaka hii leo kwamba, ninyi muwe tayari kuwaruhusu Wazanzibar warejeshe imani ya kuitumia bandari yao kwa unafuu wa ushuru kidogo halafu waruhusiwe kuja huku kama mnataka kutukamata mkono na kutuinua ili tuinuke kiuchumi tuwe sawa sawa na ninyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukubali tusikubali, Zanzibar hatuna ardhi ya kutosha ya kilimo na tunakwambieni Waheshimiwa mnaofanya kazi katika vyombo vya Muungano na upande wa pili wa Muungano kwamba, mnapoisaidia Zanzibar, *the other way around* mnafaidika vile vile. Niulizeni kwa nini? Mzanzibari ana historia ya kujitakia maisha mazuri. Sasa Wazanzibari watakapopata fedha kwa biashara kutokana na utalii au kwa mambo mengine madogo madogo, fedha ile itarudi huku. Mtu akitaka kujenga atanunua

saruji itatoka Tanga, Dar es Salaam au Mbeya. Atataka *furniture*, madirisha, milango na miti ya kuezekea, itatoka Mufindi Iringa, Songea, Mbeya na sehemu nyingine na atataka mabati na nondo. Sisi sasa hivi kwa sekta ya utalii, kwa taarifa yenu mpaka nyanya na nyama tunaagiza kutoka Bara. Yalipotokea matatizo ya nyama kuingia maradhi, tuliathirika sisi kiuchumi na nyama ikapanda bei kwa sababu ardhi yetu ndogo hatuna *production* kubwa.

Muungano huu usiwe kero, kesho tunaelekea kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki, kwa nini kero zianzie hapa? Leo Mheshimiwa Waziri Mkuu, anakutana na Mheshimiwa Waziri Kiongozi, kuzungumzia namna gani Zanzibar itafaidika na Shirikisho. Mimi naona maajabu hapa, unazungumzia chakula cha usiku wakati cha mchana hujakijua! *(Kicheko/Makofi)*

Zungumzieni kero za Muungano kwanza, tuziondoe halafu tuzungumzie Shirikisho na tumeshalielewa sisi, kama hatukuwa makini wanahatari hawa watu. Juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu, alituambia kwamba, Hoteli ya Mara Kenya wana vitanda 4,000, sisi tuna vitanda 930. Wamekusanya zaidi ya milioni 700 USD, sisi *only 30 million USD*, wana dhamila nzuri kweli hawa, tunaharakisha nini? Harakisheni kuondoa kero za Zanzibar sisi wa miaka 43 hawa n wa miaka 40, siku zijazo nani atakuwa bora?

Mheshimiwa Spika, mambo mengi tu ambayo yanatakiwa yarekebishwe haraka wala sina haja ya karatasi, yapo kichwani. Utakuta sisi tunazungumzia Muungano kwa maana ya Muungano, lakini hatujawa tayari kushikana mikono. Kuna kisiwa kimoja kinaitwa Ockland kule Finland, kina watu 28,000 na kuna Watanzania watatu tu. Mme mtu katoka Zanzibar, mke mtu katoka Singida na mtoto wao. Wako katika Muungano huu. Serikali ya Finland kwa kujua kwamba ni wenzao, wameungana wakaiweka ile sehemu kufanya *registration* za meli kama wanavyofanya Liberia na wana-*income* ya kutosha kuendesha kisiwa kile. Sisi leo tumeambiwa na Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe kwamba, kuna sera za utalii zitatangazwa kwenye *CNN* na Zanzibar itahusika. Mimi naona Wizara ya Utalii hata kama si ya Muungano, lakini Zanzibar ni sehemu ya Muungano na Watalii wanaokuja Zanzibar na Bara kwa vyovyote kutakuwa na sehemu za kusafiri baina ya Bara na Zanzibar, iandaliwe Sera Maalum ya Kudhibiti Watalii wanaoingia katika nchi yetu. *(Makofi)*

Wanakuja watalii kwa njia za *clubs*, pesa zinalipwa Ulaya. Sisi tunakokota *passports* zao kila kitu kinamalizikia huko. Akina *Ventaglio* hao *Norfolc* ni kampuni ambazo tayari zinalipiwa huko Ulaya. Lakini huku tunapokea watalii wanatumia nguvu kazi yetu, wanatumia mahoteli yetu, matokeo yake *income derived from* utalii inakuwa si nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, wakati mwingine nafikiri Bunge litumie busara kwa kuona kwamba, wachangiaji ni kidogo na sisi tuliokuwepo tuna uwezo wa kuchangia, utuongezee muda ili tutoe hivi vitu visaidie katika kuboresha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Linazingatiwa katika rasimu ya Kanuni mpya.

**MHE. IBRAHIM M. SANYA:** Sio hii ya hivi sasa? *(Kicheko)*

Sasa nataka niulize kitu kimoja, Zanzibar ilitaka kujiunga na *OIC,* kukawa na mvutano, lakini Dr. Salmin alifika akasema hapana naiachia Tanzania, ikiingia Tanzania na Zanzibar imeingia. Tumechukua hatua gani? Kuna nchi zinafaidika kama Uganda, Msumbiji na Malawi; kwa nini tusijiunge tunaogopa vitu gani; kwa sababu ni waislam? Hapana, kuna *Kuwait Fund* na *Abu Dhabi Fund,* tunapokea misaada yao kwa nini tusichukue *OIC*, kiti kiko wazi? Tujikurupushe tufanye haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu hizi nafasi za ki-Muungano. Utakuta kuna Shirika kama hili la *UNESCO* lipo kule Paris, kuna wawakilishi watano wanaoiwakilisha Tanzania *UNESCO*, wote ni upande wa pili wa Muungano, hakuna Mzanzibari hata mmoja. Inaumiza na sisi tuwe na sehemu katika Muungano, tuoneshe kwamba, tunawajali Wazanzibari. Leo tumeshuhudia hapa hapa ndani ya Bunge, siku kama hii imekuja Menejimenti ya *Air Tanzania*, wanatajwa majina niliona vibaya nikataka kudondokwa na machozi, hakuna Mzanzibari hata mmoja. Sababu ni nini; hatuna uwezo? Kama hatuna uwezo, kwa nini hamtujengei mazingira, mkachukua elimu ya juu na ufundi na sisi tukasomeshwa tukafikia hivyo viwango kama ilivyokuwa zamani, tulipokuwa na *quarter* katika Chuo Kikuu?

Kwa hiyo, naona hata suala la uvuvi wa bahari kuu, kuna kitu kimekuja hapa juzi ambacho kimeruhusiwa na *World Bank* kinaitwa *GEF*. *GEF* ni *Global Environment Facility,* inataka kujenga *research centre* moja Tanzania. Ziko nchi kama tano; Kenya, Madagascar South Africa na Msumbiji. Nafasi hii sasa ipelekeni Zanzibar na *fishing industry* iwe kule, ikiwa kule ina maana mtatoa ajira, tutakuwa tunatekeleza ile Sera ya Ari Mpya, Nguvu Mpya, na Kasi Mpya na ajali milioni moja katika kipindi cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wale wazanzibari watakapovua samaki wa bahari na ninyi mkavua wa *Lake Victoria,* mtaitangaza Zanzibar katika ramani ya dunia, kitakachorudi Zanzibar kitakuja huku kama nilivyoelezea.

Tutanunua ng'ombe wenu, hatuna mbao, hatuna chuma wala mabati, lakini tuna Wazanzibari ambao wana-*unique culture and they are very calm, cool and collected. Zanzibar must remain Zanzibar,* lakini Zanzibar kwa nafasi aliyokuwa nayo Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, kama hawa ndio watendaji wakubwa wa Serikali zetu mbili, wakaiunda Kamati kila baada ya miezi sita au tisa ikawa inatoa ripoti na ripoti ile ikawa inaletwa kwenye Baraza la Wawakilishi na Bunge tukakaa tukaipitia Katiba, Wizara baada ya Wizara, kipengele baada ya kipengele, tukaona yanayotufaa yasiyotufaa tukayaacha, itakuwa ni mfano mzuri na tutampa nafasi nzuri Muammar Gadaffi, kuwaunganisha Waafrika katika kuinua uchumi wa Bara hili la Afrika.

**SPIKA**: Mheshimiwa Ibrahim Sanya, hiyo ni kengere ya pili sasa.

**MHE. IBRAHIM M. SANYA:** Mheshimiwa Spika, ina maana huniongezei? Mimi nafikiri hata Wabunge nao wataridhia nikipewa dakika tano. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Siruhusiwi na Kanuni, mazungumzo yako yanaleta raha lakini Kanuni hairuhusu.

**MHE. IBRAHIM M. SANYA:** Mheshimiwa Spika, hii ndiyo raha ya kuwa na Upinzani ulio makini katika Bunge kama hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanya ahsante sana. S asa ni zamu ya Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini.

**MHE. DR. OMAR M. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

**SPIKA**: Mheshimiwa Mzeru, wengine wananiuliza hapa umesimama au umekaa? *(Kicheko)*

**MHE. DR. OMAR M. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, nimekaa kiuno kinaniuma. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi angalau nichangie katika hotuba hii ya Wizara mbili; Wizara ya Muungano, pamoja na Mazingira. Mimi nitajikita moja kwa moja katika uala Mazingira. Kwanza kabisa, napenda kuungana na juhudi zote zinazohusisha uboreshaji wa mazingira katika nchi yetu. Naamini kabisa kwamba, mazingira ni uhai na mazingira ni muhimu kwa maisha ya mwanadamu. Kama tunavyofahamu ni kwamba, sisi wanadamu tunabadilisha hewa na miti ambayo inaboreshwa na mazingira. Sisi tunatoa *carbon dioxide* ambayo miti inachukua lakini pia miti nayo inatoa *oxygen* ambayo tunaipokea sisi. Kwa hiyo, mazingira ni kitu muhimu, kwa namna yoyote ile ni vizuri tukaungana kuhakikisha mazingira yanaboreka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo nia nzuri sana katika kupanga mikakati ya kuboresha mazingira katika nchi yetu, lakini tatizo linakuja katika utekelezaji, hasa watendaji wetu wanapopokea majukumu ya Serikali na kuweza kuyapeleka kwa wananchi katika suala la kuboresha mazingira, hapo ndipo tatizo linapoanza. Watendaji wanakuwa kama vile maaskari polisi mbele ya wananchi na kitendo hiki kinawaletea kero sana wananchi kwa sababu hawatumii utaratibu ambao ungefaa kuwaelimisha wananchi jinsi gani ya kuboresha mazingira katika sehemu wanazoishi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano katika Jimbo langu la Morogoro Mjini. Jimbo la Morogoro Mjini ni sehemu tu ya majimbo manne, ambayo yanaunganishwa na Mlima wa uluguru; lipo Jimbo la Mvomero, Morogoro Kusini, Morogoro Kusini Mashariki na Jimbo la Morogoro Mjini. Jimbo la Morogoro Mjini, mji wake ulianzia milimani. Wananchi wa Morogoro Mjini walianza kuishi milimani kama miaka 200 iliyopita, baadae mji ukasambaa pole pole na kufikia mabondeni ambapo zamani watu waliokuwa wanaishi mlimani walikuwa wanalima mabondeni kupata chakula cha kufanya wao waweze kuishi.

Mheshimiwa Spika, lilipotokea suala la mazingira, watendaji wanafikiria kwamba, kigezo cha kuboresha mazingira katika milima ni kuwahamisha wananchi wake, kitu ambacho ni kosa. Mazingira maana yake si miti tu, mazingira ni pamoja na kuboresha ardhi na kuboresha vyanzo vya maji, pamoja na vitu vingi tu. Kwa hiyo, wananchi wale wanapoishi kule milimani, kikubwa kule ambacho ningefikiria mimi ni kwamba, wangepaswa kupewa elimu ya mazingira ili waweze kujua jinsi gani wanaweza kuishi kule milimani bila kuharibu mazingira na hiyo inawezekana kwa sababu kwa kipindi kifupi tu baada ya wananchi hawa kuwahamasisha katika suala la mazingira, wameshaanza kuboresha kwa ari kubwa sana katika Milima ya Uluguru. Sasa hivi miti imeenea, hakuna uchafuzi wa mazingira, mapori na mito yetu wala haionekani kama ilivyoonekana zamani kwa sababu inapita chini ya miti. Kwa hiyo, mtu anapopita Morogoro kamwe haoni maji, asifikiri hakuna maji. Maji yapo lakini yamefunikwa na miti. Wananchi wameshaamka sasa katika suala la kuboresha mazingira. Kwa hiyo, suala la msingi nafikiri kikubwa mno hapa ni elimu, jinsi gani ya kuboresha mazingira katika Milima hii ya Uluguru badala ya kufikiria kuwahamisha wananchi wake kuwa ndiyo *solution.* Kwa sababu kuna faida na hasara za wananchi wale kuishi milimani.

Mheshimiwa Spika, faida ya kwanza ya wananchi hao kuishi mlimani ni kwamba; kwanza kule milimani kuna mazao ambayo huku bondeni hayapatikani, yanapatikana sehemu za milima kwa sababu kuna hali ya hewa ya baridi. Kwa mfano, matunda, ndizi, mboga na kadhalika. Pia wananchi hao wanapoishi kule juu, faida nyingine ni kwamba, wao wanakuwa walinzi wa vyanzo vya maji, lakini pia wanakuwa walinzi wa kulinda ile misitu kama wakielimishwa. Lakini pia wanalima mazao ambayo yanakuwa yanaongeza ajira kwa vijana wetu walioko Morogoro Mjini ambao hawana kazi. Wanawake kwa wanaume wao hununua mazao kwa wakulima na baadaye huja kuuza huku mjini kwenye masoko na kujipatia kipato cha kuwasaidia wao na familia zao na wazazi wao ambao ni wazee, hawajiwezi. Kwa hiyo, hiyo ni faida kubwa. Faida nyingine ni kwamba, kwa sababu tunacho Chuo cha Kilimo cha Sokoine pale Morogoro kimeshaanzisha kuwafundisha hao wananchi kulima kilimo cha makinga maji. Kilimo hiki ni kizuri, kinasaidia mvua zinaponyesha, maji yasiende bondeni, maji haya yote yanaishia kwenye milima na kuleta unyevunyevu na hivyo kuboresha ardhi. Lakini, pia kuweka mbolea kwenye milima hii wakati wa kulima mazao yao ya mboga mboga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kufikiria kwamba kuwahamisha wananchi hao ndio *solution*, siyo *solution*. Kuwahamisha wananchi hao maana yake ni kusaidia kuharibu mazingira. Ili kuboresha mazingira ni kuwaacha wananchi hao waishi milimani. Mimi nakubali wako wananchi wachache ambao kwa bahati mbaya wamevuka kwenye mipaka ile tuliyojiwekea toka zamani kwamba, wameingia kwenye misitu, ni wachache tu ambao tunatakiwa tuwatoe. Lakini, hata katika kuwatoa wananchi hao kwa sababu wameshakaa muda mrefu, ni vizuri pia tukawafikiria kufuata Sheria ya Ardhi hasa Sheria Na. 4 ya mwaka 1999 ya Mijini na Sheria Na. 5(3)(g) ya mwaka 1999 ya Vijijini kwamba, wananchi hawa nao watakapohamishwa, basi Sheria hii kuhusu suala la fidia izingatiwe kwa maana kwamba, walipwe ardhi yao ile ambayo wanaishi na pia walipwe mazao yao kwa wakati huu na kwa bei ya wakati huu. Pia walipwe majengo yao na usumbufu wa kuwahamisha kama wanavyohamishwa wafanyakazi na pia walipwe pango la miaka mitatu. Siyo kuwahamisha tu, mtu unamtoa hapa unampeleka mahali pengine, hilo la

kwanza. Wananchi hawa wanaishi, wana nyumba na mashamba, unapomtoa huwezi kwenda kumwonyesha kiwanja, inabidi umpe shamba siyo kumpa kiwanja. Unampa shamba ili ndani ya shamba hilo ajenge nyumba yake na sehemu nyingine inayobaki atakuwa analima ili apate mazao ya kumsaidia yeye na familia yake.

Mheshimiwa Spika, nafikiri elimu ndio kigezo muhimu zaidi kuliko suala la kuwahamisha wananchi. Kama kigezo ni milima, milima ipo mingi katika nchi hii. Kule Tanga kuna Milima ya Lushoto. Lushoto mimi nimeishi, hakuna bonde kabisa ni milima tu. Wananchi hao wanaishi milimani, mazao yao yote wanalima milimani kwa maana ya migomba, miwa, mbogamboga, mazao ya matunda na ukisema uwahamishe, utawapeleka wapi watu hawa? Kikubwa ni kuwaelimisha jinsi gani ya kuishi na kuboresha mazingira wakiwa mlimani. Siyo Lushoto tu, lakini juzi juzi nilikwenda Mwanza, watu wamejenga nyumba kuzunguka Ziwa Victoria na kwa maana hiyo ni kwamba, wao wanaliinamia Ziwa Victoria na wananchi hao wanaishi kule kwa miaka mingi vile vile.

Mheshimwa Spika, siyo huko tu, Mkoa wa Kilimanjaro kule Usangi, Milima ya Upare, wananchi wanaishi milimani miaka na miaka, huwezi ukasema utawahamisha kule kwa sababu wako kwenye milima, haiwezekani. Kikubwa ni kuwaambia jinsi gani ya kuboresha milima. Twende Songea, sehemu za Mbinga watu wanakaa milimani, wanapanda kahawa ambapo ni zao kuu katika mazao ya Tanzania. Ukiwahamisha kule maana yake ni sawa na kusema kwamba zao la kahawa tayari tumekwisha kuliua. Kwa hiyo, wananachi hao waacheni kule milimani, lakini waelimishwe jinsi ya kuboresha mazingira, wakati huo huo wakilima mazao ambayo yanaweza kuisaidia nchi hii.

Mheshimiwa Spika, si huko tu, Mbeya ambako Mheshimiwa Waziri wa Mazingira ndiko anakoishi, kuna sehemu za kuzunguka Ziwa Nyasa, ule upande wa Kyela, Tukuyu, Chunya na Milima ya kuzunguka Mbeya Mjini, watu wanaishi kule Mbeya Mjini. Mimi nimekaa pale, nimefanya kazi Hospitali ya Rufaa Mbeya na nimewahi kwenda kule juu milimani, watu wanaishi milimani. Kwa hiyo, tunapowahamisha watu, tusiweke milima kama ndio kigezo, kigezo ni jinsi gani ya kuboresha mazingira wakati huo huo wananchi hawa wakiendelea kuishi katika milima yao.

Mheshimiwa Spika, kuna dhana kwamba, Mji wa Dar es salaam maji yake yote yanatoka Morogoro. Ni kweli sehemu kubwa ya maji ya Dar es salaam yanatoka Morogoro. Lakini, watu hawajui jiografia ya Morogoro. Morogoro ni kubwa kama nilivyosema, ni kwamba inaunganisha majimbo manne. Kwa hiyo, utakuta mito mikubwa inayotoka Morogoro; uko Mto Mbezi, Mto Mvua, Mto Kisiki, Mto Mmanga na Mto Mfisigo. Mito hii yote inaenda kuunganisha na Mto wa Ruvu Juu, halafu inakwenda kuunganisha Ruvu chini. Mito hii inaanzia upande wa Morogoro Vijijini, lakini Morogoro Mjini sisi hatuna mahusiano kabisa na Mito hiyo na hatuna mahusiano kabisa na kupeleka maji ndani ya Jiji la Dar es salaam. Mto wetu ni wa Morogoro ambao unamwaga maji katika Mto wa Ngerengere ni mdogo na Mto huo asili yake unaanzia Kilosa, hauanzii Morogoro. Kwa hiyo, kuwahamisha wananchi hawa wote katika Milima ya Uluguru upande wa Manispaa kwamba ndio kigezo kwa ajili ya kuboresha mazingira, huo ni upotofu na ni kutojua mazingira na jiografia ya Morogoro Mjini.

Mheshimiwa Spika, naomba wananchi hawa wa Morogoro wameishi miaka 200 iliyopita, kwanza mazingira siyo dharura, mazingira ni kitu kinachokwenda pole pole, ingelikuwa ni dharura, kwa miaka 200 waliyokaa kule, sasa hivi kusingekuwa na mti hata mmoja wala kusingekuwa na maji. Maana yake ni kwamba, watu hawa wameishi kwa miaka mingi na wakati huo huo wakiwa wanalima, wamejenga na kuishi. Kikubwa ni kuwaelimisha wasijenge nyumba kandokando ya vyanzo vya maji au kulima mashamba kandokando ya vyanzo vya maji na pia wasiingie kwenye misitu ya asili na hili wanalijua.

Mheshimiwa Spika, watu waliochangia katika kuchafua mazingira haya ni Serikali yenyewe, kwa maana ya Watendaji wa Idara ya Misitu, wametoa vibali vingi sana vya kukata misitu kwenye Milima ya Uluguru. Kama mnavyofahamu, sisi Waluguru hatuna *hobby* wala hatuna ujuzi wa kutengeneza fenicha, isipokuwa ni wageni wanaokuja Morogoro, kwa mfano, watu wanaotoka Iringa (Wahehe), ndio waliopewa vibali vya kukata miti. Sasa tusipewe adhabu sisi watu wa Morogoro ambao hatutoi vibali vya kukata miti.

Mheshimiwa Spika, la pili, hizi *NGOs* ambazo zimejiingiza kwa kigezo cha kufikiria kwamba wanaboresha mazingira, nazo zinasaidia sana katika kuchafua mazingira kwa sababu hazina wataalam. Kwa vile hazina wataalam, wanapanda miti mingine ambayo inakausha maji badala ya kuboresha maji. Nafikiri katika suala la kuboresha mazingira, ingekuwa vizuri wataalam wa misitu wangewashirikisha wananchi ili wajue miti bora, ambayo inaweza kupandwa kule milimani inayoboresha maji. Sisi tunayo miti ya asili ambayo inaboresha maji kule Morogoro inaitwa mikuyu na kuna misumba. Ukipanda inaboresha maji badala ya kukausha. Hizi *NGOs* zimepanda miti kule inaitwa mikaratusi maelefu kwa maelfu, ambayo inakausha maji badala ya kuongeza. Kwa hiyo, kama kuna wataalam wa misitu wanaonisikiliza, hii miti inayokausha maji ing'olewe yote au ikatwe yote, tupande miti ambayo itaboresha maji ili kwenye Milima ya Uluguru kusiwe na ukame.

Mheshimiwa Spika, hilo ndio ombi langu. Ninaomba wataalam wanaohusika katika suala la mazingira, akiwemo Waziri wa Mazingira, walizingatie sana hili, wasije wakadhani kwamba wananchi wa Morogoro labda pengine wanapinga suala la mazingira. Sisi hatupingi suala la mazingira, tunaamini kabisa mazingira ni uhai, lakini jinsi gani ya utekelezaji wa suala hili la mazingira, ndicho kigezo muhimu. Naomba wataalam wakifika Morogoro, waungane na sisi wawakilishi wa wananchi, kwa pamoja tusaidiane kupeana mawazo. Imeonekana mara nyingi tu wataalam hawa wakija Morogoro, wanakuwa wanafanya vikao wao wenyewe bila hata kutujulisha sisi wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Muungano ikiwa ni pamoja na Mazingira. Baada ya kusema hayo, nasema kwamba, naunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia moja, lakini naomba haya niliyozungumza yazingatiwe kwa asilimia 100, isije ikaonekana kwamba wananchi wa Morogoro tuna ubishi. Kama suala la kuwahamisha watu kutoka kwenye milima, basi watu wanasema *charity begins at home*. Kwa hiyo, Waziri angeanzia

nyumbani kwake kuwahamisha wananachi walio katika Milima ya Mbeya, halafu ahamie Morogoro. Kidumu Chama cha Mapinduzi. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nibuka, usifanye utani. Hatuzungumzi mambo ya chama hapa, siyo vizuri hata kidogo na sitasita kuchukua hatua za nidhamu. *(Makofi)*

**MHE. DR. OMARY M. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, naomba radhi, lakini ilikuwa ni jazba tu kwa sababu ya shida iliyonikuta. Ahsante sana.

**SPIKA:** Basi, jazba itakuponza hiyo. *(Makofi)*

**MHE. SAMEER I. LOTTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa, nataka kutoa pole kwa wafiwa wote waliopata ajali zote zilizozungumziwa. Lakini nataka pole hizi zaidi zimfikie jirani yangu, Ndugu Njohole, ambaye alipoteza watoto wawili katika ajali ya basi huko Singida. Nitakapoenda Morogoro, nitakwenda kumwona.

Mheshimiwa Spika, nataka niende moja kwa moja kwenye mada iliyonisimamisha hapa, hii aliyoiongelea Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka ya kuteremshwa watu milimani. Mimi nilishawahi kuitwa kwenye vikao husika vya chama tukaonywa kwamba, tusiwe tunakemea au tusiwe tunakwamisha mipango ya Serikali ya kushusha watu milimani. Sisi hatuna matatizo na watu kushuka milimani, nasema sina matatizo na watu kushuka milimani, isipokuwa kauli zinapishana. Rais alipokuja kwetu Morogoro, alisema watu watashuka milimani, lakini wataandaliwa mahali pa kwenda na kulipwa fidia, maandalizi yatakuwa tayari, watateremshwa watapelekwa sehemu husika. Hakuna maandalizi yoyote yaliyofanywa, watu wanateremshwa, wanalazimishwa wateremshwe, wanapewa siku mpaka tarehe fulani muwe mmeshashuka, hiyo ni amri ya Waziri Mkuu. Sasa, Waziri Mkuu analeta taarifa zake, Rais analeta taarifa zake; tujue nini cha kufanya?

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema mwenzangu, vikao vya maamuzi vinavyofanyika vya Mkoa, sisi hatushirikishwi, tunaambiwa tu kwamba haya ndiyo yameamriwa. Waziri husika anakuja Morogoro, anakutana na *RC* na *DCs* wake wanasisitiza watu washuke huko milimani, sisi hatushirikishwi. Waziri anapiga simu bwana sisi tunakwenda, ukitaka kuja uje. Katibu wa Waziri huwa ananipigia, nashukuru kwa hilo, lakini katika vikao vya maamuzi hatushirikishwi. Nataka kujua kwa nini hatushirikishwi na sisi ni wawakilishi wa wale watu?

Mheshimiwa Spika, pendekezo nililowahi kulitoa kabla na bado nalisisitizia ni kwamba, tatizo si kushushwa milimani, watu wapewe elimu kama alivyoongea kaka yangu hapa kwamba, badala ya kung'ang'ania kuwaambia watu washuke, wapewe elimu, wapewe taarifa wapande miti ya matunda. Miti ya matunda itawanufaisha kwa kipato, lakini itahifadhi mazingira pia. Kwa wale ambao wanataka kupanda mazao ya muda mfupi kama mahindi, mananasi na kadhalika, wao wanaweza wakateremka. Lakini kule juu bado kubakie chini ya himaya yao. Kama wakiondoka wao ina maana Serikali itakuwa na gharama kubwa zaidi ya kuhakikisha inapanda miti kule na kuanza kuhifadhi

mazingira wakati wananchi wanaweza wakafanya kama watakuwa wamepewa elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, narudia tena, katikati hapo tulibahataika kwenda Ngorongoro ndani ya Hifadhi chini tukakuta wafugaji na ng'ombe wamo ndani ya Hifadhi. Wale hawachukuliwi hatua yoyote, wananchi wa Morogoro wanaambiwa wateremke! Matambiko yao wayaache! Wako hapo nimewakuta na ninaamini nikiondoka nitawaacha hapo hapo. Nasema kwa nini kuwe na matabaka na maamuzi yanayopishana? Nilibahatika kwenda Kilimanjaro kwa Ndugu yangu, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, yuko juu kabisa kwenye geti la kuingia katika Hifadhi, lakini yuko kwenye mlima kule juu; kwa nini watu wa kule wasishuke washuke watu wa Morogoro tu? Kwa hiyo, naomba tutoe ufafanuzi. Nimekwenda Lushoto, nimekuta Hoteli ya Kiongozi mmoja Mkuu wa Nchi, imejenga kule juu kabisa milimani; kwa nini wasishuke wale washuke watu wa Morogoro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ananikumbushia tena kwamba *charity begins at home.* Mimi ninachoomba, vikao vya maamuzi vinapokaa tushirikishwe. Sisi tunawakilisha wananchi, wanatusikiliza, wanasikitika na vikao vya maamuzi hatushirikishwi, amri zinatolewa. Sisi tunaomba tuwe tunashirikishwa kwenye vikao hivyo.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, nitapenda kuongelea suala la Kyoto. Sisi tunavyofahamu ni kwamba, nchi hizi zinazozalisha gesi ziwe zinatupa ruzuku, lakini mpaka sasa hivi nchi nyingi hasa Marekani ambayo ndiyo inazalisha zaidi gesi, inakataa kuingia katika Mkataba huu. Je, sisi kama wazalishaji wa *oxygen* tunakuwa na msimamo gani katika hili?

Mheshimiwa Spika, kwa hayo mawili na kwa muda wako, ahsante sana. Naomba wananchi wangu wanaonisikiliza, niwatolee kauli kwamba mimi nitapigana kufa na kupona kuhakikisha kwamba, nabakia na kama kuhamishwa, basi maandalizi yafanywe kama alivyoongea Rais. Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumekwisha kamilisha orodha ya wale walioomba kuchangia na sasa hivi natoa taarifa kwamba, saa 11.00 jioni tutaanza kupokea majibu ya hoja kutoka kwa Waheshimiwa Mawaziri wawili, nusu saa kila mmoja. Waziri wa Mambo ya Muungano na Waziri anayeshughulikia masuala ya Mazingira. Baada ya hapo basi ndiyo tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi.

Kwa kuwa muda uliosalia hautoshi kuendelea na jambo lolote na shughuli iliyokuwa inafuata ni kuanza kusikiliza majibu ya hoja ambayo sasa Mawaziri wataanza saa 11.00 jioni, basi nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.47 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaahirisha kikao cha asubuhi tulisema tutakapoingia tutawaita watoa hoja, lakini tunayo nafasi ya kumwita Kanali Saleh Ali Farrah, aweze kuchangia kabla ya watoa hoja.

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na mimi kwa kunipatia nafasi *adhuhuri* ya leo, kujaribu kuchangia hoja ya Makamu wa Rais upande wa Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi vile vile kutoa rambirambi zangu kwa misiba yote iliyotokea ndani ya Bunge tukiwako hapa, Mwenyezi Mungu awasaidie na awape subira wote waliopatwa na matatizo hayo. Baada ya hapo kabla sijasahau, mimi ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina furaha na mimi kupata hii nafasi niweze kuchangia mawazo kidogo na kusema yale ninayoyafahamu ikiwa ni changamoto katika mchango huu. Zanzibar ni visiwa na tena visiwa vyenyewe viko 25. Zanzibar ni finyu, imezungukwa na maji na ukanda wa mawe, kwa hiyo, ardhi ya kulima ni finyu mno. Zanzibar inategemea sana vitu kadhaa ambavyo viko vingine vya asili na vingine ambavyo tumejaribu kuvikuza. Utakuta Zanzibar asili yake ina uchumi mdogo sana wa nazi na karafuu. Lakini vile vile Zanzibar ina bandari na mapema bandari hii ilishakuwa ni changamoto katika kukuza uchumi kwa nchi yetu.

Sasa nimesimama hapa kwanza kuizungumzia bandari hii na nimesimama vile vile kujaribu kusema ya kwamba, ndani ya Muungano huu, Zanzibar lazima ionekane kwamba sasa hivi ina chechemea, uchumi ni mdogo, watu tumeongezeka. Tukija kulinganisha ni karibu 1/36 Zanzibar ina watu milioni 1.1 *where as* Tanzania Bara ina milioni 36 ukijumlisha zinakuwa milioni 37. Kwa hiyo, utaangalia hapa jinsi kipato kinavyoweza kupatikana kwa upande wa Zanzibar, ndiyo utaweza kuamini ya kwamba, kwa kweli kipato chetu ni kidogo. Nakumbuka mimi kunako mwaka 1950 nikiwa mdogo, nilipokuwa napata historia niliambiwa wakati huo tulikuwa watu 350,000. Hebu angalia jinsi tulivyoweza kuongezeka, wakati huo tulikuwa watu 350,000 lakini bado uchumi wa Zanzibar ulikuwa unategemea bandari na *services* ndogo ndogo.

Kwa hiyo, nilichokuwa najaribu kusema ndani ya Muungano huu, najaribu kushauri jinsi tunavyoendelea kuchechemea, Serikali ya Muungano iweze kusaidia uchumi wa Zanzibar ili tuweze kusonga mbele. Kwa mfano, Zanzibar hii tukiitazama historia yake, Zanzibar inajulikana tokea karne ya tano, imeanza kuchanganyikiwa tokea karne ya tisa na kumi na imeanza kutawaliwa tokea karne ya 15. Ina maana Wareno na Waarabu wametutawala karibu kunako miaka 350. Lakini hapa ni katika miaka 300 tu ndiyo tulikuwa tunategemea karafuu na nazi.

Kwa kweli hali ya Zanzibar ilikuwa mbaya sana. Hatukuwa na namna nyingine ya kuweza kupata changamoto ya kuongeza kipato isipokuwa kufikiria bandari. Ninashukuru ya kwamba, ukitazama historia ya Zanzibar, bandari ambayo ilitangazwa

mwaka 1995 wakati wa awamu ya sita, ilitangazwa kuwa bandari huru. Hii bandari huru ilitangazwa mwaka 1895, ilikuwa tayari ni karne moja. Nataka kuisema hiyo, karne moja ni miaka 100 ya sisi kuwa na bandari na kuendeleza uchumi wetu. Kwa hiyo, nilichokuwa najaribu kukisema ni kujaribu kulinganisha. Miaka 100 ya kuwa na bandari si mingi na ni kama itakuwa haijaleta tija yoyote.

Sasa katika mipango ya Serikali ya Muungano wanajaribu kutengeneza Bandari ya Bagamoyo. Nilikuwa naomba isimamishwe Bandari Bagamoyo, itengenezwe treni itakayotoa vitu Bagamoyo kwenda sehemu nyingine, lakini nilikuwa na wazo ya kwamba, Bandari ya Bagamoyo isingekuwa huru, hapo itakuwa Zanzibar imekatwa miguu kabisa. Kwa sababu kama Serikali ya Muungano haikusaidia miundombinu ya Zanzibar ambayo sasa hivi tunachechemea, kama Serikali ya Muungano haikuweza kusaidia elimu ambayo vilevile nayo tunachechemea, kwa kweli itakuja kuwa tabu, wananchi watalalamika vibaya sana. Kwa hiyo, nilichokuwa najaribu kusema kwa upande wa bandari, nashauri bandari huru ibaki Zanzibar ili iweze kuleta *income* kwa wananchi na bBndari ya Bagamoyo iwe bandari kama kawaida, sisi tuweze kupata nafasi ya kutoa vitu nje. Hili ndilo la kwanza ambalo nilikuwa najaribu kulitolea mawazo na kulisemea.

Pili, Muungano tunao muda mrefu zaidi ya miaka 40 lakini bado sisi tumejikita katika Wizara zilezile ambazo zipo za Muungano tu na zaidi ya hapo katika hizo hizo Wizara za Muungano, kuna migogoro na matatizo. Kwa mfano, ndani ya Bunge hili swali lilijibiwa *National Service* haiko katika Muungano, ukitazama suala la namna hiyo bado ni gumu na lina muda mrefu kuliko umri wangu wote niliofanya kazi jeshini. Mimi nimekuja kulisikia hapa. Nilikuwa naamini ya kwamba ni Wizara ya Muungano na kweli nasema ni Wizara ya Muungano, kwa sababu unajua *theory* na *practical* ni vitu vya *out* lakini *practical* inaendeshwa na *theory*. Ninavyoelewa mimi ndani ya Muungano huu kama nchi imeunganisha dola, jeshi limekuwa moja, kama nchi imeunganisha dola vyombo vya Serikali vimekuwa vya aina moja ikapiga hatua ikaenda kwenye chama nacho wakati huo kikawa ni chama kimoja cha CCM, kwa kweli nchi hiyo imeunganika na ni tabu kuporomoka. Ni *total union,* kwa vyovyote vile itakavyokuwa ni *total union,* yaani Muungano kamili. Sasa ikawa Muungano kamili basi mimi nilichokuwa nashauri, suala lililojitokeza hapa ndani ya Bunge hili kuhusu *National Service* iunganishwe mara moja na ipunguze kero hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar tunachechemea kielimu, tunazo shule mimi ndiko nilikosoma huko mpaka kufikia kiwango hiki, lakini utakuta bado tuna matatizo ya kuweza kuwa na elimu iliyokuwa sawa na Tanzania Bara au kupanda juu. Humu ndani ya Bunge nimekuja kusikia tulikuwa tunajaribu kukimbilia sana na kuomba nafasi za kuweza kuingia *University* mpaka tukaomba *quarter,* kwa sababu kiwango chetu hakipandi juu au hakijapanda juu. Licha ya kuwa sisi ni wasomi, shule kule zimeanza zamani sana lakini utakuta elimu inatuletea matatizo jinsi ya kuipanga na kuweza kuinyanyua. Naamini kwa kweli kama shule za Zanzibar hazijakuwa na mabweni watoto wakasoma, tutakuwa na tabu kukinyanyua kiwango cha elimu kwa kiwango cha kimataifa kinachotakiwa. Sasa hivi karibu Rwanda na Burundi inaingia, Uganda na Kenya inaingia, suala hili nilikuwa naliona naliogopa zaidi na sikuweza kulisema pale

Zanzibar wakati nikisimama katika mikutano. Mtaniwia radhi kama nitakosea, sisi Wazanzibari tutakuwa ni watumwa kwa sababu tutakuwa tunatumika hatutafikia kiwango cha kuweza kupata elimu sawa sawa.

Naishauri Wizara ya Elimu iwe ya Muungano. Mimi sijaona ya kwamba tunaungana juu halafu chini huku kunabaki kuna *vacuum* au kunabakia kweupe, ni vyema Wizara nzima ya Elimu ingekuwa ni Wizara ya Muungano.

La mwisho ambalo nataka niliseme ni kuwa ndani ya Muungano kuna kero nyingi, kuna kero ya asilimia 4.5 na kuna kero ya bandari. Hii kero ya bandari kwa kweli mimi nilikuwa naomba imalizike. Mheshimiwa Waziri Mkuu, akikaa pamoja na Waziri Kiongozi, wangejaribu kulimaliza suala hili kama walivyomaliza suala la *passport* ndani ya Bunge. *Passport* ilipigiwa kelele humu ndani ya Bunge, nakumbuka nikiwa mwanajeshi likamalizika mara moja, ikawa hakuna kusafiri kwa *passport* baina ya Zanzibar na Dar es Salaam au Dar es Salaam kwenda Zanzibar. Kwa hiyo, suala hili lingetolewa maelezo likaweza kumalizika mara moja ili tupunguze hizi kero. Kero zinakuja wakati wa bugudha zinazidi na wananchi wanalalamika kiasi ya kwamba, hawawezi kuvumilia. Lakini kwangu si tabu kwa sababu kwenye maisha ya kila siku, hata ukikaa na mkeo ndani ya nyumba, mnakuwa na matatizo lakini mnatafuta *solution.* Mnatafuta ni jinsi gain mtafanya ili muweze kutanzua tatizo hilo. Kwa hiyo, hili naliomba lifikiriwe na tulizungumzie liweze kupata ufumbuzi.

La mwisho kabisa kabla kengele haijanigongea, Bunge naliona halifanyi kazi zake kama Bunge, kwa sababu naona hakuna vikao vya Muungano au mambo ya Muungano yanayoletwa ndani ya Bunge na kuzungumzwa kama unavyoletwa Muswada. Kwa kweli hiki chombo wananchi wangepaswa kusikilizwa na ninajaribu kusema kweli, hili lingeleta msisimko kama inavyoleta msisimko bajeti. Kwa sababu masuala yote yangezungumzwa hapa yangesikika na baadaye yakapatiwa uamuzi kila kitu kinaonekana kinakwenda. Hili suala la kero lingeisha.

Kwa hiyo, bado tunawategemea viongozi wetu na mimi nilikuwa natoa ushauri ya kwamba, wakishakaa kitako wakishaibua Muswada ukija hapa mbele tukikaa tunaweza tukalizungumza vizuri, kati ya mikutano yetu tuchague vikao kadhaa ili tuweze kuzungumza juu ya masuala ya Muungano. Sasa Bunge hili halizungumzi Muungano, tunaogopa nini mpaka inakuwa namna hiyo? Naona tunawanyima wananchi haki yao kuweza kujua sisi tunawawakilisha kiasi gani ndani ya Bunge hili. Kwa hiyo, suala hili naomba kama litakuwa limepata ridhaa ya ukumbi huu, liwekwe katika majaribio ili tuweze kuona matokeo yake yatakuwa namna gani. *(Makofi)*

Kwa leo nilikuwa nina machache ya kuzungumza, ninasema tena kwa mara ya pili ninaunga mkono hoja na ninaomba ushauri nilioutoa vile vile uzingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote katika Ofisi ya Makamu wa Rais kwa shughuli nzuri wazipangazo kila siku katika Wizara zao. Aidha, nawapongeza wataalamu wote waliomo katika Wizara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwimba na Wilaya ya Kwimba kwa jumla kwa viongozi wote kutoka Wizara hii waliobarikiwa na Mwenyezi Mungu kupata fursa ya kutembelea Kwimba na hususani Jimbo la Kwimba viongozi wakuu waliopata fursa hii ni Mheshimiwa Makamu wa Rais. Tunashukuru sana kwa elimu aliyotupa juu ya mazingira elimu hiyo imekuwa msingi wa juhudi zetu kuendeleza juu ya ustawi na maendeleo ya mazingira bora katika Wilaya yetu, tunamshukuru sana.

Kiongozi mwingine ni Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira. Tunamshukuru na kumpongeza kwa kutenga siku nzima Wilayani kwetu tena katika majimbo yote mawili Kwimba na Sumve na kufanikiwa kutembelea maeneo kadhaa shule za sekondari na msingi zikiwemo!

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza na kumshukuru sana kwa muda huo alioutenga kwa ajili ya kujionea kuelewa mazingira ya Kwimba na kutoa ushauri wake wa dhati, ushauri wake pia tumeuzingatia na kama alivyoomba shule zote zisitambuliwe kwa majengo na mabati bali kwa misitu inayozizunguka.

Hivi sasa shule zote zitakuwa katika mashindano ya shule kujificha katika misitu. Naamini muda si mrefu shule zetu zote hazitakuwa zikionekana kwa mbali kwa majengo na mabati ni kutokana na ziara za viongozi hao. Wilaya imehamasika kubaini vyanzo katika kila kijiji na kushindanisha vijiji hivyo kulinda vyanzo vyake.

Ombi langu pamoja na matatizo mbalimbali viongozi hawa waliyoyapata yakiwemo ya kutokuwakuta Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo hususani ziara ya Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na ubovu wa barabara, wasivunjike moyo, wapange ziara tena Wilayani na Jimboni Kwimba, ili waje wataamini matokeo ya ziara zao na kutoa elimu mpya na maelekezo mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuimarisha kuaminiana ndani ya Muungano, hata hivyo mimi binafsi bado naendelea kutoa ushauri kama niliyoutoa mwaka jana katika Bajeti kama hii. Natoa ushauri huo nikiamini kuwa bado ni ushauri muafaka kama utakubalika, ombi langu la muda mrefu ni kuziomba Serikali hizi mbili ya Mapinduzi Zanzibar na ya Muungano zikae na ziangalie uwezekano wa kuziunganisha Serikali hizi ili tuwe na Serikali moja. Kwa kuona kwangu nchi hii kwa muda mrefu sasa ni moja na Serikali ni moja tu. Serikali mbili kwangu mimi ni dhana tu na ninaamini ikiwa itatangazwa Serikali moja hakutakuwa na athari yoyote inayofikiriwa na baadhi.

Kwa imani yangu hii itaondoa hata hizi zinazosemwa kero za Muungano. Kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukiongozwa na Rais mmoja bila madhara. Watanzania bora wanaongoza kama Rais nchi hii bila taabu, Wazanzibari (Tanzania Visiwani) vivyo

hivyo kuna hofu zipi ziletwazo na Serikali moja mbona mipaka kati ya Bara na Visiwani wananchi hawaioni? Mbona wananchi hawana wasiwasi huo? Je, viongozi wana wasiwasi wowote? Sidhani hofu chanzo chake hoja kiko wapi? Iseme iwe wazi ili kama ni ya kweli tuione kama haina ufumbuzi. Naunga mkono hoja.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Makamu wa Rais kwa kazi nzuri ya kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais katika majukumu yake ya kuongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia Mawaziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais wanaoshughulikia Mazingira na masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu, imefafanua vyema kuhusu hatua mbalimbali zinazochukuliwa katika kutatua kero za Muungano. Hata hivyo, baadhi ya wananchi wanajiuliza maswali mbalimbali kuhusu kero hizo kwamba je, kero hizo ziko upande wa Tanzania Zanzibar tu? Je, mgao huo wa 4.5% unaozungumziwa kwamba hauridhishi unazingatia vigezo gani kama eneo, idadi ya watu? Je, kuna tofauti gani kati ya masuala ya Muungano na masuala yenye sura ya Kitaifa? Kwa nini Bajeti ya Serikali ya Muungano inachangia Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar?

Kuhusu mazingira, napongeza juhudi zote zinazofanywa na Shirika la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* chini ya usimamizi wa Ofisi ya Makamu wa Rais. Shirika hili linabeba jukumu kubwa la kusimamia sheria ya mazingira ya mwaka 2004 hivyo inahitaji kujengewa uwezo wa kuweza kufanikisha jukumu hilo. Mazingira ya ofisi za shirika hili hayaridhishi kuna umuhimu wa Serikali kulisaidia shirika.

Kwa vile nchi yetu ni kubwa ni vyema *NEMC* kuwa na matawi angalau Kikanda kwa vile Halmashauri za Wilaya na Miji hazina wataalamu wa mazingira wanaotosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *EIA*. *EIA* hufanywa kabla miradi haijaanza lakini baada ya mradi kuanza na kumalizia hakuna ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa uharibifu uliojitokeza umedhibitiwa. Kwa mfano tunaona mashimo makubwa yaliyochimbwa baada ya kutoa changarawe/kifusi yakiachwa bila kufukiwa baada ya kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais ndiyo inaratibu masuala yote ya mazingira ambayo ni mtambuka. Mazingira na suala pana lakini nyeti sana hivyo ni vyema Serikali ikaiwezesha ili iweze kumudu jukumu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichangie kwenye Wizara ya Mazingira, na nitaanza kwenye mifuko ya kufungia bidhaa kutoka madukani kwa umaarufu inaitwa mifuko ya *rambo.* Mifuko hii hakuna ubishi juu ya athari zake za kuharibu mazingira. Mifuko hii haiyayuki ukiichoma hata ukaizika

chini. Sehemu inayotupwa mifuko hii, halafu sehemu hiyo akatokea mtu akajenga basi tunaambiwa kwamba nyumba hiyo iliyojengwa kwenye jalala ambalo lina mifuko hiyo nyumba inaweza kupasuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshaona wanawake wengine wanapowasha moto wanatumia mifuko hiyo ili kufanya moto uwake. Wakati mfuko huo ukishika moto basi huwa unatoa moshi mzito na husababisha waliopo karibu kukohoa. Je, tumeshafanya utafiti wa kuona athari ya moshi huo kimazingira na pia athari ya moshi huo kwa binadamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshawahi kutembelea mkoa wa Iringa na uongozi wa mkoa huo wamepiga marufuku mifuko hiyo kutumika mkoa wa Iringa na utautafuta wa dawa huupati. Je, inamaana Serikali nzima imeshindwa kupiga marufuku mfuko huo?

Mheshimiwa Naibu Spika au kuna maslahi ya mkubwa fulani katika kiwanda cha mifuko hiyo? Naomba majibu ya hilo tu maana Muungano umeshaongelewa na wengine. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niungane na wenzangu wote waliosimama kuchangia hotuba hii. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie suala la ujenzi wa Ikulu ya Wete iliyoko Mkoa wa Kaskazini Pemba ambayo hili ni jengo la Jamhuri ya Muungano. Hii sio mara ya kwanza kuchangia jambo hili lakini imenibidi nilikumbushie tena kwani nilihisi kuwa kwa vile nimelizungumza muda mrefu huenda likawekwa katika Bajeti hii ya mwaka 2007/2008 hasa kwa vile halikuzungumzwa katika Bajeti ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kuwa Serikali katika Bajeti hii imepanga kulijenga jengo hili lakini haikuona umuhimu wa kuliainisha kwa sura nyepesi katika Bajeti hii ili kusiwepo na majadiliano marefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kwa unyenyekevu mkubwa kulifikiria jengo hili kwani sasa limezidi kuharibika hata maji ya mvua yanaingia ndani kutokana na mipasuko iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba naomba Serikali itakapoamua na itakapokuwa tayari kuanza ujenzi wa jengo hili itumie wakandarasi kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwani kuna tetesi kuwa huenda kazi hii kuwa watakabidhiwa vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hivyo naomba sana kuwa kazi hii wapewe vikosi vya Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa wakati wowote Mheshimiwa Rais atakapofanya ziara Mkoani humo italeta aibu kubwa ndani ya Mkoa huo kwa sababu

hatuna hata sehemu ya kumkaribishia na hiyo sio aibu ya Mkoa tu ni aibu hata kwa Serikali ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais upande wa Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo kubwa la uharibifu wa vyanzo vya maji hali ambayo inasababishwa na uharibifu wa mazingira. Ni dhahiri Wizara inayohusika imefanya juhudi kubwa za kuhakikisha mazingira yanayotunzwa kwa kuwahamasisha wananchi kwa kutumia vikundi na taasisi zisizo za Kiserikali. Hata hivyo wapo watu ambao husababisha uharibifu huo kwa makusudi mazima kwa mfano, uchomaji moto misitu pamoja na kulima kwenye vyanzo vya maji. Bado nadhani inaweza kuwa tiba endapo Wizara itaandaa semina kwa nchi nzima kwa maana ya kuwatuma Maafisa kufanya kazi hiyo ili iwe elimu kwa wananchi.

Pili, wakati semina hiyo ikiendeshwa ni vema ikaeleweka kwamba watakaobainika kukiuka watachukuliwa hatua za kisheria. Hapa ina maana itungwe sheria kali kwa wakiukaji na waharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iwe na usimamizi mkali kwa vile vikundi na taasisi zisizo za Kiserikali zinazopewa fedha za mazingira na kuzitumia visivyo. Kwa maana nyingine ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za mazingira, kabla ya kupewa fedha hizo ni vema kupitia kwa makini nia ya mradi na pia kukaguliwa mara kwa mara kwa kuhusisha uongozi wa Wilaya. Ina maana fedha za mazingira zifahamike Kiwilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ufanisi mkubwa katika Taifa letu akisaidiwa na Mheshimiwa Dr. Hussein ALI Mwinyi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ambao pia nawapongeza kwa pamoja kwa utendaji wao mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina yaliyomo katika hotuba ya mwaka 2007/2008 yanaridhisha sana na kwa hiyo, naanza kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi nianze mchango wangu kwa kumpongeza sana na kumshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, kwa kutembelea maeneo mbalimbali nchini yaliyokumbwa na mafuriko wakati wa mvua za masika mwaka 2006 na kuwafariji wananchi walioathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mikumi kwa jumla na hususan katika Kata ya Kidodi ninamshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa ziara yake kwetu na kwa msaada wa fedha jumla ya shilingi 8,000,000 alizotoa kwa wananchi katika Kijiji cha Ruaha ambao nyumba zao zilibomolewa kabisa na mafuriko na kusababisha kifo cha mtu mmoja. Fedha hizi zimepangwa kuwahamisha na kusaidia ujenzi wa nyumba nyingine katika eneo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa ya Serikali kukabiliana na kudhibiti sababu zinazoharibu mazingira, baadhi ya maeneo nchini yamekumbwa na uharibifu wa kudumu hasa baadhi ya mito mikubwa kubadili kabisa njia asilia za kutiririsha maji mfano wa maeneo haya ni Vijiji vya Ruaha, Mhenda, Mikumi, Tindiga, Mabwerebwere na Malangali, jirani na Kilosa. Kubadili njia kwa mito katika Vijiji hivyo kunasababisha kujirudia mafuriko makubwa kila mwaka na kuleta uharibifu wa kubomoa nyumba, kuharibu kwa kusomba mazao na kuharibu miundombinu muhimu, hususan barabara. Uharibifu mkubwa na hasara kubwa zinawaongezea wananchi umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Serikali ieleze itatumia njia zipi mapema iwezekanavyo ili kuirudisha mikondo ya mito iliyosambaratika katika Vijiji tajwa ili irejee katika njia mbadala za kudumu ili kuepuka mafuriko kujirudia kila mwaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani na matumaini kuwa Serikali italipa uzito unaostahili tatizo hili. Narudia kuiunga mkono hoja hii.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua ambazo zinachukuliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Kiongozi bado utatuzi wa kero za Muungano hauendi kwa kasi kwani vikao vitatu kwa mwaka havitoshi. Kama vinatosha, je, ni kero ngapi zilizotatuliwa na kupatiwa ufumbuzi wa kudumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kufahamu lile gawio la asilimia 4.5 kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni hatua gani zilizochukuliwa kwani inaonekana kwa shilingi 27,338,623,000 ni ile ile 4.5%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Zanzibar ni nchi ambayo ina Serikali yake na hali yake ya uchumi ni duni, ni budi kuiangalia kwa jicho la huruma na kuiwezesha kupata misaada yake wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Zanzibar ni Kisiwa ambacho kimezungukwa na bahari, basi ile asilimia 20 itokanayo na uvuvi katika Bahari Kuu, gawio liwe kama ilivyopangwa.

Napenda kuipongeza Tume ya Haki za Binadamu kuweza kufanya kazi zake Zanzibar, kwani Tume hiyo kufanya kazi Zanzibar kutapunguza malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mifuko ya plastiki nalo bado linaendelea kuchafua mazingira kwani bado ipo na inaendelea kuchafua mazingira. Ni vema hatua za ziada zikachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ukataji wa miti ovyo nalo bado linaendelea kuchafua mazingira kwani ile kauli mbiu ya kata mti, panda mti haichukuliwi hivyo miti inakatwa na mingine haipandwi, hivyo basi tunakaribisha jangwa, hivyo ni budi kupanda miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati mbadala ya kuni bado haijapatikana kwa hiyo mkaa unaendelea kuwa nishati ambayo inatumiwa na wengi hivyo miti itakatwa kwa hivyo tutafute nishati mbadala ili kulinda mazingira yetu. Ahsante.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kutoa pole kwa familia ya Mzee Hamis Chifupa kwa kuondokewa na mtoto wao na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Amina Chifupa. Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naanza kutoa mchango wangu. Mambo yanayohusu Serikali ya Muungano na Zanzibar yana vipengele visivyopungua arobaini. Mpaka hivi sasa ni vipengele vingapi kati ya hivyo vilivyotekelezwa na vingapi havijatekelezwa. Tunaomba kero zote za Muungano zishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wabunge tunaotoka Pemba, kama Rais wa Muungano akija katika Kisiwa cha Pemba sisi huwa hatushirikishwi katika ziara zake wala hatupati mwaliko wowote, kwa nini na ukiangalia sisi ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri, kwa kweli usafiri unatupa shida sana katika Kisiwa cha Pemba kwa sababu hizi zifuatazo:-

Kwanza, naanza kwa bandari ya Wete. Gati iliyopo katika bandari hiyo ni mbovu na ni ndogo haiwezi kuchukua meli kubwa hata meli zetu za hapa Tanzania kama *MV Mapinduzi, Sepideh* na nyingine nyingi, kutokana na udogo na ubovu. Kwa hiyo, tunaomba Serikali zote mbili ziangalie suala hilo kwa kuwa wasafiri wanaotumia bandari hiyo ni wengi kutoka Tanga – Dar es Salaam – Zanzibar na ni meli mbili tu zinafika bandarini ambazo ni Aziza na Mudathir pekee na ni mpaka maji yajae ndio meli hiyo ifunge gati, ikiwa maji hamna wasafiri hubaki nje mpaka maji yajae. Je, ni lini itafirikiriwa kujengwa? Pia na bandari ya Mkoani, tunaomba ikarabatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Karume Airport,* Pemba. Uwanja huo, sasa ni mashimo matupu, ni mbovu, haufai tokea ulipojengwa mpaka leo haujakarabatiwa. Je, ni lini uwanja huo utakarabatiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirikisho la Afrika Mashariki, ukiangalia sisi wenyewe Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano tuna matatizo na bado hatujaweza kuzitatua, kuna kasoro nyingi tu. Je, leo iwaje tuungane na nchi tano wakati baadhi ya nchi hizo nazo zina migogoro ndani ya nchi zao? Je, hamuoni kuwa wataka kutuzidishia matatizo katika Taifa letu?

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujikita moja kwa moja kwenye hoja ya Mazingira. Ni dhahiri kabisa kwa mwanadamu kuonekana nadhifu, ni kutokana na mavazi. Hali kadhalika kwa ulimwengu hususani ardhi na maji na mizunguko yote ya umbile la nchi ni jinsi ambavyo hali asilia inavyolindwa na kuboreshwa na mwanadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ulinzi wa mazingira, Mungu aliumba ulimwengu vizuri na akazawadia wanadamu wawe na mamlaka kwa viumbe vingine vyote na kuendeleza vizazi vyao. Mwanadamu aliruhusiwa kutumia mimea iliyo ardhini na maji kwa manufaa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa la mwanadamu badala ya kulinda mimea hiyo huhusan miti ya asili, kasi kubwa imekuwa ni kukata miti hiyo ikiwemo mivule kwa nguvu zote na kuharibu mazingira. Pamoja na kuwepo sheria ya kutokukata miti hiyo, haifuatiliwi. Kupitia Wizara ya Mazingira, naomba sheria hii ifuatiliwe kwa karibu pamoja na Wizara Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuboresha mazingira mambo yafuatayo yazingatizwe:-

(a) Elimu ya mazingira ihimizwe shuleni toka chekechea na isisitizwe hata kwenye familia, vikao vya koo na kwenye nyumba za Ibada. Ikiwezekana iwe rasmi kuwa mtoto akizaliwa tu aoteshewe mti na aendelee kuutunza na kuongeza mingine maishani mwake.

(b) Mifuko ya plastiki ipigwe marufuku kabisa mikubwa kwa midogo ila mradi ni *malboro* na kadhalika.

(c) Kila Mkoa ufanyiwe ushindani kwa kuboresha mazingira kwa nyanja zote.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa hotuba zote mbili kuhusu Muungano na Mazingira.

Napenda niipongeze Serikali inavyofuatilia kwa makini na kwa kina masuala ya Muungano. Aidha, naipongeza Serikali pia kwa jinsi inavyosimamia kwa makini suala la mazingira. Jitihada zinaonekana, ila naishauri Serikali chini ya uimarishaji wa mazingira kwa watu binafsi, hususan tatizo liko maeneo makame kama vile Mwanza, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma na Mara. Wananchi wengi katika maeneo haya hawana habari na suala la mazingira katika maeneo yao.

Nashauri msisitizo uwekwe kwenye mazingira kwa kila Kaya na Kijiji ikiwezekana kuwe na mashindano. Wananchi wahamasishwe na kulazimishwa. Mazingira katika taasisi za Serikali kama vile shule, magereza na vyuo mbalimbali viwe ni mifano. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi atoe ushirikiano wa kutosha ili wanafunzi wanapohitimu waelewe dhana na umuhimu wa kuhifadhi mazingira.

Kuhusu mazingira katika maeneo ya machimbo, maeneo ya migodi mikubwa uharibifu wa mazingira ni mkubwa sana. *EIA* na *EMP* havifuatiliwi kiasi cha kutosha. Kwa mfano Mgodi wa Geita ni kati ya migodi inayoharibu mazingira. Imeondoa milima na kufyeka misitu yote, lakini hatuoni mahali popote wanapopanda miti. Tafadhali kuwe na ufuatiliaji wa karibu katika migodi ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kuwa kumekuwa na mgongano wa maelezo kati ya Wizara za Serikali kwa wachimbaji wadogo. Hali hii husababisha kero. Kumekuwa na utaratibu wa Wizara ya Nishati na Madini kutoa leseni ya utafiti maeneo ya misitu, wakati huo huo Wizara ya Maliasili na Utalii inaamua kuwafukuza wachimbaji kama ilivyotokea Matabe, Wilaya ya Chato. Hali hii inawafanya wananchi washindwe kuelewa amri mbili tofauti kutoka Serikali moja.

Hivi sasa kuna maombi ya wachimbaji wadogo kuruhusiwa kuendelea kuchimba eneo la Matabe. Wizara ya Nishati na Madini imekwisharidhia na imepeleka maombi hayo Wizara ya Maliasili na Utalii na ili ruhusa itoke inabidi yapitie Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ili maandalizi ya *EIA* na *EMP* yafanyike. Wakati wanasubiri uamuzi wangepelekwa askari ambao wanasababisha vurugu na mapambano kati ya wananchi na vyombo vya dola. Hali hii imetusikitisha sana. Wananchi hawa wamekuwapo muda mrefu, hata hivyo sura ya misitu haipo tena kwa wakulima, wafugaji na wachoma mkaa. Zaidi ya hapo Wizara ya Nishati na Madini imekwisha panga kuwa litakuwa eneo la wachimbaji wadogo.

Kwa maelezo hayo naiomba Serikali hususan Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ichukue hatua za haraka kwenda kuangalia eneo la Matabe ili iwaruhusu au kuwaambia wachimbaji hawa kufanya kazi eneo hilo. Maombi yamekuwa ya muda mrefu. Suala la Kamishna wa Madini wanalifahamu hata Mawaziri wote wawili wa Nishati na Madini na wa Maliasili na Utalii wanalifahamu. Naomba sana idhini itolewe ili Serikali isionekane kero kwa wananchi hawa ambao ni wengi sana na wametapakaa kila mahali. Wako tayari kufuata maelekezo watakayopewa na Serikali watatoa ushirikiano wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kueleza kuwa zoezi hili la kuhamisha mifugo kwenda Ihefu halikufanyika vizuri, lilijaa uonevu na dhuluma na kuipaka tope Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nieleze kuwa maeneo mengine kama vile Biharamulo, Bukombe, Karagwe wafugaji walinyanyaswa sana na kunyang'anywa mifugo yao. Wengi wao hivi sasa hawana imani na Serikali kwa matendo waliyofanyiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Tume iliyokwenda Ihefu ni vizuri pia ifike maeneo ya Bukombe, Biharamulo na Karagwe. Kule kisingizio kikubwa kilikuwa kuwa wafugaji ni wakimbizi. Kweli hali hii haikupendeza kwa wafugaji. Baadhi ya viongozi walitumia nafasi hiyo kujinufaisha binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitishwa sana na hotuba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muungano. Hasa wanaposema wanapunjwa kiuchumi na mapato. Napenda turuhusiwe nasi tuseme tunavyoona hivi sawa Zanzibar yenye watu lati tisa kuwa na Wabunge zaidi ya 70 na Geita yenye watu laki nane kuwa na Wabunge watatu na bado kuna wawakilishi na Kata zao zote zina barabara za lami. Wanataka Zanzibar ifanane na Dar es Salaam? Waende Rufiji, Geita na kadhalika waone hali za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero ya Muungano kubwa ni kwamba tumewalea wenzetu kiasi ambacho hawaoni ukweli.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nitoe shukrani zangu kwako kwa jitihada zako ambazo zimelifanya Bunge letu kuwa kioo kwa Watanzania wote. Pia nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, kwa umahiri wake wakati akiwasilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wangu pamoja na hotuba hii kuwa inakidhi sina budi kuelezea yangu ambayo nitaomba Wizara hii inipatie majibu.

Kwa kuanza nitazungumzia Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar. Kauli ya Serikali juu ya Ofisi hii muhimu huko Zanzibar imekuwa kama hadithi. Kauli ya kupatikana eneo la kujenga ofisi hiyo imetolewa muda mrefu. Kama ni hivyo sasa ni vyema Serikali ingetupatia tarehe itakayoanza ofisi hiyo kwani Mheshimiwa Makamu wa Rais anapokwenda Zanzibar hana ofisi yake mahsusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bandari ya Kisiwa cha Pemba, mara nyingi tunapoizungimza Pemba hapa Bungeni huonekana ni siasa. Kisiwa cha Pemba ni eneo la Muungano, cha kushangaza ni kuona eneo pekee lililosahauliwa. Bandari za Pemba hazifai, Bandari iliyojengwa Mkoani ni tuta na hivi sasa ikinyesha mvua huwa mto juu yake, ni vema Serikali itueleze ni lini Pemba itapatikana Bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muungano wetu, Serikali imethibitisha kuwepo kero za Muungano na kusababisha Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi wa Zanzibar kukutana ili kutatua kero hizo. Ni vema basi Watanzania waambiwe, viongozi wetu hawa wameshakaa mara ngapi na wametatua jambo gani katika Katiba yetu na naomba nipatiwe mambo yenyewe yaliyotatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafuta Zanzibar, ni lini suala hili la mafuta litapatiwa mtaalamu au ni kitendawili na kuhusu gesi kama gesi ni mali yetu; je, Zanzibar inafaidika nini na gesi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu muda uliowekwa juu ya utatuzi wa matatizo ya Muungano, sioni sababu ya viongozi wetu yaani Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kukutana kwa mara tatu kwa mwaka na kusema mazungumzo haya huenda yakachukuwa miaka 15. Kama ni maradhi basi mgonjwa atakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo uchumi wa Zanzibar umekuwa mdogo sana na hicho kinachopatikana kutoka Muungano yaani 4.5% ya mgao ni moja ya lalamiko kubwa ndani ya Muungano. Je, kama Serikali imeliona hili la kuwa upande mmojawapo wa Muungano unaathirika, kwa nini muda wote uwe mkubwa kutatua mtatizo hayo?

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa kuwasilisha hotuba ya Ofisi yao, wakisaidiana na watendaji wao wote kwa ufasaha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza wapiga kura wa Jimbo la Jang'ombe kwa kuniwezesha kuingia katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuunda Tume ya viongozi wakuu wa Serikali ikiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi kwa kujadili masuala ya Muungano na kero zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero za Muungano ni nyingi sana na naamini si rahisi kuondoka kwa mara moja, zitaondoka hatua kwa hatua lakini kuna mambo ni kero lakini ni madogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji waliomo ndani ya Serikali wanachangia sana kukuza matatizo haya ya Muungano kwani suala la magari ya ZNZ ambazo zinatoka Zanzibar sioni sababu ya kukaa na kuvutana, kwani hata Waziri Mkuu alisimama ndani ya Bunge hili na kuahidi tatizo hili atalishughulikia lakini hadi hii leo kauli hiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hawajaithamini na kuongeza usumbufu kwa gari hizo kana kwamba ni gari zilizotoka nchi za nje. Aidha, suala la usafiri wa magari kutoka ZNZ kuingia mfumo mpya wa *T…A…* huo hatuna pingamizi nao, isipokuwa magari ya ZNZ yakionekana Tanzania Bara kufanywa kama ni uhaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuthamini haki ya wanyama na kuachana na uchafuzi wa mazingira, napenda kuishauri Serikali kuachana na nia ya kujenga hoteli ya kitalii ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro kwani uwezo wa maeneo mengine kwa ujenzi wa Hoteli hiyo inawezekana bila kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, natoa pongezi za dhati kwa niaba ya wananchi wangu wa Hai kwa sehemu zote mbili za

Muungano na Mazingira kwa Mawaziri wote wawili, Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wengine wote.

Kuhusu kazi inayofanyika upande wa Muungano tunaafikiana nayo kabisa ila ningependa kuuliza kama Mtanzania kutoka upande wa Bara anaweza kupata na kumiliki ardhi upande wa Zanzibar? Kama haikuwa inawezekana, ningeshauri iruhusiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la pili kwenye Muungano ni kuhusu malalamiko ya viwango vya ushuru kwenye pande zetu mbili kuwa yafanyiwe kazi na kuomba hayo malalamiko madogo yaliyopo lakini lazima viwango vizingatiwe pasiwepo na upendeleo wa upande mmoja kutoka ushuru kidogo. Napongeza mazugumzo yanayoendelea kati ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi.

Kwa upande wa mazingira kazi zinakwenda vizuri lakini tunahitaji kuongeza kasi na sheria zetu za mazingira zisimamiwe ipasavyo na zitekelezwe kwani kinyume na hapo bado mazingira yetu yatazidi kuharibika na hizo sheria kudharauliwa.

Suala la mifuko ya plastiki lazima tuwe *serious* zaidi kwani bado ipo na inaendelea kuingizwa nchini. Uhamishaji wa mifugo uende sambamba na tahadhari ya mazingira kwa kuandaa mazingira yanayofaa. Naomba Wizara ya Mazingira itutembelee kule kwetu Hai ili tuweze kutembelea maeneo mbalimbali kwa nia ya kuelimisha na kutoa msisitizo na uhifadhi wa mazingira kwa mfano vyanzo vya maji, uoto wa asili na kadhalika. Kwa mara nyingine ninawapongeza na kuunga hoja mkono.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nawapongeza Mawaziri wote wawili kwa hotuba zao nzuri na zenye mwelekeo ya kudhibiti suala la Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa salaam za rambirambi kwako Mheshimiwa Spika, wazazi na ndugu wa Marehemu Amina Chifupa Mpakan, Mungu aiweke mahali pema peponi roho ya marehemu, vilevile Mungu awape furaja wazazi na ndugu wa marehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijadili machache yanayohusu hotuba zote mbili. Kwanza suala la mabadiliko makubwa yanayotokea ya tabia nchi. Naomba Serikali iweke mikakati kwa ujumla njia na mipango sahihi na yenye kuonekana ya kuhifadhi mazingira hasa ambayo itashirikisha wananchi ambao ndio wadau wakubwa wa kuhifadhi mazingira. Usimamizi uimarike ikiwa kuongeza idadi ya watumishi katika Halmashauri watakaosimamia katika ngazi za Vijiji na Kata, Kamati za Mazinigra zilizopo kwenye vijiji zipewe uwezo wa kusimamia kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi waelimishwe kwa nguvu zote kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na wajibu wao katika kupambana na suala la mabadiliko haya. Suala la nishati mbadala ni muhimu ili kupunguza ukataji miti na hasa suala la mkaa ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira.

Suala la kuhamisha mifugo ni vizuri ieleweke kuwa wanyama au mifugo wanazaliana na wanaongezeka je, watahamishiwa wapi tena? Naomba Serikali iweke mpango wa kudumu ili wafugaji wasisumbuliwe tena kwa kuwahamisha bali niombe Serikali wapi itawapimia, wakulima na wafugaji na kuwamilikisha ili wayatumie maeneo hayo kudhibiti ongezeko la mifugo na kuondoa ugomvi kati ya wakulima na wafugaji.

Kuhusu usafi wa mazingira katika Manispaa na Halmashauri, ni lini Serikali itasaidia Manispaa na Halmashauri kuzipatia zana kama magari na vifaa kwa ajili kukusanyia taka? Vile vile Manispaa hizi zihimizwe kutumia vikundi mbalimbali kufanya usafi katika maeneo yao vikiwepo vikundi vya akinamama. Naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hotuba hii katika eneo la mazingira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, hoja kuhusu tatizo lililojitokeza katika chemichemi za Qanded katika Bonde la Eyasi, Wilaya ya Karatu. Chemichemi hizi zinategemewa sana na vijiji vya Qanded, Mbuga Nyekundu, Djobay, Dembechand, Manyola, Barazani, Malekchand, Endamaghang na Laghangarezi, kwa matumizi ya nyumbani lakini pia kwa umwagiliaji. Kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Uhifadhi Mazingira na Vyanzo vya Maji, Halmashauri ya Wilaya ya Karatu ilichukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuondoa mwekezaji aliyekuwa amejenga nyumba ya ghorofa na kubomoa nyumba yake baada ya ushauri wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya *(DC).*

(ii) Kuondoa mnada wa vile hasa wakati wa mvua uchafu wote ulikuwa ukitiririka kwenye chemchem hizo na hivyo kuathiri watumiaji wa maji kwenye vijiji vilivyotajwa. Mnada sasa kwa azimio la *full council* umehamishwa kwenye eneo lingine ndani ya kijiji hicho hicho.

(iii) Baraza la Madiwani pia lilipitisha kuwa ujenzi wa sekondari katika eneo hilo hilo, unaofanywa na Serikali ya kijiji uhamishiwe eneo lingine ambalo liko na wataalamu wa Halmashauri wamelikagua lakini uongozi wa kijiji umekataa kata kata kwa sababu wanazojua wenyewe.

(iv) Katika hatua hiyo Halmashauri ya Wilaya kupitia Mheshimiwa Mwenyekiti wa *Council* na Mbunge tumeomba *NEMC* itusaidie kufanya *EIA* kabla ujenzi huo wa shule ya sekondari haujaendelea. Tuna taarifa kuwa wataalamu wa *NEMC* wameenda Karatu mara mbili na safari moja wamefika hadi Qanded, Eyasi cha kusikitisha waliokwenda hawakumshirikisha hata Diwani wa maeneo hayo ambao ndio wanaopokea kilio cha wananchi wa vijiji vilivyotajwa na ambao ndio waathirika wakuu. Vyanzo hivyo vitakapoharibika au kuchafuka Madiwani hao ndio wanaojua sababu za kumwondoa mwekezaji aliyetajwa juu pamoja na mnada lakini maoni yao inaelekea hayakuhitajika. Je, huu ndio utaratibu sahihi wa *EIA,* bila kushirikisha wadau wote?

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi leo zaidi ya miezi minne tangu *NEMC* ilipoenda Qanded nimeomba taarifa ya *EIA* kupitia Halmashauri na hata kupitia Waziri tumeshindwa kupatiwa taarifa iliyo rasmi wala isiyo rasmi. Lakini ujenzi wa sekondari unaendelea. Je, utaratibu huu ni sahihi? Kwa utaratibu huu vyombo vya kisheria kama *full council* inaposimamia utekelezaji wa sera na maagizo ya Kitaifa inawekwa pembeni kwa mtindo huu. Iwapo kuna *double standard* Halmashauri itawashawishi vipi wananchi wa kawaida kutunza vyanzo vya maji na kuwaondoa kwenye mabonde oevu iwapo Serikali yenyewe inayumba?

Kwa taarifa na uzoefu wetu pale tulipomwondoa Serikali ya kijiji imewekeza *camp site* ya utalii na mapato ya *camp site* tunahisi yananufaisha viongozi wachache wa kijiji cha Qanded na mwekezaji huyu ndiyo aliyetoa fedha za kujenga sekondari si uamuzi wa mkutano mkuu. Je, kwa utaratibu huu wa *NEMC* tutafika wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu ya kina katika jambo hili vinginevyo natoa taarifa na nalenga kushika mshahara wa Waziri. Tumefanya tulivyofanya, Bonde la Ihefu sasa kigugumizi hiki kinatoka wapi?

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Mto Kilombero lenye eneo la kilomita za mraba 40,000 ni eneo lenye ardhi oevu. Sehemu kubwa ya ardhi hiyo inafaa kwa kilimo. Ofisi ya Makamu wa Rais iliyotolewa mapema mwaka 2006 ilitoa agizo la kuondoa wafugaji kwenye Wilaya hii ili kuweka matumizi bora ya ardhi hususan kwa shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda huu ninapotoa mchango wangu bado mifugo haijaondolewa sehemu nyingi kiasi cha kuleta mgongano kati ya wakulima na wafugaji. Baadhi ya uharibifu unaofanywa na wanyama hao ni kubomoa kingo za mito na kuongeza udongo, mchanga kwenye mito *(sedimentation),* kuharibu mazalia ya samaki aina ya *cichlidae* ambayo huwa kwenye ardhi ambayo hufurika wakati wa masika na kubakiza mabwawa ambayo ndiyo huwa mazalio ya samaki wenyeji wanaita sehemu hizo mifufu na kukomaza ardhi ya kilimo kiasi cha kufanya kulima kwa trekta kuwa ngumu kabla ya mvua kunyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yangu ilipitisha dodoso kwa kata zote 19 za Wilaya ili kubaini ridhaa ya wananchi kuhusu mifugo kati ya Kata zote ni kata mbili tu ndizo zilizopendekeza kuwa na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali kwa Wizara ya Mazingira ni kuwa itatusaidiaje wananchi wa Wilaya ya Kilombero kutekeleza waraka wa Makamu wa Rais?

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa hotuba yake nzuri yenye kueleweka. Hivyo naunga mkono hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa asilimia mia moja.

Pamoja na maelezo ya masuala ya Muungano yalioelezewa ambayo tayari yashafanyiwa kazi, lakini bado utekelezaji wake unasuasua. Hivyo basi yafanyiwe kazi kikamilifu na hayo ambayo bado yanayoshughulikiwa yajaribu kuharakishwa ili kupunguza maneno kwa wasioutakia mema Muungano wetu. Nautakia Muungano wetu udumu milele na naunga tena mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuchangia katika hoja hii iliyopo mbele yetu leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazungumzo ya kero za Muungano, Serikali imesema kwa mwaka wanakaa mara tatu, je, kwa mwendo huu wa jongoo si itachukua zaidi ya miaka 20. Mambo haya hayajatatuka kutokana na hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi wameshakaa mara ngapi na wametatua mambo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mafuta ni mambo ya Muungano, nafikiria na gesi vile vile ni ya Muungano na tunaambiwa Serikali bado inatafuta mtaalamu wa mafuta, je, Serikali ya Zanzibar inafaidika vipi na gesi? Serikali mpaka leo bado inapata mgao wa 4.5% ingawa Serikali imeshapata mapendekezo na Serikali bado inasuasua je? Kwa kufanya hivyo Serikali ya Muungano haioni kama wanaidhoofisha Serikali ya Zanzibar, ambayo uchumi wake kila siku unazidi kudidimia? Naiomba Serikali jambo hili waliharakishe ili waweze kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kero nyingine ya Muungano ni kuhusu *TRA* jinsi inavyowasumbua wafanyabiashara wa Zanzibar, naomba jambo hili lishughulikiwe haraka sana ili usumbufu unaowapata wananchi wa upande wa pili wa Muungano upungue au umalizike kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kuchangia kidogo kuhusu mazingira, naomba Serikali izidi kuongeza mikakati kuhusu mifuko ya plastiki kwani bado inaendelea kuonekana mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niwashukuru Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa hotuba nzuri zinazohusu Wizara hizi nyeti zilizopo Ofisi ya Makamu wa Rais. Kadhalika nitumie fursa hii kuwapongeza watumishi wote wa Wizara hizi mbili kwa maandalizi mazuri ya kuandaa Bajeti ya mwaka 2007/2008, kama utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha Bajeti ya mwaka huu naomba nichangie ifuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu Muungano wa Tanzania na Zanzibar. Muungano huu ni nguzo muhimu sana katika umoja wetu wa Kitaifa. Muungano umedumisha udugu zaidi kati ya Bara na Visiwani, lakini katika Muungano wetu huu ni kwa nini basi wigo usiongezwe kwa kuweka ushirikiano zaidi ikiwa ni pamoja na kuongeza Wizara ili ushirikiano uongezeke zaidi, kwa suala hili ningeshauri Wizara kama ya Kilimo, Chakula na Ushirika nayo iwe ya Muungano, Wizara ya Maji, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kuhusu Wizara hizi kuwa za Muungano kwa sababu muhimu kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa sera inayotumika ya nchi zetu ni sera zinazofanana, kadhalika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 hadi 2010. Pia mahusiano ya kijamii yamekuwa sana ambapo sasa Wabara kufanya shughuli Zanzibar au Wazanzibar kufanya shughuli za kimaendeleo Bara ni jambo la kawaida kabisa. Hivyo kwa Wizara hizi nyeti nilizozitaja ni kiungo kikubwa kwa shughuli za wananchi wa pande hizi mbili kwa shughuli za kila siku. Nashauri elimu itolewe kwa wananchi iwe ya kutosha kuelewa Muungano kwa pande zote mbili. Ofisi ya Waziri iongezewe watendaji ili kufanya kazi ya kuelimisha shughuli za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazingira, juhudi za Wizara kuelimisha wananchi kuhusu utunzaji wa mazingira bado ndogo, Wizara iboreshe shughuli zake na ihakikishe elimu ya kutosha inatolewa kwa kada zote ili wananchi waelewe mazingira ni nini na namna zipi zilizo bora katika kuboresha na kutunza mazingira. Kuhusu uchafuzi wa mazingira udhibitiwe vya kutosha na wale wanaohusika wachukuliwe hatua kali kama funzo kwa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitapenda katika majumuisho yake anieleze juu ya uchafuzi wa mazingira unaotendeka katika Ziwa Kitangiri ambapo sasa hali hiyo inaendelea kudhoofisha Ziwa na kupunguza ukubwa wake na hata kama jambo ambalo ni hatari kwa Ziwa hilo muhimu katika jimbo langu la Iramba Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwa kuwapongeza Mawaziri wote kwa hotuba, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, kwa hotuba nzuri, pamoja na watendaji wote wa Wizara hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwa upande wangu nichangie upande wa mazingira. Kwa kuwa uharibifu na mazingira kwa Mkoa wa Tabora ni mkubwa sana hasa pale ambapo ukame wa Mkoa wa Shinyanga kuendelea kuwepo na kusababisha wafugaji wengi kuhamia Tabora kwa kuwa ni karibu sana. Kwa kuwa Tabora ina maeneo

makubwa ya misitu na ambayo inahifadhiwa na Serikali ni vema ikachukua hatua za makusudi ili kuinusuru kuwa jangwa. Kwa kuwa wafugaji hufyeka miti kuzuia ndorobo na kwa kuwa hupenda kukaa katikati ya msitu na kuwa vigumu kuna gundua ni vema nikashauri kama ifuatavyo:-

Kwanza kuwe na shirikisho la Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji kwa kuwapatia semina na vipeperushi zaidi na pili, kutoa elimu ya mazingira kwenye mitandao mbalimbali kama vile kwenye luninga, redio hasa zile ambazo zimefunguliwa kwenye Mikoa *(TTV* – ipo Tabora), *Radio CG*, ambazo husikika kwenye Mikoa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo oevu, kwa Mkoa wa Tabora sehemu za Wilaya ya Urambo ambayo inapakana na Mto Malagalasi eneo hili lina vijiji ambavyo tayari vina hati miliki ya ardhi kiasi kwamba kila wanapoondolewa hudai fidia na kwa kuwa Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kukidhi madai hayo, hivyo basi, naomba niiombe Serikali isaidie maeneo hayo. Kama sijakosea sana eneo la Mpanda Mlowoka ni karibu sana na wananchi waishio Mto Malagalasi kwenye vyanzo vya maji ambayo inajulikana kama *Rambar Side* kama hivyo ndivyo basi naomba nayo ifanyiwe kama ifuatavyo:-

(i) Kuwepo mkakati wa makusudi kama ulivyofanyika Mbarali, kwa Serikali kusimamia kikamilifu.

(ii) Kutoa vitendea kazi kwa mradi ili watumishi waweze kufika kwenye maeneo husika kama vile gari, kwani kwa kupeleka pikipiki haitasaidia kutokana na urefu na umbali wa maeneo hayo.

(iii) Hifadhi za Uyumbu nazo ziangaliwe kwa makini.

(iv) Kusaidia kulipa fidia kwa vijiji vinavyoishi kisheria kwenye hifadhi hizo ili wananchi waweze kutunza mazingira.

(v) Barabara ziimarishwe kati ya hifadhi na hifadhi ili iwe rahisi kukagua wahalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza *NEMC,* kwa kazi nzuri waliyofanya kwa kuzuia mifuko ya plastiki na mji kuwa msafi hasa Jiji la Dar es Salaam na hata hapo Dodoma. Pongezi za pekee ziende kwa Mwenyekiti Mheshimiwa Hilda Ngoye, kwa kufuatilia kwa kina maeneo yenye matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kuwa kufanyike mkakati wa makusudi kwa kufuatilia viwanda vyenye ukaidi wa utunzaji wa mazingira kwenye maeneo yanayozunguka viwanda vyao na kuhakikisha sumu au dawa zao ambazo zinatumika zihifadhiwe bila kuleta madhara kwa watumishi. Tulitembelea kama Kamati na tuliyaona hayo kwenye baadhi ya viwanda Dar es Salaam. Naunga mkono hotuba hii.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema na kuweza kushiriki katika kikao cha leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikupongeze wewe, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Muungano wetu ni wa muda mrefu, zaidi ya miaka 40 sasa na kwa kuwa hapo mwanzo kulikuwa na vipengele visivyozidi kumi na moja na hivi sasa kuna zaidi ya vipengele 30 vilivyoongezeka. Je, Serikali haioni kuwa ni vyema kupata ufumbuzi wa vipengele vilivyopo badala ya kuendelea kuongeza vipengele vingine?

Kwa kuwa nchi yetu hivi sasa imo katika mchakato wa kukusanya maoni kuhusu Shirikisho la Jumuiya ya Afrika Mashariki, je, Serikali haioni kuwa ni vyema kuzipatia ufumbuzi wa kudumu kero zote za za Muungano kabla ya kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki? Je, Serikali haioni kuwa kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki tukiwa na kero nyingi za Muungano ambazo hazijapatiwa ufumbuzi hakutaonyesha mwelekeo mzuri kwa nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mgao wa sasa wa 4.5% kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni mdogo sana kiasi ya kuifanya SMZ ishindwe kutekeleza shughuli zake mbalimbali za kunyanyua uchumi wa Zanzibar na hivyo kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar. Tunaomba mgao mpya upatikane kwa haraka iwezekanavyo ili Zanzibar iweze kunufaika na matunda ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa sasa wa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi kushughulikia kero za Muungano haukidhi mahitaji hasa ukizingatia kuwa viongozi hawa wote wawili wanatoka CCM wakati nchi yetu imo katika mfumo wa vyama vingi. Pia ukizingatia kuwa Muungano ni wa wananchi wote wa pande mbili za Muungano na sio wa viongozi wa CCM peke yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, imani ya kweli ndio itakayosaidia kutatua kero za Muungano, ahsante.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii ili nichangie suala zima la mazingira, mazingira ni uhai na bila mazingira mazuri basi vizazi vijavyo vitatusuta. Katika Bajeti ya mwaka huu tumeona ni jinsi gani bidhaa za mafuta zimepanda, hiki ni kiashiria tosha kwamba bidhaa zote zitapanda kwani nishati ya mafuta ndio chimbuko la uchumi na maendeleo. Hali hii itafanya wananchi zaidi ya asilimia 80 wataendelea kutumia kuni na mkaa ambayo kwa kiasi kikubwa itaathiri mazingira. Lakini haiishi hapo tu kwani misitu ndio chanzo kikuu cha mvua. Tanzania kwa kipindi kirefu sasa imekuwa na ukame kutokana na sababu mbalimbali kubwa ikiwa ni ukataji ovyo wa misitu. Tunaomba Serikali wakati inazuia watu wasikate miti pia iwape nishati mbadala na ya bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *NEMC,* taasisi hii ni chombo ambacho kimeundwa kisheria lakini bado haijawa na meno ya kutosha. Mfano mzuri ni pale taasisi hii inapotoa tamko la kuzuia uharibifu wa mazingira na wahusika kukataa kutii amri kama ilivyotokea kwa kiwanda cha *Karibu Textile*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mlima Kilimanjaro, wakati nilipouliza swali la kupungua kwa barafu Mlima Kilimanjaro, Waziri alikiri kuyeyuka kwa barafu kwa kasi kubwa sana, je, Serikali ina mikakati gani ya kuunusuru Mlima huu unaoingizia Taifa hili fedha nyingi za kigeni?

Kuhusu Muungano, Muungano wetu tunaupenda na tunapaswa kuuheshimu na kuulinda kwa gharama zote. Ni jambo la kusikitisha kuona viongozi wetu wakuu wa nchi hizi mbili wakienda kwa *pace* ndogo mno kwani kero hizo zinajulikana lakini utekelezaji unasuasua bila sababu za msingi. Ieleweke kuwa uvumilivu una mwisho wake, watu wakichoka kusubiri huweza kufanya mambo ambayo si mazuri kwa nchi zetu.

Mwisho, naomba ile *political will* iliyokuwepo iendane na utekelezaji, tuache itikadi, tuweke Utaifa mbele.

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH:** Mheshimwa Spika, Zanzibar na Tanganyika zimeungana Aprili, 1964, kwa upande wa Serikali tena baadhi ya Wizara tu. Kichama Zanzibar na Tanganyika zimeungana mwaka 1977. Hapo ndipo Muungano ulipokamilika kwani nchi mbili zilizoungana kwa upande wa dola (jeshi) na itikadi ya chama basi Muungano huo ni wakudumu na imara.

Muungano ulisaidia sana Zanzibar katika kuulinda kwa vile ilikuwa changa. Tanganyika hivi sasa ina watu milioni 36 na Zanzibar hivi sasa ina watu milioni moja tu Tanzania kwa ujumla wake ina watu milioni 37.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar tangu awali ni Visiwa vinavyotegemea bahari hasa kutokana na ufinyu wa eneo lake la ardhi. Zanzibar inategemea sana Bandari ndipo Rais wa awamu ya sita alipotangaza mkakati wa uchumi kutegemea bandari huru. Mnamo mwaka 1975 ikiwa ni karne moja imepita tangu Zanzibar yenyewe itangaze bandari yake huru mwaka 1895. Hivyo basi, Serikali ya SMT kwa kujali na kuonesha nia ya kutaka kuisaidia Zanzibar kiuchumi, nashauri katika mbinu za miundombinu za SMT itakapofungua bandari Bagamoyo nafasi ya bandari huru ingeachiwa Visiwa vya Zanzibar kwa maendeleo ya wananchi wake na pia kunyanyua pato la uchumi wake. Bandari ya Bagamoyo iteue bandari ya Zanzibar kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, SMT haina budi kuisaidia Zanzibar katika kusimaisha miundombinu ya kukuza pato la Zanzibar katika kufunguwa viwanda vya kusindika samaki ndani ya eneo la *EEZ*. Zanzibar isaidiwe kupata mikopo na ubia ya kufungua viwanda hivyo angalau vitatu Zanzibar Kaskazini, Kati na Kusini mwa barabara ya Zanzibar. Pemba kujengwe viwanda viwili Kaskazini na Kusini mwa Pemba. Viwanda

hivi vitasaidia sana kunyanyua hali ya uchumi wa Zanzibar na kutoa ajira kwa wananchi wake wenye asili ya Pwani na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, SMT lazima isaidie kuimarisha mfumo wa elimu Zanzibar kuanzia elimu ya chekechea hadi Chuo Kikuu. Zanzibar kielimu tupo nyuma kulinganisha na Tanzania Bara. Zaidi ya hilo basi vyema Wizara ya Elimu ingekuwa ya Muungano ili Zanzibar iweze kubebwa kwa maendeleo ya Taifa zima. Hapa Zanzibar lazima isaidiwe kwenye umahiri na walimu, mbinu za ufundishaji, kupatikana vifaa vya kufundisha. Zanzibar lazima iwe na shule za mabweni kama Bara ili iweze kutoa wanafunzi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi na Zanzibar haumudu shule za mabweni. Serikali ya SMZ kwa ujumla inachechemea kutokana kuwa na uchumi dhaifu na upungufu wa kipato. Pato la Taifa lazima lipangiwe mikakati miundombinu ili kuweza kukokotowa kodi ili kuendeshea huduma za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ni kama mshipa wa damu wa Serikali katika kukuza kipato Zanzibar haina miundombinu endelevu kwa pato la uchumi wake, karafuu haina bei na nazi pato lake limedumaa. *Package tourism* ina uwa utalii Zanzibar na hili ni kusudi la vyama vya upinzani.

Kero za Zanzibar kila siku zinazidi bila ya sababu zozote za maana hasa tunapozingatia Tanzania na wananchi wa pande mbili kusumbuana. Nashauri gari za ZNZ zinazoingia Tanzania Bara zipatiwe tamko la kutumika Bara kama vile gari za *T*... zinavyoendeshwa visiwani na vile vile si vyema na haipendezi pale mwananchi wa Zanzibar anapotozwa ushuru kwa watu binafsi ambao wameshalipia ushuru wanapoingia nayo katika bandari za Tanzania Bara na kero hii ni manyanyaso makubwa ambayo yaondolewe kama vile *Passport* ilivyoondolewa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Muungano limetitia kuibuka na heshima ya Bunge la Muungano kwa sababu ya kutokuwa na Mkutano na Muungano ndani ya mikutano yake ya 20 katika kipindi cha kutoka miaka mitano. Upinzani kero na manyanyaso yote yameibuka baada ya Bunge kutokea na kuweza kuzungumzia matatizo ya wananchi wake. Nashauri vikao vya namna hiyo sasa ni wakati mzuri wa kuanzishwa, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza mtoa hoja kwa hoja yake nzuri ambayo imetupatia mwelekeo mzuri katika masuala ya yahusuyo mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kwa kuchangia kwamba zimeonekana kuwepo shughuli nyingi sana za binadamu ambazo huharibu na kuchafua mazingira yetu

kwa kiasi kikubwa mno. Baadhi ya shughuli hizo ni kama kilimo cha kizamani, shughuli za viwanda, ufugaji duni pamoja na uvuvi na ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona jinsi mmomonyoko wa udongo unavyoharibu mazingira yetu, hivyo ni dhahiri kabisa Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, ili kuhakikisha kilimo cha kisasa kinaendelezwa. Ni lazima kuhimiza kwa nguvu zote kilimo cha matuta ya kontua. Vile vile tuzuie kwa nguvu zote ukataji ovyo wa miti ambapo pia tutaweza kuzuia mmomonyoko na jangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo madhara makubwa sana yatokanayo na viwanda vyetu. Ni muhimu kabisa kutembelea mara kwa mara viwandani humo na kuangalia namna mazingira yetu yanavyoharibika. Mfano, viwanda vingi hutiririsha maji yaliyo na mchanganyiko wa kemikali katika vyanzo vyetu vya maji. Hii ni hatari kwa binadamu na vile vile huua *species* za viumbe vilivyomo katika vyanzo hivi vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vingine vimekuwa vikifusha moshi mkubwa ambao unasababisha madhara ya maradhi kwa binadamu. Ni jukumu la Serikali kufunga viwanda vyote vinavyopakana na makazi ya watu ili kuondoa matatizo makubwa ya kiafaya kwa wakazi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, itolewe pia elimu kwa wafugaji ili waondokane na tabia ya kuweka mifugo mingi katika eneo moja, kwani kufanya hivyo husababisha mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo pia na tabia ya uvuvi na uwindaji holela. Ni lazima suala hili liangaliwe kwa umakini kwani linaweza kusababibisha kupotea kwa *species* mbalimbali. Kwa mfano, uvuvi wa samaki ambao bado hawajakomaa kwa kuvunwa, kuwinda wale wanyama ambao wamebakia wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli nilizoziorodhesha ni muhimu sana katika maisha ya kila siku ya binadamu, kuziepuka ni vigumu. Lakini, iwapo Serikali itaweka sera bora juu ya utunzaji wa maingira, basi uharibifu utakuwa mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya maji *(water catchments)* ni lazima viangaliwe. Ziwekwe sheria kali za kudhibiti uharibifu wa vyanzo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upandaji miti lisiwe la msimu tu. Tujaribu kupanda miti kwa misimu yote kwani kila aina ya mti inakubali kuota katika msimu fulani, hivyo ni lazima sera ya upandaji miti itekelezeke katika msimu wote wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu pia kuweka sheria juu ya *bi-product Recycling* hasa zile za viwandani, kwani mara nyingi *bi-products* hizo huwa ni chanzo cha uchafuzi wa mazingira. Lakini, *bi-products* hizi hizi zikizungushwa tena na kutengenezwa na kutoa bidhaa nyingine, tutapunguza sana uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia semina mbalimbali juu ya utunzaji wa mazingira zitolewe kwa wingi vijijini na zisiishie mijini tu. Kwa hayo machache, naomba kuwasilisha. Ahsante !

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mawaziri wote wawili kwa kuweza kuwasilisha hotuba zao ambazo ni nzuri. Ninaziunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kama ifuatavyo, kwanza ni mambo ya Muungano:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Tanzania Visiwani uanze kufanywa ikiwa sawia na kuongeza idadi ya watumishi wa Ofisi hiyo ili ikidhi haja yake.

Pia taarifa ya maamuzi za kero ya Muungano zitolewe kwa Watanzania kila mwezi ikiwa na aina ya kero ambazo Watanzania wengi hawazijui, utafiti wa gesi na mafuta Tanzania Visiwani ufanywe sambamba na ule unaofanywa Tanzania Bara na Serikali ya SMT na SMZ ziangalie uwezekano wa kuziunganisha baadhi ya Wizara/Taasisi zake kuwa za Muungano, kwa mfano, JKT, Magereza (Vyuo vya Mafunzo) ili kuzifanya Wizara kamili za Muungano (Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kadhalika).

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibuwa wa Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais urejeshwe kama ulivyokubalika na waasisi wa Muungano wa Tanzania kwa vile utaratibu wa sasa haumpi Rais wa Zanzibar hadhi anayostahili Kimuungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho vya Uraia Tanzania vitolewe kwa Watanzania wote Tanzania Bara na Visiwani kwa makini hasa kwa upande wa Tanzania Visiwani na mipakani mwa nchi yetu. Idara ya Uhamiaji isiachiwe zoezi hili peke yake. Naipongeza Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa jengo la Kisasa la Ofisi Ndogo ya *BOT* huko Zanzibar. Ninaomba ufunguzi wa jengo hilo ufanywe haraka ili jengo hilo lianze kutoa huduma zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa taasisi za Muungano wasikae upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano tangu wanapoajiriwa hadi kustaafu kwao, bali wawe wakifanyakazi kwa kubadilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya mazingira, nishati mbadala zilizobuniwa na baadhi ya wananchi kwa matumizi ya kupikia na kadhalika zitangazwe na kuenezwa kote nchini ili wananchi watumie. Aidha, Serikali idhibiti kwa dhati bidhaa ambazo zimebainiwa kuwa na madhara kwa matumizi ya binadamu. Utaratibu uliopo sasa unatoa mwanya wa kuchukuliwa bidhaa hiyo iliyotupwa au kufukiwa, ambapo hufukuliwa na baadhi ya wananchi na kuiuza kwa walaji. Kwa mfano, ngano, mchele, mafuta ya kupikia na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uingizaji wa vifaa vya *electronics* nchini hasa vilivyotumika kama vile *television, computers, printers,* pamoja na vifaa vingine chakavu, uangaliwe upya kwa vile bidhaa hizi ni hatari sana kwa afya na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, *polution* inayotokana na moshi wa magari hasa kwenye miji mikubwa, umechangia uharibifu wa mazingira ya afya ya mwanadamu. Serikali iyatoze kodi kubwa magari yanayotoa moshi mwingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda kama vile *Tanzania Breweries* kilichopo Ilala, Jijini Dar es Salaam, kichukue hatua madhubuti za kuzuia uchafuzi wa mazingira kwa afya ya wananchi wanaokaa katika maeneo ya jirani na kiwanda hicho. Viwanda vijengwe mbali na makazi ya watu.

**MHE. PAUL P. KIMITI :** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kabla ya yote, naunga mkono hoja hii na kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais akisaidiwa na Waziri wake Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na watendaji wake wote kwa jitihada walizozifanya kwa kipindi chote cha mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa unajulikana kwa tatizo la kuanza kugeuka kuwa jangwa kama jitihada hazitachukuliwa haraka kunusuru hali hii. Mwaka jana nilituma nakala kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu tatizo hili na katika makala maalumu iliyoandaliwa na *Capt*. Zeno Nkoswe, niliomba Wizara yetu itafute njia yoyote ile ili kusaidia jitihada za Mkoa katika kuukoa Mkoa usiathirike na hali ijayo ambayo hata heshima ya Mkoa kuwa na uwezo wa uzalishaji wa chakula inaweza kutoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa sijapata majibu ya nini Wizara inashauri na imechukua hatua ipi kunusuru hali hiyo isitokee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa una eneo kubwa sana ambalo linafaa kwa kuanzisha msitu wa Kitaifa kama ilivyo *Sao Hill Forest*. Hali ya hewa ni sawa kabisa na miti ya *Sao Hill,* inaweza kustawi kama inavyostawi katika msitu huo. Wawekezaji wa ndani na nje waombwe kuja Mkoani Rukwa kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya miti/misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kumekuwepo na utata wa matumizi ya dawa ya kuua mbu iitwayo *DDT* ambayo licha ya kuwa ilisaidia sana kupunguza mazalio ya mbu miaka ya 1960 na 1970, lakini Mashirika ya *WHO* na *FAO* baadaye wakasitisha matumizi yake. Lakini, inaonekana kuwa dawa hii imeruhusiwa tena, lakini wakati huo huo kuna wanaharakati wa mazingira wakiendelea kukataza matumizi yake. Je, ukweli uko wapi kuhusu utata huu ambao umeanza kujitokeza?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006/2007, Bazara la Utafiti wa Mazingira *(NERA),* lilitambua kuwepo maeneo tete katika Mkoa wa Rukwa na kutakiwa yaanze kushughulikiwa. Je, hatua ipi inayofuta ili kusaidia hali isiendelee kuwa mbaya kwa maeneo yote oevu ya Ukanda huu wa Kusini Magharibi ikiwa pia ni kwa Mkoa wa Kigoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa huwezi kutenganisha kati ya ongezeko la idadi ya watu na hifadhi ya mazingira, je Wizara inashughulikia vipi suala hili ili lisionekane kuachiwa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji au Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pekee? Nashauri katika kipindi hiki cha Bunge kuandaliwe kikao *(Symposium/Seminar)* kwa Wabunge ili kwa undani zaidi waone uhusiano wa namna ya kurekebisha hali kama hii isiendelee kuathiri ukuaji wa uchumi na madhara yake kwa umaskini kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais kupitia kwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kwa kumteua Mheshimiwa Hilda Ngoye, Mbunge mwenzetu kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mazingira. Uzoefu na uwezo alioupata wa kuhifadhi Mlima Rungwe na *Livingstone Mountain,* vinatupa imani kuwa atatusaidia sana kuendeleza hifadhi katika maeneo yetu yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuwashukuru wewe na Mheshimiwa Spika, kwa kutuongoza kwa kasi na viwango vya hali ya juu. Viwango vya michango ya Waheshimiwa Wabunge, nadhani utakubaliana na mimi hakika ni vya hali ya juu na ni michango ya kina sana. Nampongeza na kumshukuru vile vile mwenzangu Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuwasilisha hotuba yetu kwa ufasaha mkubwa. Niseme kabla sijasahau kwamba, naunga mkono hoja yetu kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia kwa kufanya majumuisho katika maeneo manne yafuatayo: Nitaanza kwa rambirambi na kutoa shukrani, nitapitia masuala ya kijumla na ya kisera kuhusu sekta ya mazingira, lakini vile vile nitapitia masuala ya utekelezaji wa sera, sheria na mikakati mbalimbali, baadaye nitafanya hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana ya rambirambi, natoa rambirambi kwa familia, ndugu na marafiki kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia huandikwa kwa njia mbalimbali, mojawapo huwezi ukaamini lakini hivi vikaratasi ambavyo tunapeana ujumbe, nilikuwa napitia juu ya deski langu wiki hii nikijitayarisha na michango katika kuchangia hoja hii, nikakuta kikaratasi kimoja nilimwandikia Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia 19 Aprili, 2007 kabla sijaondoka kwenda Dar es Salaam. Kwa bahati mbaya sikuweza kumpa lakini kilisema nakushukuru ahsante sana. Nimesahau ni kwa nini lakini hakupata huo ujumbe. Kwa sababu wote tunakwenda huko aliko, basi naamini nitapata siku moja ya kumshukuru. *(Makofi)*

Natoa rambirambi pia kwa wananchi wa Mwanza na Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza, kwa kupotelewa na wenzetu wachapakazi wazalendo; aliyekuwa Mbunge

mwenzetu hapa, Marehemu Stephen Kazi, Ndugu Hezron Ndoho na Ndugu William Kasubi. Vile vile natoa rambi rambi kwa waliofiwa na wale waliopotea katika ajali za barabarani huko Mbeya, Singida na Arusha. Kwa wote nasema Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Rungwe Mashariki sijui niwashukuru kwa njia gani, wamekuwa na imani kubwa kwangu na wamekuwa ni mhimili mkubwa kwangu kisiasa. Tumekuwa pamoja katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. Nawaomba tuendelee na umoja huo na mshikamano ili ndege ya maendeleo aliyozungumzia Mheshimiwa Edward Lowassa isituache. Vinginevyo tutabaki kwenye chumba cha abiria tukibishana nani atakaa kiti gani. Nadhani tunaelewana? Mimi naahidi kuendelea kuwatumikia kwa uwezo atakaonipa Mwenyezi Mungu, kwa bidii, juhudi, kwa nguvu zangu zote na kwa moyo wangu wote. *(Makofi)*

Namshukuru vile vile Mheshimiwa Makamu wa Rais, tumebahatika kufanya kazi chini yake. Msimamo wake, maelekezo yake na uongozi wake ni thabiti kabisa. Kwa siku hadi siku tunaongozwa na si mwingine bali ni Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Waziri Mkuu, tunamshukuru kwa usimamizi wa Serikali. *(Makofi)*

Namalizia shukrani zangu kwa kuishukuru familia yangu, mke wangu Lucy, watoto wangu Max, Sekela, Emmanuel, wakwe zangu Johana na Digna na mjuu wangu Tusekile na watoto zaidi 100 ambao tunawalea kupitia Kituo cha Malezi cha Mama Lucy Mwandosya. Leo hii familia yote hii kubwa imewakilishwa kwenye *gallery* ya Spika na Mke wangu Lucy na vilevile mmoja wa watoto hao 100 anaitwa Cecilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa natoa majumuisho na majibu katika masuala ya kisera ya kijumla na vile vile ya kisheria. Ukizingatia Sheria ya Mazingira Namba 20 ya mwaka 2004, kuna mambo mawili yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge na wameandika katika michango yao ya maandishi; nayo ni kuhusu usafi viwandani na uchafuzi unaotokana na mifuko ya *plastic*. La pili, wamezungumzia kuhusu elimu hasa elimu ya mazingira na kusisitiza umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kutekeleza mpango wa elimu kwa umma kupitia *radio, television*, mikutano, mijadala, mikutano ya hadhara, mashindano ya usafi wa mazingira na kadhalika, lakini vilevile tutaendelea kutoa elimu mashuleni, vyuoni. Baraza la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira lina wajibu mkubwa wa kusimamia na kusukuma elimu kwa umma kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Vilevile kila sekta ina wajibu wa kusisitiza hili suala la elimu kwa umma katika suala zima la mazingira na asasi zisizo za Kiserikali zina wajibu mkubwa. Naomba kila mradi unaoanzishwa unaohusu mazingira, usisitize elimu kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye masuala ya utekelezaji, nitaanzia na Maoni ya Kamati, ambayo yalitolewa kwa ufasaha mkubwa na Msemaji wa Kamati, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura. Tumepokea na tutatekeleza maoni na ushauri mzuri wa Kamati ya Maliasili na Mazingira. Tumefaidika sana na michango yao wakati wote tunapokuwa nao na tunawashukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Wamezungumzia vilevile kuhusu zoezi la kuwahamisha wafugaji kutoka Ihefu. Niseme tu kama Serikali, tumejifunza mengi, uzoefu tulioupata na ushauri utakaotokana na Tume Teule ya Mheshimiwa Rais, utatusaidia sana kama Serikali kuboresha utendaji hasa tunapokuwa na *operation* ya namna hiyo. Naomba Waheshimiwa Wabunge, tungojee tu matokeo hayo ya Tume ambayo imewasilisha ripoti yake kwa Mheshimiwa Rais. Pamoja na hayo niseme tu kwamba, hali ya mazingira ya Ihefu imebadilika, imekuwa nzuri. Changamoto kwetu ni kufanya mazingira hayo yaendelee kuwa bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mifuko ya *plastic,* wachangiaji wote wameisifu hatua ya Serikali ya kupiga marufuku mifuko laini ya *plastic*, wote wamesema hatua za ziada zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kupiga marufuku mifuko yote ya *plastic*. Wamekwenda mbali sana kuliko Serikali. Niseme tu tutazingatia hilo tutakapofanya tathmini ya utekelezaji wa agizo hilo, hatua za ziada zitachukuliwa ikibidi kwa mfano tunaweza tukaiga Rwanda ambao wamepiga marufuku kabisa hii mifuko ya *plastic*.

Lakini tumefanya nini *NEMC?* Katika kipindi hiki imekagua viwanda 18 lakini viwanda viwili ambavyo lazima nivitaje hapo *Omar Packaging* cha *Mwalimu Nyerere Road* na *Saafa Plastic Limited* cha Buguruni, vimebainika kuendelea kutengeneza mifuko. *NEMC* imewapa karipio, ni matarajio yangu kwamba watafuata hilo karipio vinginevyo *NEMC* ina uwezo wa kivifungia hivyo viwanda. Lakini vilevile tutaendelea kutoa elimu kuhusu suala zima la *plastic* na tutahakikisha kwamba, kwa zile *plastic* zinazoruhusiwa basi nembo zinawekwa ili tuweze kufuatilia zinatengenezwa na nani na ukaguzi utaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu Kenya niseme wametuiga kwa sababu Waziri wa Fedha wa Kenya, Mheshimiwa Amosi Kimunya, katika Hotuba yake ya Bajeti ya 14 Juni, 2007, amepandisha ushuru wa *plastic* kwa asilimia 120 na amepiga marufuku mifuko laini ya *plastic*. Waziri wa Fedha, Mipango na Uchumi wa Uganda, Mheshimiwa Dr. Soluma naye katika hotuba yake ya bajeti ya Juni, 2007 amepiga marufuku mifuko ya *plastic* chini ya *micron 30*, mifuko wanayoiita wao Buvelo, ambayo sisi tunaiita Rambo.

Ameongeza ushuru kwa asilimia 120 kwa mifuko ambayo ni minene zaidi ya hapo. Mtakumbuka kwamba, hizi ni hatua ambazo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilizichukua mwaka 2006. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba, hatua za pamoja Afrika Mashariki zitatusaidia sana kudhibiti mifuko hii. *(Makofi)*

Tathmini ya athari kwa mazingira imeweka bayana katika kifungu cha 81 mpaka 104, ulazima wa mradi wowote ule ambao umeainishwa kisheria kufanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira na hakuna leseni yoyote itakayotolewa na mamlaka yoyote kutekeleza mradi wowote au miradi yoyote bila hati ya tathmini ya athari kwa mazingira. Katika miradi 25 ambayo mpaka sasa tumeifanyia tathmini ya athari kwa mazingira, miradi 24 imepewa hati na mradi mmoja tu ndio ambao umekataliwa.

Asilimia 40 ya miradi hiyo iko katika sekta ya madini, asilimia 20 katika sekta ya kitalii, asilimia 16 viwanda vya kemikali na vyakula, asilimia 12 ni nishati na asilimia 12 nyingine iliyobaki ni kwa ajili ya barabara, mafuta na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie utekelezaji wa suala la tathmini ya haraka ya athari kwa mazingira ya ujenzi wa shule za sekondari ya Kwandede huko Karatu.

Hili ni eneo tete kimazingira, kuna chemichemi kama 29 na ziko katika lindi maji,ni chanzo mto Balai ambao unaelekea Ziwa Eyasi, ni bonde maarufu kwa kilimo cha vitunguu hasa kwa Kata za Balai na Mang'oka.

Tarehe 10 mwezi wa Nne mwaka 2007, *NEMC* ilipokea barua kuhusu tatizo lililopo, ni kama mgogoro vile wa ujenzi wa Shule hiyo. Vile vile Mheshimiwa Slaa aliwasilisha maoni yake au malalamiko yake kwangu kuhusu suala hilo. Tarehe 4 mwezi wa Nne nilituma ujumbe wa wataalam kufanya tathmini kutoka Baraza la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira. Tumepokea rasimu ya ripoti, ripoti inakamilishwa, wadau wote hasa Halmashauri husika, Uongozi wa Mkoa pamoja na Mheshimiwa Mbunge watapata ripoti hiyo baada ya muda sio mrefu. Kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi na Vyanzo vya Maji, natambua mchango wa Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka na Mheshimiwa Lotto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetembelea vijiji katika maeneo yao, baadhi ya vijiji hivyo katika milima ya Uluguru ni Kiloka, Kinole, Tawa, Matombo, Kibungo Juu, Msitu wa Kimboza, Ruvu, Maseyu na Mikese. Nimejifunza mengi sana hasa umuhimu wa elimu ya asilia au elimu ya jadi na utamaduni katika hifadhi ya mazingira.

Nilielezwa jinsi ya kupima wapi, au umbali gani, huwezi ukafanya shughuli za kilimo na makazi kwa kutumia mawingu yanapoonekana. Hii ni elimu ya jadi. Kwa maana hiyo, sio kweli kwamba walikuwa katika vilele vya milima. Nilielezwa kwamba mawingu sasa yameshuka kutokana na uharibifu wa mazingira; au yamepanda kutokana na uharibifu wa mazingira. Vinginevyo, zamani mawingu yalikuwa chini na ule ndiyo ulikuwa mstari ambapo mtu haruhusiwi kulima kupanda juu. Kwa hiyo, ilikuwa ni elimu kwangu.

Sasa miaka 50 kwa mfano mipaka iliwekwa Morogoro Mjini kutumia katani, kupiga marufuku kilimo na makazi katika eneo juu kidogo ya mji wa Morogoro. Milima ya Morogoro ya Uluguru ni tofauti sana na milima ya nyanda za juu Kusini. Maana niliombwa kwamba *charity begins at home*; ningeanzia kuwaondoa watu wa milima ya nyanda za juu Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba nyanda za juu Kusini milima yake ni uwanda wa juu unaotokana na kinachoitwa *escapment* kwa sababu ya bonde la ufa. Ni tofauti sana na milima ya Uluguru. Nawaalika Waheshimiwa Wabunge na wengine mje mwone jinsi hali asili inavyorudi baada ya kuwaondoa watu kwenye miteremko ya safu za milima ya *Livingstone* ili kulinda vyanzo vya maji. Hili halikufanyika na awamu hii ya nne, hapana. Lilifanyika wakati wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakati kitu

kilichokuwa kinaitwa *Operesheni Sogea* ili wote waliokuwa milimani washuke wapate huduma muhimu na hawajarudi mpaka leo. Imekuwa faida kubwa kwetu. Hii ni moja ya faida ya Operesheni Vijiji.

Sasa kwa upande wa Kiloka na Kinole wengi wameshuka, wengi walikuwa wakilima, lakini wanakuja kuishi chini na walikuwa na mguu mmoja juu, mguu mmoja chini. Kwa hiyo, hatujapata tatizo kubwa kuhusu hilo. Lakini tumeelezwa kuhusu kwa nini tunazingatia milima ya Uluguru.

Milima ya Uluguru ina umuhimu mkubwa sana kwa Taifa, kanda na kimataifa. Milima ya Uluguru ni moja ya maeneo 25 yenye umuhimu wa bionuwai ya misitu duniani na milima ya Uluguru inatambulika kimataifa. Milima ya Uluguru pamoja na milima mingine ya Tao la Mashariki ina aina 74 za wanyama wakubwa, yaani *vertebrates* na kati yao 13 hawapatikani sehemu nyingine yoyote duniani isipokuwa huko.

Lakini kuna mimea adimu na vile vile ni chanzo kikubwa cha maji Morogoro na Dar es Salaam. Sasa unaweza ukasema wabaki huko huko; lakini baada ya miaka 20 watakuwa wengi na madhara yatakuwa makubwa zaidi na maji yatapungua. Mimi naona afadhali hiyo operesheni iendelee. Ni ngumu, lakini tunafanya haya kwa kizazi cha sasa na kizazi kinachokuja. Ukilinganisha milima ya Uluguru na milima mingine ya Tao la Mashariki, sehemu ya milima ya Uluguru imeharibika zaidi katika kipindi cha miaka 20 iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukalinganisha na milima kama vile ya Ukaguru na Rubeho, huko ni kuzuri zaidi kuliko milima ya Uluguru. Nayo inatokana na *stress* kutokana na watu walivyozidi. Kwa hiyo, hamna utata tufanye nini. Nadhani wote tunakubaliana kwamba kwa kweli inabidi tudhibiti uharibifu uliopo na unaoweza kutokea kutokana na watu kuendelea kuishi katika vilele vya safu ya milima ya Uluguru.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba nimewasilikiza kwa makini sana wenzangu na ninawaelewa vizuri sana. Naomba wanielewe na watuelewe kwamba, kazi ya udhibiti wa mazingira ni ngumu. Kama unataka kupendwa, usiingie katika kazi hiyo. Sawa sawa na mambo ya dini, kama unataka kutenda dhambi usiende Kanisani, kwenye Msikiti au mahali kama hapo. Sababu ni moja! Unaposhughulikia kazi ya udhibiti wa mazingira, matokeo yake utayaona miaka 25, 30 kuanzia sasa. Kwa hiyo, ndiyo maana wanasema wameniambia wenzangu wanasema mazingira siyo dharura. Sikubaliani nao. Mazingira ni dharura. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nalinganisha sasa na wenzetu wa dini wanaofanya kazi huko, wao *time frame* yao ni kubwa zaidi maana yake wanazungumzia Ahera. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema tunafanana fanana. Kwa hiyo, kama unazungumzia kupata kura 2010 mambo ya mazingira haya hayatakusaidia sana. Kwa hiyo, nimewaelewa ndugu zangu. *(Kicheko/Makofi)*

Utekelezaji wa mkataba wa usimamizi wa hifadhi endelevu wa hifadhi wa Ziwa Tanganyika. Burundi, Tanzania DRC Congo na Zambia, ndiyo tumetia saini mkataba huo. Masharti ya Mkataba karibu yote yamezingatiwa. Mamlaka ya Ziwa Tanganyika yameanzishwa mwezi wa Nne mwaka huu. Ilizinduliwa Dar es Salaam. Lakini sharti moja tu bado ni kwamba nchi zote ziwe zimeridhia mkataba kabla ya Wafadhili hawajatoa fedha za kutusaidia. Mpaka sasa Jamhuri ya Kimokrasia ya Congo haijaridhia. Kwa hiyo, tumekwama, lakini tunajitahidi, tuelewe wenzetu wametoka mbali sana.

Kwa hiyo, tuwavumilie, lakini hata hivyo katika wiki mzima hii, wiki mbili hizi nimekuwa na mazungumzo marefu na Mheshimiwa Balozi Halfani Mpango, Balozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo DR - Kongo hapa nchini na vile vile nimekuwa na mazungumzo na Balozi Ngilangwa, Balozi wetu wa DRC Congo na wanalisukuma hili suala na wote kwa pamoja naamini tutafanikiwa hivi karibuni. Jana tu wamenitaarifu kwamba suala hili la kuridhia Mkataba lilikuwa limewekwa katika orodha ya shughuli za Bunge la Jamhuri ya Kimokrasia ya Congo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Balozi Ngilangwa alikuwa anafuatilia. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba wote tukiridhia, basi mkataba, mradi na mamlaka itakuwa imeanza rasmi kwa nchi zote husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uharibifu wa misitu Mkoa wa Mbeya, Mheshimiwa Zambi amechangia na sana sana amezungumzia kuhusu *Chumwa range* kwa uchungu kabisa. Niseme tu Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuwa Mkoa wa Mbeya alipata taarifa kuhusu uharibufu huo kutoka kwa Mkuu wa Mkoa na alitoa maelekezo ambayo tutayafanyia kazi kwa pamoja na Mkoa, Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Makamu wa Rais. Nadhani pale ambapo mambo yameuzidi Mkoa, basi tutashirikiana katika hifadhi ya *Chumwa Range.* Lakini katika mazungumzo, vile vile ameulizia kuhusu upandaji miti maeneo ya wazi ya kiwanja cha ndege cha Songwe.

Niseme tu kwamba, Mheshimiwa Maua Daftari amenithibitishia kwamba hii shughuli ya kupanda miti katika maeneo yaliyo wazi ili kuzuia vumbi na kuleta mandhari nzuri katika kiwanja cha eneo wazi katika kiwanja cha ndege cha Songwe itaanza kufanyika katika kipindi cha mvua za masika kitakachoanza mwezi Novemba.

Lakini niseme tu vile vile kwa niaba ya Serikali, kwamba nawathibitishia wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwamba fedha zipo za kumalizia kiwanja cha ndege cha Songwe na mchakato wa kumpata mzabuni karibu utakamilika. Niseme tu kwamba kiwanja hiki vile vile kipo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Nawaeleza tu ndugu zangu wa Mbeya kwamba ni vyema Mkoa na kanda ujiandae na matumizi ya kiwanja hiki. Nilikutana na rafiki yangu mjini Arusha aliniambia: "Nimegundua dhahabu Mbeya." Nikamwuliza, eneo gani? Akasema, siyo dhahabu, isipokuwa kiwanja cha ndege cha Songwe. Akasema sasa nanunua ardhi ili nihamie huko. Basi nawaeleza ndugu zangu wa Mbeya jinsi wengine wanavyokichangamkia kiwanja hicho.

Uchafuzi kutokana na viwanda hasa *KTM Karibu Textile Mills,* niseme kwamba, kabla ya mwaka 2005 viwanda vingi hapa nchini vilijengwa bila kuzingatia umuhimu wa

tathmini ya athari kwa mazingira. Lakini Sheria ya mwaka 2004 inaitaka *NEMC* ivifanyie ukaguzi viwanda hivyo.

Kwa hiyo, *Karibu Textile Mills* imetakiwa na imeandaa mpango wa usimamizi wa mazingira, yaani *environmental management plan* na imeandaliwa na *Clean Production Center* ya Tanzania, Kituo madhubuti kabisa cha kwetu.

Kamati ya kusimamia utekelezaji inahusisha *NEMC*, Wizara ya Maji na Manispaa ya Temeke, tutaisimamia hiyo *Karibu Textile Mills* kwa karibu sana. Vinginevyo, *NEMC* itachukua hatua za zuio *au prohibitory order.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niseme mambo ya msingi tu kuhusu mazingira. Kila mwananchi na mtu yeyote aishiye Tanzania ana haki ya kuishi katika mazingira mazuri, safi na salama. Vile vile kila mwananchi, vikundi na jamii kwa ujumla wana nafasi na haki ya kuhusika katika maamuzi au kuyapinga maamuzi ambayo yanakwenda kinyume na maslahi yao na maslahi ya Taifa katika suala zima la hifadhi na usimamizi wa mazingira. Kila mwananchi ana haki na wajibu wa kuhusika katika sera, mipango na mchakato mzima wa usimamizi na hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile msingi mwingine ni pale ambapo uwezekano upo kwamba matumizi ya maliasili na uchafuzi wa mazingira unaweza ukaleta madhara ambayo inakuwa vigumu kuyarekebisha, hivyo kukosekana kwa uhakika wa taarifa za kisayansi. Haiwezi kuwa sababu ya kutochukuwa hatua za tahadhari za kulinda mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, mazingira ni urithi wa pamoja wa kizazi cha sasa na vizazi vinavyokuja, au kwa maneno mengine, tumerithi mazingira kutoka kwa watoto wetu, wajukuu zetu na vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja yetu jioni ya leo. Wachangiaji walikuwa ni wengi sana na ninapenda nichukue nafasi hii kuwashukuru wote kwa dhati kwa michango yao mizuri sana ambayo nataka niwahakikishie tutaifanyia kazi katika kuboresha masuala ya muungano na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wa maandishi wako 37 na wachangiaji waliozungumza wako 10. Kama ilivyo ada nitaomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Naanza na waliochangia kwa maandishi. Mheshimiwa Khamis Seif, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Dr. Wilbroad P. Slaa, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid na Mheshimiwa Omar Ali Mzee. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini na Mheshimiwa Suzan A.J. Lyimo. *(Makofi)*

Waliochangia kwa kuzungumza ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Anastazia J. Wambura - Mwakilishi Kamati ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno - Mwakilishi wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala. Mheshimiwa Riziki Omar Juma - Msemaji wa Kambi ya Upinzani juu ya Masuala ya Muungano, Mheshimiwa Suzan A.J. Lyimo - Mwakilishi wa Kambi ya Upinzani juu ya Mazingira, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir - Mbunge wa Matemwe, Mheshimiwa Ibrahim Mohammed Sanya, Mheshimiwa Dr. Omar M. Nibuka, Mheshimiwa Sameer I. Lotto, Mheshimiwa Col. Saleh Ali Farrah na Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nataka niseme kwamba ni faraja kubwa sana kuona kwamba wananchi wote wa Tanzania wanapenda Muungano wetu uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo imethibitika hivi karibuni wakati wa kuadhimisha miaka 43 ya muungano wananchi wengi waliohojiwa na wote walikiri kwamba muungano wetu una faida na wangependa uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hivyo tu, hata ndugu zetu wa Kambi ya Upinzani nao vile vile wangependa Muungano wetu uendelee. Aidha, sote tunakiri vile vile kwamba muungano wetu una matatizo. Kuna kero ambazo lazima tuzishughulikie. Hii sio siri, ni jambo ambalo sote tunakiri na kwa hiyo tutafanya kila juhudi ya kuhakikisha kwamba kero hizo zinashughulikiwa kwa maslahi ya Taifa letu na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha ni kwamba Kambi ya Upinzani haitaki kukubali mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika kutatua kero hizo. Mimi napenda niwasihi ndugu zetu kwamba kwenye mafanikio wakubali na wapongeze juhudi za Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nithibitishe kwamba yapo mafanikio makubwa juu ya masuala ya Muungano yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka mmoja tu wa Serikali ya Awamu ya Nne. Mafanikio hayo yako katika maeneo saba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tuna tatizo hapa la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kushindwa kufanya kazi zake upande wa pindi wa Muungano yaani Zanzibar. Ndugu zetu wa upinzani walilisemea hili kwa uchungu mkubwa kwamba ni kwa nini iwe hivyo? Serikali hii kupitia vikao vyetu vya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi lilishughulikia suala hili. Leo nafurahi kusema kwamba matatizo yaliyokuwepo yalirekebishwa na sasa Tume hii inafanya kazi zake pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mafanikio na hayana budi kupongezwa na pande zote mbili. Tatizo lililokuwepo katika utendaji wa Tume hii lilikuwa ni kwamba Sheria tuliyokuwanayo ilikuwa haimtambui Waziri anayehusika na masuala ya Utawala Bora Zanzibar na kwa hiyo, Waziri huyo hakuweza kufikisha ripoti za Tume hii katika Baraza la Wawakilishi. Kwa kutambua hilo, Bunge lako Tukufu lilifanya mabadiliko ya sheria hiyo na sasa hivi suala hili kama nilivyosema limekwisha. Tume inafanya kazi zake pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo tumepata mafanikio na tumelimaliza katika kipindi hiki kifupi, ni suala zima la uvuvi katika ukanda wa bahari kuu, yaani *dips fishing authority.* Nchi yetu haina bahari kuu mbili, ina bahari kuu moja. Kwa hiyo, awali ilikuwa kuna mamlaka za pande mbili zinazofanya kazi ya kutoa leseni na kadhalika. Pande zote mbili kwa bahari hiyo hiyo moja kuu. Ilikubalika kwamba iundwe mamlaka moja kama chombo cha Muungano kitakachofanya kazi kwa niaba ya pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hilo lilihitaji marekebisho ya sheria iliyokuwepo. Jambo hilo limefanyika. Sheria ililetwa katika Bunge lako Tukufu na ikapitishwa na tumemaliza suala hili kwamba sasa kutakuwa na mamlaka moja tu ya uvuvi itakayoundwa kwa ajili ya kushughulikia masuala ya uvuvi katika bahari kuu na tumekubaliana kwamba mgao wa mamlaka hii uwe kama ifuatavyo:-

Asilimia 50 ya mapato yake yatumike kwa ajili ya kuendesha mamlaka yenyewe. Asilimia 30 itumike kwa ajili ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na asilimia 20 ipelekwe Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Mgao tuliokuwa nao sasa hivi ni wa asilimia 4.5 kwa Zanzibar lakini ilionekana wazi kwamba suala la uvuvi, suala la bahari ni kiini cha uchumi wa Zanzibar ndiyo maana ikakubalika basi wapate asilimia 20. Hilo ni la pili katika mafanikio ndani ya kipindi cha mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu lililofanyiwa kazi na Kamati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi ni suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Suala hili halijakamilika. Lakini limefika pazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, si jambo la siri kwamba nchi nyingi zimegombana, zimepigana vita kwa sababu ya mafuta. Sio suala la kuharakisha, ni suala la kuhakikisha kwamba ufumbuzi wa kudumu unapatikana. Kamati ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi imepata muafaka ufutao:-

Kwanza, atafutwe Mshauri Mwelekezi wa kuzishauri Serikali zetu mbili juu ya namna bora ya kugawana rasilimali itokanayo na mafuta na gesi asilia. Mshauri Mwelekezi huyu kwa nini anatafutwa? Ni kwa sababu masuala ya mafuta katika nchi zenye Muungano, siyo Tanzania tu, ni vyema tukapata utaalam na uzoefu wa nchi nyingine. Nitatoa mifano, nchi nyingine zenye Muungano. Mathalani, *United Arab Emirets* ni nchi yenye Muungano na ni nchi yenye mafuta. Mfano mwingine ni Uingereza. Kule *North Sea* upande wa *Scotland* wa mafuta na wao wameungana.

Mfano mwingine ni *Canada, Qubec* na *Canada* huku wameungana na kuna mafuta. Kwa hiyo, Mshauri Mwelekezi huyu atatupa uzoefu wa wenzetu wamefanyaje katika suala hili kwa madhumuni ya kupata ufumbuzi wa kudumu juu ya mafuta. Mafuta ni rasilimali ambayo inaweza ikatusaidia sana lakini tusipoangalia mafuta ni rasilimali ambayo inaweza kutugombanisha. Kwa hiyo, ni jambo la msingi kabisa kuhakikisha kwamba jambo hili linafanywa kwa utaratibu unaokubalika. *(Makofi)*

Tunavyozungumza, Hadidu za Rejea zimeshatayarishwa na baada ya Mshauri Mwelekezi kutupa taarifa hiyo, taarifa hiyo itajadiliwa na pande zote mbili za Muungano kwa madhumuni ya kupata muafaka juu ya namna bora ya kugawana rasilimali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la nne lililopata muafaka katika kipindi hiki ni suala la fedha. Masuala mazima ya fedha, Muungano wetu kero nyingi tunazozisikia zinahusu masuala ya uchumi. Tukaona kuna umuhimu basi wa kushughulikia masuala hayo kwa ukubwa wake, sio moja moja, ndiyo maana ninazungumzia sasa masuala ya fedha kwa ujumla wake. Kuna maeneo matatu ambayo yamefanyiwa kazi.

Kwanza, kuna eneo zima la mgao wa misaada, mgao wa misamaha wa madeni, mgao wa faida ya Benki Kuu kwa Serikali zetu mbili. Kama tunavyotambua sote, wengi wenu mmechangia kwamba kwa nini bado ni asilimia 4.5. Sasa kuna chombo maalum kinachoitwa *JFC Joint Finance Commission* iliyopewa kazi ya kufanya kazi mbili tu. Kwanza ni kutafuta njia bora ya kugawana rasilimali za Muungano na pili, ni kuangalia jinsi gani pande zote mbili zitachangia gharama za Muungano. *JFC* imefanya kazi yake na imefikisha taarifa yake Serikalini kama walivyotangulia kusema wenzangu kwamba *JFC* imetoa hiyo ripoti na hiyo ripoti lazima ishughulikiwe kwa pande zote.

Hivi tunazungumza Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa upande wa Muungano umetayarishwa. Ni mategemeo yetu kwamba itakuwa hivyo hivyo kwa upande wa *SMZ* ili hatimaye tupate muafaka wa jinsi bora wa kugawana rasilimali za Muungano na kuchangia gharama za Muungano. Nnaomba Waheshimiwa Wabunge mliochangia katika hili mvute subira kwa sababu hatima ya jambo hili itakuwa ni msingi mzuri wa kuondoa kero nyingi zinazotukabili katika Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili katika fedha ni suala la mkakati wa pamoja wa misaada Tanzania, yaani *Joint Assistence Strategy for Tanzania.* Hili lilikuja kutokana na malalamiko mengi yaliyokuwepo kwamba pengine misaada ya miradi haisaidii kwa upande wa Zanzibar. Kulikuwa kuna wengi wanalalamikia hili. Ikaonekana kwamba uundwe huu mkakati maalum wa pamoja kwa maana kwamba kuna

wajumbe kutoka pande zote mbili. Kwa kila mradi utakaopitishwa wenye fedha za wafadhili lazima kuwe kuna *component* ya Zanzibar vile vile. Nafurahi kusema kwamba miradi kadhaa imekwishaingiwa katika utaratibu huu. Moja, nikitoa mifano. Ni suala zima la *ASBP Agricultral Sector Development Programme*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Kilimo Zanzibar itapata fedha kutokana na mpango huu. Mradi mwingine ambao umepangiwa fedha ni *Millenium Challenge Account* ni mradi ambao Tanzania imepeleka miradi yake ambayo inatakiwa ikiwemo barabara, maji na kadhalika na kuna *component* ya Zanzibar vile vile.

Eneo lingine ni *TASAF*. Hili sio geni, sote tunafahamu kwamba fedha za *World Bank* lakini zinafaidisha pande zote za Muungano bila matatizo yoyote. Eneo lingine ni mradi wa *Marine and Coastal Environmental Management Project,* yaani *MCEMP*. Huu ni mradi ambao utakuwa pande zote mbili za Muungano na vile vile kuna mradi wa *Zanzibar Basic Education Improvement Project,* ni mradi wa dola za Kimarekani milioni 42 ambao ndiyo sawa na ule mradi wa *MMEM* uliokuwa kwa Tanzania Bara. *(Makofi)*

Kwa hiyo, lazima tukubali kwamba sasa malalamiko yale yaliyokuwa yanaelezwa kwamba Zanzibar hawafaidiki na miradi ya wafadhili sio kweli. *Just* imeondoa kwa sababu sasa tunapanga miradi hiyo kwa pamoja. Eneo la tatu katika upande wa Fedha, ni suala zima la kodi la Ushuru wa Forodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamezungumzia hapa kwamba sio vyema kwa mtu kuleta bidhaa kutoka Zanzibar kuja Tanzania Bara akatozwa tena ushuru. Suala hili limeshughulikiwa na Kamati ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi.

Tumekubaliana kwamba iundwe Kamati yenye Wajumbe kutoka Wizara za Fedha za pande zote mbili kushughulikia ni kwa nini matatizo haya yapo, walete taarifa kwenye Kamati yetu ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi ili tupate ufumbuzi. Na ninafurahi kusema kwamba Kamati hiyo imeundwa, lakini kikubwa hapa ni kuoanisha kodi za pande mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani hata siku moja kwamba upande mmoja wa Muungano watu walipie kasoro halafu wachukue bidhaa zile walete upande wa pili, itaua ukusanyaji wa ushuru upande wa pili. Kwa hiyo, imeonekana kuna umuhimu kwamba sasa kodi ziwe sawa pande zote mbili ili kero ya kutozwa mara mbili iondoke, lakini vile vile kusiwe na mwanya kwamba mtu anapitishia Zanzibar ili alete hatimaye Tanzania Bara. *(Makofi)*

Wenzetu wa *TRA* wamefanya kazi moja ya kufunga mtandao unaoitwa *Ascudor plus plus.* Waheshimiwa Wabunge nimezungumza nao wanasema pamoja na kufungwa huko bado kuna matatizo. Hayo ni matatizo ya utekelezaji na nitatolea ufafanuzi baadaye kidogo. Lakini kuna suala la usajili wa magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili liko wazi kabisa na wenzetu wa Wizara ya Fedha wamesema kwamba sasa hivi sheria tulizokuwa nazo za usajili wa magari ni mbili tofauti kwa pande mbili. Zanzibar wana sheria yao na Serikali ya Muungano wana Sheria yao. Lakini ni suala linalozungumzika. Tunachosema ni kwamba kama tuliweza kubadilisha sheria kufanya marekebisho ya Sheria ya Tume za Haki za Binadamu na Uvuvi katika bahari kuu, hakuna sababu kwa nini na hili lisizungumzwe.

Wenzetu wa Zanzibar wamezungumza kwa uchungu kwamba haifai kwa mtu kuleta gari yake na *ZNZ* akaonekana kama vile kaleta kutoka nchi za nje. Nakubaliana nao na nataka niwahakikishie kwamba hili ni suala ambalo linaweza likazungumzwa kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika eneo la tano la mafanikio katika kipindi cha mwaka mmoja, ni suala la ushiriki wa Zanzibar katika shughuli za kimataifa. Kulikuwa kuna malalamiko kwamba Zanzibar inawakilishwa vipi katika shughuli za Mataifa, ni kweli katika mapatano ya Muungano, masuala ya Kimataifa, masuala ya ushirikiano wa Kimataifa ni masuala ya Muungano. Sasa kulikuwa kuna malalamiko kwamba pengine Zanzibar haiwakilishwi vizuri. Kamati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi imelifanyia kazi suala hili. Vilevile na tumepata muafaka mzuri sana. Tumekubaliana yafuatayo:-

Kwanza, misafara ya kuwakilisha nchi katika Mikutano yote iwe ya *East African Community*, *SADC*, *AU*, *UN Agencies* kote, lazima iwe na wataalamu au viongozi kutoka pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Pili, maeneo yote yenye faida ya kiuchumi yaorodheshwe ili Zanzibar na wao wapate mgao wao. Hili limepelekea suala la *IMO International Martium Organisation* iliyoonekana kwamba Zanzibar wanataka uanachama kama Zanzibar katika taasisi haikuwezekana kwa sababu ni kinyume na Katiba na Taratibu. Suala la ushiriki katika Taasisi za Umoja wa Mataifa ni suala la Muungano. Lakini kilichokuwa kinaleta bughudha ni kwamba, pengine kuna faida za kiuchumi ambazo Zanzibar inakosa. Sasa tumekubaliana ziorodheshwe faida zote za kiuchumi zinazotokana na *IMO* na Wizara ya Miundombinu, imeambiwa ikae pamoja na Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar waainishe ni maeneo gani ya kuweza kupata faida kwa pande zote mbili.

Maeneo kama leseni za meli, maeneo kama mafunzo, maeneo kama miradi ya miundombinu na kadhalika. Hilo limefanyika na tutaendelea kulifuatilia kuhakikisha kwamba Zanzibar inapata mgao wake. Lakini sio *IMO* peke yake, sasa kuna masuala makubwa kuhusu *East African Community. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar kama nilivyosema lazima iingie pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika *East African Community* kwa sababu ni suala la Muungano. Lakini kama hoja ni kwamba pengine Zanzibar itapunjika kutokana na miradi limeshughulikia pia miradi ifuatayo, kutoka Zanzibar itaingizwa katika miradi ya Afrika Mashariki. Masuala ya uboreshaji wa Bandari, masuala ya uboreshaji wa viwanja

vya ndege, masuala ya umeme kwa maana ya *East African Power Master Plan,* yote yatakuwa ni miradi ya Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Sasa ukitazama utaona kwamba suala zima la pengine Zanzibar kupunjika na kuwa ndani ya Muungano, hapa Kamati hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi imefanya kazi kubwa sana ya kutatua kama nilivyoeleza. Lakini kuna suala la *SMZ* kujiunga na *FIFA*.

Ni kweli kwamba wenzetu wa Uingereza, England imeingia peke yake na Scotland imeingia peke yake. Pengine basi kwa *FIFA* suala hilo linakubalika. Sasa hilo sio suala la jazba ni suala la kukaa chini kuzungumza na kukubaliana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi naweza kusema katika hili kwamba mazungumzo yataendelea na bila shaka mzungumzaji alisema sahihi kwamba pengine *ZFA* kuingia *FIFA* wanaweza wakapata misaada ikanufaisha zaidi kuliko tunavyopata hivi sasa kwa upande mmoja. Kwa hiyo, hili tunasema linazungumzika wala sio suala ambalo linaweza likaleta kero katika Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije sasa katika upande wa suala la sita katika mafanikio ya kipindi cha mwaka mmoja. Ni suala la miradi ya pamoja kwa pande zote mbili za Muungano. Kulikuwa kuna malalamiko kwamba mbona miradi haifanyiki kwa pamoja? Ipo! Mradi wa *TASAF* kama nilivyoutaja, umefika Pemba, Unguja na uko katika mikoa na wilaya zote za Tanzania Bara na unafanya kazi nzuri na Waheshimiwa Wabunge mnakubali hilo. Mradi wa *SELF*, huu unashughulika na mikopo ya wajasiliamali wadogo wadogo, upo pande zote za Muungano na hata zile fedha mpya za Mheshimiwa Rais Kikwete, yale yanayoitwa mabilioni ya Kikwete sio kwamba yataishia Tanzania Bara peke yake, hata Zanzibar yatafika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nadhani tukisema kwamba hizi kero kama Msemaji wa Kambi ya Upinzani alivyosema sio sahihi, nasema lazima tufike sehemu tukubali kwamba kuna mambo makubwa yamefanyika ndani ya kipindi kifupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la saba na la mwisho ni vikao vya ushirikiano kwa masuala yasiyo ya Muungano. Ofisi yetu Kamati ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi sio kwamba inatizama kero tu za Muungano, kuna maeneo ya ushirikiano ambayo sio ya Muungano. Nataka nitoe taarifa kwamba Wizara 14 zimefanya vikao vya ushirikiano, Wizara 14 kati ya pande mbili zetu. Madhumuni ya vikao hivyo ni kubadilishana uzoefu. Tunajua fika kwamba uzoefu unatofautiana kubadilishana wataalam. Kuna maeneo ambayo wataalam wake, kwa mfano huku upande wa Tanzania Bara, watalaam ni wengi katika nyanja nyingi ikiwemo afya, elimu na kadhalika. Mawaziri hawa wanakutana, wataalam wanakutana kwa madhumuni ya kuongeza ushirikiano kwa maeneo ambayo pia sio ya Muungano.

Naomba vilevile nieleze hapa kwamba kuna suala la elimu kama ndugu aliyesema Col. Farah hapa mwisho, anasema kwanini Wizara ya Elimu isiwe moja tu? Kwa hivi sasa sio moja na ni kwa sababu elimu ya msingi haiko katika maeneo yale 22 ya Muungano. Lakini ushirikiano ni mkubwa sana. Sasa hivi kuna suala la kuzungumza

kuoanisha mitaala kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Ili fursa iwe moja, mtakumbuka kwamba mtihani wa *Form Four* unatungwa na Baraza la Mitihani.

Kama mitaala haiko sawa, ndugu zetu wa Zanzibar lazima wao watakuwa na fursa ambayo ni pungufu kwa sababu hawana mitaala inayofanana na mtihani ule unaotungwa. Kwa hiyo, hili ni suala ambalo linazungumzwa na bila shaka nina uhakika Wizara zetu mbili za elimu zitapata ufumbuzi katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba maeneo hayo saba niliyoyataja yamefanyika ndani ya kipindi cha mwaka mmoja. Nawaomba ndugu zetu wa upinzani wakiri pale ambapo mafanikio yamepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikao hiki cha Kamati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi hakitaishia katika kutoa maamuzi tu, hatua inayofuata kutazama na kuratibu utekelezaji, ndio maana tumekubaliana kwamba kikao kinachofuata cha Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi kisije na *agenda* mpya badala yake tupitie maeneo yote ambayo tulishayatolea maamuzi hii maana yake ni nini? Maana yake kama bado kuna matatizo ya kiutekelezaji kama wanavyosema ndugu zetu pale kwamba pamoja na *ASKUDA* bado kuna bugudha, hapa yataonekana katika kupitia maamuzi.

Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba bila shaka kikao hicho kinachofuata kitatizama maeneo yote ambayo yameshafanyiwa uamuzi lakini bado kuna kasoro za kiutendaji ili nazo zishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba kulikuwa kuna maswali mengine kwamba Zanzibar ipewe fursa kamili ya kushiriki kutafuta misaada ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar haikatazwi kutafuta misaada. Unapozungumzia *bilateral donors*, Zanzibar ina uwezo huo na mifano ipo. Zanzibar imezungumza na Serikali ya Japan na imepatiwa msaada kwa ajili ya maji ya Mkoa wa Mjini Magharibi moja kwa moja. Kuna mfano mwingine, Zanzibar imezungumza na Serikali ya Norway itapatiwa *sub marine cable* ya umeme kutoka Tanga mpaka Pemba. Kwa hiyo, hakuna suala la kukatazwa kufanya mazungumzo ya moja kwa moja na *bilateral donors,* hata sio kweli. Hili lilichangiwa na Mheshimiwa Ali Khamis Self. Lakini kuna eneo lingine Wabunge wengi walitaka kujua kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar itajengwa, lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahikishie kwamba, fedha katika mwaka huu wa fedha zimetengwa kiasi cha shilingi milioni 324 zitazoanza ujenzi lakini hatutasubiri ofisi hii ikamilike, tutakodi sehemu Zanzibar ili Ofisi ya Makamu wa Rais upande wa Zanzibar ianze kazi zake mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Juma Said Omar, alikuwa anasema Muungano wetu zaidi ya miaka orobaini na mwanzo ulikuwa na vipengele 11 na sasa hivi viko zaidi ya 30 na utaratibu wa kuongezwa umekuwa holela sio kweli. Vipengele kweli vilianza 11, sasa hivi viko 22

kwa mujibu wa nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na kuna utaratibu wa kikatiba wa kuongeza au kupunguza vipengele, hivyo na utaratibu huo ulitumika kutoka hiyo 11 mpaka 22, kwamba lazima theluthi isiyopungua mbili ya Wabunge ya kura za Wabunge za pande zote mbili zipitishe jambo lolote la kubadilisha ile orodha ya masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna suala lingine alilouliza Mheshimiwa Bujiku Sakila, yeye aliomba Serikali zetu zikae na kuangalia uwezekano wa kuziunganisha Serikali hizi kuwa moja tu. Kwani Serikali mbili na dhana itaondoa masuala ya kero za Muungano. Mheshimiwa Bujiku Sakila napenda nimuarifu au niseme kwamba kwa sasa sera ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni ya kuwa na Serikali na kuimarisha Muungano na tutaimarisha Muungano na Mashirikiano kati ya Serikali zetu na Serikali itaendelea kushughulikia kikamilifu vikwazo vinavyojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano.

Kama nilivyosema awali kwamba wachangiaji walikuwa wengi na sio rahisi kuweza kuyajibu yote haya, lakini nitaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaandika, tutaleta kwa maandishi ili tuweze kujibu maswali yote yaliyoulizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema, sasa naomba nitamke kwamba naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 26 – Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 – *Administration General* …Tshs. 2,465,419,000/=

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu 10 *Sub-vote* 1001 *item* 250100 Mshahara wa Waziri.

**NAIBU SPIKA:** Nimekwambia hii ni ofisi ya Makamu wa Rais, Mshahara wa Waziri haupo hapa bwana, ni nyumbani kwake na mambo ya binafsi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 – *Administration General* … Tshs.2,505,734,700/=

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu 10 *Sub-vote* 1001 *item* 250100 - Mshahara wa Waziri. Wakati Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wanachangia hapa waligusia juu ya Tanzania kujiunga na *OIC*. Kama tunavyojua kwamba Zanzibar iliwahi kutaka kujiunga na *OIC,* lakini kwa sababu moja au nyingine haikuweza kufanya hivyo na Rais wakati ule Salmin Amour alisema kwamba suala hili analiachia kwa Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyozungumzwa hapa ni kwamba *OIC* inanufaisha watu wa itikadi zote katika nchi kama Uganda, Malawi na hapa Tanzania, ingelikuwa ni hivyo hivyo. Sasa ningependa kupata ufafanuzi ni lini basi Tanzania itajiunga na *OIC* ili nasi kupata maslahi hayo tunayotarajia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Zanzibar haikuweza kujiunga kama Zanzibar katika Jumuiya hiyo kwa sababu hilo ni suala la kimataifa na ilitolewa taarifa kwamba Tanzania kama Jamhuri ya Muungano itakapokuwa tayari, basi suala hilo litafanyika. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa avute subira mpaka hapo nchi itakapokuwa tayari kujiunga na taasisi.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijatosheka na jibu la Mheshimiwa Waziri kwa sababu naona suala hili halihitaji gharama kubwa, labda bajeti yetu mara hii sio nzuri tusubiri mwaka ujao. Labda kuna vipingamizi gani ambavyo vinasababisha hadi leo tusijiunge?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba suala hili linahitaji maamuzi ya Serikali na kwa maana hiyo ni kwamba endapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa imelipitisha na Serikali ya Jamhuri ya Muungano iwe imelipitisha na kwa pamoja tukubaliane kwamba tutajiunga na taasisi hii ndipo tutaweza kufanya hivyo. Mpaka sasa hivi jambo hilo halijapitishwa rasmi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila kabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance Accounts* … … … Tshs.188,740,000/=
Kifungu1003 - *Policy and Planning* … … Tshs.418,395,800/=
Kifungu 1004 – *Information, Education, Communication Unit*... ... ... Tshs.157,655,200/=
Kifungu 2001 – *Union Secretariat* … … .. Tshs.28,024,804,100/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu5001 – *Environment*… … … … … Tshs.4,195,019,200/=

**MHE. DR. OMAR MZERU NIBUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa taarifa ni kwamba kwetu sisi mimi ndio mrefu kuliko wote na kukiwa na kitu kipo juu zaidi, basi mimi ndio natumwa kama sikuweza mimi basi tunatafuta Polisi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 50 *sub-vote* 5001 kifungu kidogo cha 250100, mshahara wa Waziri. Nilipokuwa natoa ufafanuzi hapa nilimweleza Mheshimiwa Waziri kuhusu mazingira kwamba milima ya Ulunguru kwanza ni...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, mshahara wa Waziri unakuwa kwenye *vote* ya kwanza kabisa. Hapa wewe tumia kifungu hicho bila kutumia mshahara wa Waziri. Waziri hapa hayupo *departimental office.*

**MHE. DR. OMAR MZERU NIBUKA:** Nakushukuru sana. Nilipokuwa natoa maelekezo kwa Mheshimiwa Waziri, kwanza nilimweleza kwamba milima ya Uluguru inachukua sehemu kubwa. Kuna Majimbo mengi sana ambayo yanaunganika katika milima ya Uluguru...

**MWENYEKITI:** Sasa kifungu gani katika hapo?

**MHE. DR. OMAR MZERU NIBUKA:** Programu 50 *subvote* 5001 250100.

**MWENYEKITI:** Sasa wewe ukimnyang'anya mfanyakazi mdogo hana mamlaka yeye wala hana maamuzi? Unaiona tofauti? Hapa ni swali la sera, huwezi kumwuliza mfanyakazi tu Mkuu wa *Department* hii, ambayo unamchukulia mshahara wake na wafanyakazi wengi wote, sasa ndio unachotaka kufanya?

**MHE. DR. OMAR MZERU NIBUKA:** Nilikuwa naomba maelezo.

**MWENYEKITI:** *No,* tafuta ki-*sub-vote* huku unachokijua. *Sub-vote* gani katika fungu 50?

**MHE. DR. OMAR MZERU NIBUKA:** Kuhusu *environment*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hebu tuzungumze. Ndio maana tunasema hivi, naomba ukae kidogo. Tunapoingia kwa mfano katika Wizara ya Makamu wa Rais na Mazingira, tunapochukua mshahara wa Waziri pale tunazungumza mambo ya sera.

Sasa katika masuala ya sera kweli Waziri anahusika kwenye mambo ya sera na Baraza la Mawaziri anahusika na mambo ya sera, ukija kwa Mkurugenzi, Mfanyakazi wa *department* ya mazingira ukimweleza habari zozote zile, yeye ni mtekelezaji tu. Ndio maana hapa uwe labda na *sub- vote* hapa katikati, tutakuruhusu. Lakini mshahara wa hawa wafanyakazi hapana.

**MHE. DR. OMAR MZERU NIBUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi hoja yangu ilikuwa ni kwamba wakati ulikuwa unatoa maelezo.....

**MHE. SAMER L. LOTTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi bado tunajifunza na kwa bahati mbaya leo hatujazungukwa na makada ambao wangetuelekeza. Lengo lilikuwa kupata ufafanuzi katika maelezo tuliyotoa ambayo hatukuridhika na majibu ya Waziri pengine kama tunaweza kubana mahali pengine. Naomba utuongoze. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Kwa bahati mbaya, kwa mujibu wa taratibu zetu hamna sehemu nyingine. Hilo ni swali la sera ambalo nyinyi mmechelewa kujifunza kule mlikotakiwa kutangulia. Lakini kwa upendeleo kwa sababu ya kujifunza nawaruhusu suala moja tu, hebu uliza sasa bila kifungu chochote. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. OMAR MZERU NIBUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ufafanuzi wangu ni kwamba wakati nikiwa natoa hoja kuhusu watu wangu wa Jimbo langu la Morogoro Mjini kwa maana ya Manispaa ya Morogoro kuhusiana na milima ya Uluguru nilimweleza Mheshimiwa Waziri kwamba milima ya Uluguru kwanza inachukua eneo kubwa na eneo hili linachukua karibu Majimbo mengi tu na nilikuwa nimemtajia Mimbo moja moja. Lakini pia milima hii ya Uluguru sisi kama Manispaa ya Morogoro tunachukua sehemu ndogo sana ya milima hii.

Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu hoja akasema kwamba milima hii ina umuhimu kwa sababu kuna wanyama ambao sehemu nyingine hawapatikani, lakini pia ni vyanzo vya maji kwa Mji wa Dar es Salaam. Sasa mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri katika Manispaa ya Morogoro sisi hatuna mnyama hata mmoja ambaye yeye anaona ni mnyama ambaye hayupo katika sehemu nyingine.

Sasa asichanganye sehemu nyingine kwa sababu ule mlima ni mkubwa unakwenda mpaka Kisaki, unakutana na pori la Selous. Mimi nazungumzia sehemu yangu ya Morogoro Mjini. Hilo la kwanza. Lakini kama suala la muhimu wa maji kwa ajili ya Dar es Salaam, milima ya Uluguru nilimwambia kwamba iko mito ambayo kwa muunganiko wake inaingia katika mto Ruvu Juu, inaingia Ruvu chini na kwenda Dar es Salama na mito hiyo nimemtajia kwa majina uko Mto unaitwa Mto Mbezi, Mto Mvua, Mto Kisiki, Mto Mmanga na Mto Mfizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mito hii yote iko Morogoro Vijijini, haihusiani na Morogoro Mjini na iko mbali. Sisi Morogoro Mjini hatuna *connection* ya moja kwa moja na Dar es Salaam, sisi mto wetu ni mdogo, mto wa Morogoro unaingia mto wa Ngerengere na huu mto wa Ngerengere asili yake unatokea Kilosa. Sasa anapongumzia sisi watu wa Morogoro kwa ajili hiyo, ni kama kutuingiza katika kapu lisilotuhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilimwambia kwamba sisi kule milimani kunazalishwa mazao ambao vijana wa Morogoro ambao hawana ajira kwa kutumia mazao hayo wanalangua kwa wakulima kule wanajitafutia riziki na kupata ajira yenyewe ya kujiajiri Mjini ambao kwa kufanya hivyo wasichana na wavulana wanaepukana na maambukizo ya Ukimwi. Sasa anapotaka kuzungumzia kwamba watu wa kule lazima watashuka, sasa hajanifafanulia kwamba hawa watu wengine ambao wataathirika watafanya nini? Kwa hiyo, nilikuwa naomba majibu kutoka wka Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya ndugu zangu, Waheshimiwa Lotto na Mheshimiwa Mzeru kwa kuzungukwa leo na makada lakini pamoja na hiyo nitajitahidi kutoa ufafanuzi wa ziada.

Ni kweli Mheshimiwa Mzeru eneo analolizungumzia ni eneo ambalo ukitoka Dodoma zile safu za milima wanayoiona kwanza naweza kusema ni usoni. Mimi nilichozungumzia ilikuwa ujumla wa safu za milima ya Uluguru ikiwa ni pamoja na eneo hilo analolizungumzia Mheshimiwa Mbunge.

Ni kweli vile vile kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, eneo analolizungumzia liko katika Manispaa ya Morogoro. Ni kwa sababu hiyo, ambayo kutokana na matumizi kidogo ya ardhi na mipango ya Manispaa ya Morogoro inabidi ndugu zetu hawa wahame. Na sio hivyo tu, kumetokea na mazungumzo mengi baina ya viongozi wote wa vijiji wa Kata, wazee, viongozi wa jadi, watu mashuhuri pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenyewe. Hizi ni taarifa nilizozipata mchana huu kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro. Ilitokea hoja hapa kwamba Waheshimiwa Wawakilishi walikuwa hajawahusishwa au hawahusishwi katika maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niseme kwa kweli kwa kuwatetea viongozi wa Morogoro kwamba sio hivyo na wameweza kuniorodheshea siku hata vikao ambavyo Waheshimiwa Wabunge wenyewe walihudhuria.

Niseme vile vile kwamba, katika orodha ya viongozi wote waliohusika walikuwemo viongozi wa Chama Cha Mapinduzi katika ngazi za vijiji na katika ngazi za Wilaya. Kwa hiyo, haya ni maamuzi ya pamoja. Sasa nini ambacho kinatokea katika eneo analolizungumzia Mheshimiwa Dr. Mzeru, eneo hilo ambalo anasema ni eneo la milima usoni kama ukitoka Dodoma, wale wananchi wamepatiwa maeneo katika Kata ya Kihonda eneo linaitwa Kegea na mazungumzo bado yanaendelea kwa maana ya katika hii njia shirikishi ambayo nimetaja ya kuwahusisha viongozi pamoja na wananchi ili katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais na agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja pale Morogoro, basi wananchi hawa waweze kupata fidia waweze kuonyeshwa mahali pa kuhamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa imezungumzwa kuhusu kilimo kinachofanyika kule juu. Nimesema hapa kwamba, hiyo vile vile ni hoja mojawapo ya kuwaomba ndugu zetu hawa washuke kwa sababu jinsi watu watakavyozidi kule juu, basi ndivyo hivyo, achana na Dar es Salaam kwa maana ya upande wa vyanzo vya maji upande wa Morogoro Vijijini ambako nilieleza nimeshafika mara nyingi lakini ukichukua sasa kwa milima ya Uluguru upande huu wa usoni ninaosema ni chanzo cha maji kwa mji wenyewe wa Morogoro. Kwa hiyo, Morogoro yenyewe kama Manispaa itafaidika katika kipindi cha muda wa kati na kipindi cha muda mrefu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu washirikiane na Uongozi wa Mkoa katika kufanikisha zoezi hili. Tunajua halitachukua mwezi mmoja, litachukua muda, lakini madhumuni yetu yawe ni yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya kazi moja na kama nilivyosema hili suala la usimamizi wa mazingira ukitaka kupata umaarufu kwa maana ya kupendwa, haiwezekani. Ni suala gumu, lakini masuala magumu yana faida kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kifungu1001 *Administration and General* …………Sh.2,936,300,000/=

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Sub-vote* 1001, kifungu kidogo 6309 na kile kingine cha 6389, inaonyesha kwamba *vote* zote hizi mbili ni kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar. Naomba kujua kwa nini hizi *vote* mbili zote zinashughulikia kitu kimoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha zinashughulikia ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais sehemu tofauti za Muungano. Kuna makosa hapa. Hii ya kwanza ya Sh.365,000,000/= ni ujenzi wa Ofisi ya Makamu Rais Zanzibar na hii ya pili ya Shilingi bilioni 2.6 ni kumalizia ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Dar es Saalaam.

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Naomba urudie tena.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *construction of Vice President Office and Residence Zanzibar* Sh. 324,800,000/= hizi ni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar. Halafu hii Shilingi bilioni 2.6 ni kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Dar es Salaam.

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan tuko sawa?

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Sawa!

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Tunakushukuru kwa kuonyesha hilo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumuzi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 *Environment* ……………...……..............10,675,400,000/=

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote 31, sub-vote 5001.* Katika mchango wangu nilioutoa kwa maandishi, nilimtaka...

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Hebu rudia tena. Ni *sub-vote 5001* halafu…

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH:** Nimesema *vote 31, subvote 5001.*

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Haya *sub-vote* ndogo ipi?

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH:** Nazungumzia suala la uhifadhi wa mazingira katika Ziwa.

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Kuna vifungu vidogo vidogo pale kipi katika hivi?

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Ziwa ambalo halikutajwa hapa.

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Basi hamna. Hatufungui mjadala.

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH:** Eeh, *sub-vote 6569*.

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Sawa endelea.

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti….

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Hapa ni *Lake Tanganyika Environment Management Project.*

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH:** Eeh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia suala la maendeleo ya Ziwa Kitangiri linalofanana kabisa na Ziwa Tanganyika.

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge *I beg your pardon.* Hapa tunapitisha matumizi, hatuzungumzii kitu chochote, tulichozungumzia zamani. Unatakiwa uingie pale, kama ungetaka ungekwenda kwenye

*policy issue.* Sasa hapa *policy* inakwenda kwenye matumizi kabisa! Hii ni *Lake Tanganyika,* ukizungumzia hilo Ziwa lingine mbona halipo hapa?

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH:** Mazingira yenyewe yamezungumzia Ziwa na sisi tunazungumzia suala la maendeleo ya Ziwa.

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Usibishane na Kiti. Kwanza ulitakiwa kukaa chini wakati nazungumza.

Waheshimiwa Wabunge, tunapoingia katika *stage* hii ndio tuna-*finalize* zile hesabu mlizopitia kwenye Kamati zenu na alizosema Waziri. Kwa hiyo, hatuwezi kuleta *story* nyingine yoyote *unrelated.* Ukita *story* ndio tunaingia katika kifungu kile tunachosema cha *policy issue* pale mwanzoni, lakini ukiingia huku unazungumzia *a sub item*.

Kwa hiyo, ndio maana hapa hatuwezi kuingiza katika ile *Lake Kitangiri* kwa sababu haipo hapa. Kwa hiyo, naomba sana tuzingatie hilo.

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Eeh, tunaendelea na Mheshimiwa Kabuzi.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninazungumzia *vote 31, sub-vote 5001, item 6507 - NEMC*.

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Sawa.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, niliulizia suala la Matabe ambalo linategemea uamuzi wa *NEMC* kuishauri Wizara ya Nishati na Madini. Eneo la Matabe ni eneo lenye madini na Wizara ya Nishati na Madini ilionyesha nia ya kuwasiadia wachimbaji wadogo. Nafikiri baada ya maagizo ya Mheshimiwa Rais kwamba watafutiwe mahali pa kuweza kufanyia kazi zao, wakati wachimbaji wadogo wa Matabe walipoanza kuleta maombi yakapelekwa…

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Mheshimiwa hapa ni *specific project* ya *NEMC*. Wewe ungetaka kusema hayo ungerudi tena pale pale tulipoanza kuongelea Wizara katika *current expenditure* hapa ni *development,* ni mradi maalum wa *NEMC*. Kwa hiyo, huwezi kuzungumzia habari ya madini hapa sio penyewe.

Mnaona! Mkiangalia mambo ambayo hayako kwenye kitabu tunapoingia katika Wizara ile ni suala la sera. Sasa haya madini pia ni sera ya wachimbaji wadogo wadogo, lakini huwezi kuingia hapa, hapa sio penyewe tutakuwa tunazungumza tu.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa maelekezo yako, lakini shughuli iliyobaki ni *NEMC* inatakiwa itoe uamuzi kusudi ifanye shughuli hiyo. Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumzi imepitia bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais na asasi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe makisio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**MHE. ANNE S. MAKINDA – MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nina matangazo. Asubuhi wakati Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir anachangia hoja hii alitamka kwamba: "Hata kama Mheshimiwa Spika amekataza kutoa salamu za rambirambi, lakini nawajibika kusema kwa sababu wapiga kura wangu wamenipigia simu na hivyo nawawakilisha."

Sasa naomba kufafanua kwamba alichosema Spika sio kwamba msitoe salamu za rambirambi wakati unachangia hoja. Pale ni muda wako dakika kumi na tano zako unaweza kuwapongeza hao na kuwapa pole, hiyo sio ile iliyokatazwa. Iliyokatazwa ni wakati wa kipindi cha maswali na haijakatazwa kwa Wabunge tu wanaouliza maswali na Mawaziri wanaojibu. Huwezi kuanza kipindi cha maswali unaanza kusema habari za wapi sijui kwa sababu kanuni 34(1)(d), masharti kuhusu maswali. Kifungu 34(1) kinasema:

"Maswali yaweza kuulizwa endapo masharti yafuatayo yatazingatiwa: Kifungu 34(1)(d), swali halitahusu mambo zaidi ya moja na lisiwe refu kupita kiasi." Sasa wewe unatakiwa kuuliza swali sio unaanza kusema habari nyingine hizi, hairuhusiwi.

Halafu pia kifungu cha 35(1), katikati pale, kuuliza swali, swali linatakiwa kuulizwa kwa kutaja namba ya swali. Unasema: "Mheshimiwa Spika, naomba swali langu namba fulani lijibiwe." Ndio inavyotakiwa kuuliza sio kuanza habari fulani kwanza aah, aah.

Tunatumia dakika tano kwa kila swali, toka Waziri anaulizwa mpaka anajibu na maswali ya nyongeza. Tukianza tena habari nyingine zitakuwa zile zile ndio zinachukua *five minutes*.

Kwa hiyo, naomba tuzingatie hayo. Hakusema kwamba msitoe salamu za rambirambi wakati unapewa dakika zako kumi na tano za kujadili pale unaweza kabisa. Lakini wakati wa maswali na hii naiomba kabisa.

Hata yale maswali mnaanza sijui kuhusu mwanzo, historia, mnatumia muda, jibu swali ulilolulizwa.

Kwa hiyo, naomba hili tulizingatie kwa siku zijazo. Kwa hiyo, tusahihishe kwamba hakusema msitoe salamu za rambirambi wakati mnachangia hoja. Kwa sababu Bunge ni geni, hatujui hivi tunapopita katika Kamati ya Matumizi, wakati tunaingia katika Wizara kwa sababu huu ni mwanzo, hizi ni Wizara kama ya tatu tu, tunaposema mshahara wa Waziri na iwe ni Waziri sio watu wengine hawa *departmental heads.* Ndio maana tunapoanza *vote* mnasimama wengi, pale unaweza kusema Waziri mimi nilijadili hivi hukunijibu, Waziri atabidi akujibu tu. Unaweza kusema mimi nilikuwa na *issue* yangu nilipojadili hukuzingatia, unaweza kujibiwa pale. *(Makofi)*

Tukiondoka pale lazima iwe *specific*. Ukiingia kwenye Kitabu cha Nne cha Maendeleo ndio kabisa, tunazungumzia *project* fulani, sasa wewe ukiingiza nyingine mbona haina hela humu na kanuni zetu zinasema huwezi kuongeza pesa humu? Tunapitisha zile tulizopitia.

Kwa hiyo, tunaomba mtumie nafasi kujifunza. Kama una swali lako unajua kesho ni Wizara ya Kilimo anza kufikiria sasa wewe unataka kuuliza sehemu za namna gani kuliko kuwa tunakuzuia katika sehemu hii. Kwa hiyo, naomba tuelewane hivyo na mtumie muda kujifunza.

Baada ya kusema hayo, naomba kuahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.43 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 5 Julai, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*